ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake

37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Tatu – Tarehe 18 Juni, 2013

(Kikao Kilianza saa 3:00 za asubuhi)

Dua

Mhe. Naibu Spika, (Mhe. Ali Abdalla Ali) Alisoma Dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 66

Utaratibu wa Ajira katika Jeshi la Wananchi wa Tanzania (TPDF)

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Jeshi la Polisi na Jeshi la Wananchi wa Tanzania (TPDF) ni vyombo vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hufanya shughuli zake nchi nzima, kupitia fedha za walipa kodi wa nchi hii bila kujali rangi, kabila au jiografia ya mtu alipo. Kwa kuwa vyombo hivi vina kazi kubwa ya kulinda raia na mali zao sambamba na ulinzi wa nchi yetu pamoja na mipaka yake, na kwa kuwa kila Mtanzania mwenye sifa na uwezo anayo haki ya kupata ajira na hatimae kupata nafasi za kufanya kazi katika vyombo hivi.

(a) Ni utaratibu gani unaotumika katika kutoa ajira katika vyombo hivi.

(b) Je, kuna uwiano "*ratio*" maalum ya ajira baina ya Tanzania Bara na Zanzibar, baina ya Mkoa na Mkoa au baina ya Unguja na Pemba.

Mhe.Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kabla ya kujibu swali na mimi naomba niwashukuru vijana wetu waliokuja kutembelea katika Baraza hili la Wawakilishi. Vijana karibuni sana.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako na kabla ya kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 66 lenye vifungu (a) na (b), naomba kutoa maelezo yafuatayo.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli Jeshi la Polisi na Jeshi la Wananchi wa Tanzania ni vyombo vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na hufanya shughuli zake

nchi nzima kupitia fedha za walipa kodi wa nchi hii bila ya kujali rangi, kabila au Jiografia ya mtu anapotoka.

Pia ni sahihi kwamba vyombo hivi kwa pamoja vina kazi kubwa ya kulinda raia na mali zao sambamba na ulinzi wa nchi yetu pamoja na mipaka yake. Aidha, kila Mtanzania mwenye sifa na uwezo anayo haki ya kupata ajira na hatimae kupata nafasi ya kufanya kazi katika vyombo hivi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo;-

a) Mhe. Naibu Spika, kuweka utaratibu wa ajira kwa kila taasisi ni jambo la kawaida. Kwa upande wa vyombo vyetu vya ulinzi vya Jeshi la Wananchi na Polisi kuna utaratibu wanaoutumia katika kutoa ajira ikiwa ni pamoja na:-

1. Kuwa Raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwenye umri wa kati ya miaka 18-25.
2. Awe amefaulu vipimo vya afya na kuwa na tabia njema.
3. Awe na elimu isiyopungua Kidato cha Nne na amefaulu kwa kiwango kinachotakiwa.
4. Anatakiwa pia asiwe na matege, asiwe na upungufu wa vidole vya mikono, asiwe na makengeza pamoja na sifa nyengine zinazohitajika kwa sababu za kiulinzi.

b) Mhe. Naibu Spika, suala la ajira katika vikosi hivi limewekewa utaratibu maalum wa uwiano, kutokana na mahitaji ya askari wanaotakiwa kuajiriwa kila mwaka na pale yanapotokea mahitaji maalum. Hivyo, vyombo hivi vimeweka utaratibu wa kuhakikisha kunakuwepo na uwiano katika ajira za vikosi hivi kwa pande zote mbili za Muungano, ili kuhakikisha usalama wa nchi yetu na mipaka yake inalindwa.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya ndugu yangu Mhe. Waziri, naomba niulize swali moja dogo la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa chombo hiki kinaongozwa na kiongozi wake mkuu kwa upande wa jeshi ni (TPDF) na kwa kuwa Zanzibar kuna wapiganaji wengi ambao hawana matege, wana sifa ya kuwa majeshi na ni majeshi madhubuti, tangu zamani hivi sasa na mpaka baadae tumeshatoa majeshi madhubuti kama vile Brg. Yussuf Himidi na kadhalika.

(a) Je, Zanzibar imeshawahi kutoa Kiongozi Mkuu wa majeshi TPDF.

(b) Ikiwa haijawahi kutoa kiongozi huyo, na kwa kuwa vijana wetu wana sifa. Hii itakuwa kwamba vijana wetu hawana uwezo au ni sababu tu ya hawa ndugu zetu wa damu kutubagua au kutufanyia mambo mengine.

Mhe.Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kama alivyosema ni kweli kabisa kwamba wapo Wazanzibari makini, majemedari wana uwezo mkubwa sana kuongoza katika Jeshi la Wananchi wa Tanzania na wapo hivi sasa wana vyeo vikubwa katika jeshi hilo. Lakini kwa kuwa uteuzi huo ni mamlaka ya Rais wa Jamhuri ya Muungano ndio maana mpaka sasa haijatokea kwa TPDF kutokea upande wa Zanzibar. Lakini nasema siku zote kwamba haya ni baadhi ya matatizo yaliyojitokeza katika Muungano wetu na ndio maana tukaanza na mchakato mpya wa katiba kurekebisha mambo kama haya. Ni kweli upo umuhimu kwa Zanzibar pia kutoa TPDF ili kuongoza jeshi letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa hivyo sifa zipo kwa Wazanzibari kuweza kufanya kazi hiyo na naamini katika mchakato huu wa katiba utawepo utaratibu mzuri ili na Zanzibar iweze kutoa TPDF.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, ajira ni jambo linaloendelea na katika nchi hii na vijana wetu huajiriwa katika sehemu mbali mbali ikiwa ni pamoja na sehemu za ulinzi. Je, katika sehemu hii ya ulinzi vijana wanapotangaziwa kuwa kuna nafasi na wakienda kwenye usaili, huyo Afisa Tawala hutoa kauli ambayo huwa ni ya mwisho kwa baadhi ya wale asiowapenda na ikabidi kukosa haki yao, ni utaratibu umewekwa kwa makusudi au vipi.

Mhe.Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, ningeomba arudie swali lake hilo, sijamsikia vizuri na ningeomba aseme kwenye spika, kwa sababu bila ya kusema kwenye spika na akainamia tatizo la *echo* humu ndani bado lipo na lina matatizo.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Naibu Spika, swali ni hivi, inapotokea vijana wetu kuajiriwa huwa na utaratibu wao wa kufanya usaili na wale wanaofanikiwa ndio wanaopata hizo ajira kwa idadi inayotakiwa. Lakini katika sehemu hii ya ulinzi, mara nyingi Afisa Tawala huwa yumo katika wale watu wanaohusika na ajira ile, na hutokea wakati mwengine kauli yake ikawa ni ya mwisho kwa mtu kabla ya kufanyiwa usaili na kukosa haki yake. Je, huu ni mpango wa makusudi umewekwa.

Mhe.Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, nitajitahidi kulijibu swali lake, japokuwa sijalisikia na kulielewa vizuri.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba vyombo hivi vina utaratibu wake wa ajira na vinafanya hivyo kutokana na mazingira yake ya kiulinzi na usalama. Kwa hivyo, wanaweka utaratibu maalum katika ajira. Wale wanaoonekana baada ya usaili, hawana dosari na wametimiza vigezo hakuna sababu yoyote wasiajiriwe. Kufanyika jambo jengine lolote ni kinyume na utaratibu uliowekwa. Kwa hivyo, kama yapo malalamiko ya jambo hili na Mhe. Mjumbe ana ushahidi nao, basi atuletee rasmi serikalini ili tuyawasilishe kunakohusika na utaratibu ufanyike ili wananchi wote wapate ajira hii bila ya upendeleo wa aina yoyote.

Nam. 27

Uwekaji wa Taa za Barabarani

Mhe. Hassan Hamad Omar - Aliuliza:-

Kwa kuwa mji hupendeza kwa taa za barabarani, na kuwa kivutio kwa wakaazi wa mji huo pamoja na wageni wanaoingia, lakini kwa sasa ni muda mrefu taa za barabarani kwa mji wa Chake Chake na Wete haziwaki.

Je, ni lini taa hizo za barabarani zinatarajiwa kuwekwa katika mji huo wa Chake Chake

Mhe.Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 27 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, nakubaliana kabisa na Mhe. Mjumbe kwamba mji hupendeza kwa taa za barabarani na kuwa kivutio kwa wakaazi wa mji huo pamoja na wageni wanaoingia. Nakubaliana na yeye kwamba kwa muda mrefu sasa ni kweli kuwa taa za barabarani katika Mji wa Chake Chake na Wete haziwaki.

Sababu kubwa ya kutowaka kwa taa hizo ni yale matatizo tuliyokuwa nayo ya umeme katika Kisiwa cha Pemba. Nashukuru Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar imefanya mambo makubwa ya kupeleka umeme Kisiwani Pemba, kwa hivyo tatizo la umeme hilo *Alhamdulillah* sasa halipo. Lakini baadae tukagundua kwamba ile mitandao ya miji ile yote imekufa, waya na mabalbu vyote vimekufa na gharama zake zote ni kubwa. Baraza hili pia tulikuwa na deni la umeme kwa ZECO na hilo serikali imelisimamia kulilipa kila taasisi imetakiwa kulipa umeme unaostahiki.

Kwa hivyo, kwa sababu zote hizo tukaona kwamba tuje na mpango ule ambao tumeuanzisha Unguja wa *pilot project* wa umeme wa kutumia taa za *solar*. Mradi huu ambao umefanikiwa kwa kiwango kikubwa kwa majaribio katika mji wa Unguja, chini ya ufadhili wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China. Sasa serikali inaendelea na mazungumzo na ndugu zetu wa Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, ambapo miongoni mwa barabara zitakazofaidika na mradi huu ni taa za barabarani za mji wa Chake Chake kwa kuanzia, baadae tutakwenda miji mingine ya Pemba. Mradi huu *Inshaallah* maombi yakikubaliwa unatarajiwa kutekelezwa kwa mwaka huu wa fedha, ahsante.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa rafiki yangu mpenzi Mhe. Subeit Khamis Faki ana misemo yake anasema, *'cheo ni chema*' na jambo jema huigwa na sisi tumejifunza kutoka Unguja hii, kwa kuwa tunaona mji wa Unguja unapendeza kwa taa hizi za *solar power* alizozizungumzia Mhe. Waziri.

Je, Mhe. Waziri kwa sababu nchi hii ni ya visiwa, kuna kisiwa cha Unguja na kisiwa cha Pemba na sisi neema inayofuata hapa na kule itufikie. Ni lini taa hizo ziliwekwa Unguja na kule Kisiwani Pemba zitapelekwa ili mji wa Chake Chake na Wete uzidi kupendeza.

Mhe.Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema mradi huu kwa Unguja ulikuwa ni kama *pilot project*, yaani kama mradi wa majaribio kuona kwamba utafanikiwa vipi. Kwa bahati nzuri mradi umeonesha mafanikio mazuri sana. Sasa tukaona wenyewe, du! Kumbe kweli, kama unavyosema kwa nini tusingefanya hivi mapema.

Lakini tunawashukuru sana ndugu zetu wa Jamhuri ya Watu wa China walipokuja na wazo hili na limefanikiwa. Sasa kama nilivyosema maombi yetu tumejumuisha na miji mikuu yote ya Pemba. Kwa hivyo, nazidi kusisitiza kwamba maombi yetu yakienda kama tulivyoomba *Inshaallah* ndani ya mwaka huu wa fedha ujao miji ya Pemba nayo itang'ara, ahsante.

Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, naomba kidogo kutoa majibu ya nyongeza, ili ndugu zetu Waheshimiwa Wawakilishi pamoja na wananchi wa Pemba waweze kufahamu juhudi za serikali kuhusiana na taa za barabarani.

Mhe. Naibu Spika, mazungumzo tumeshaanza kwa ajili ya miji ya Pemba nayo, kama Mkoani, Wete na Chake Chake kuweza na wao kuwapatia taa

ambazo zitakuwa ni za *solar* kwa barabara za Pemba. Lakini kama unavyokumbuka Mhe. Naibu Spika, mji wa Unguja bado hatujaumaliza, tumo katika kufanikisha kumaliza ili tuanze na miji ya Pemba.

Kuna barabara inayotoka Hospitali ya Mnazi Mmoja kuelekea uwanja wa ndege, kuna barabara inayotoka Mwembeladu kuelekekea Amani, kuna barabara inayotoka Malindi kuelekea Saateni, kuna barabara inayotoka Kiembesamaki kuelekea Amani. Barabara hizi zinategemewa kumalizika kwanza wakati wowote kuanzia sasa taa zitakapokuwa zimewasili na baadae tutakwenda katika miji ya Pemba tukianzia na mji wa Chake Chake.

Mhe. Naibu Spika, kuna wengine wanataka tuanze na mji wa Mkoani. Lakini nataka niseme tu kwamba mazungumzo yetu ni mazuri na ndugu zetu wa China na hizi taa kwa kweli zina gharama, lakini kitakachotusaidia ni kwamba hatutokuwa na gharama kubwa ya uendeshaji, kwa sababu zinatumia jua. Nawaomba sana ndugu zangu kutoka Pemba katika mji yetu ya Pemba waendelee kuiamini serikali yao na tunatarajia kipindi chochote katika mwaka huu au mapema mwakani, basi na miji ya Pemba nayo itakuwa taa zinaanza kuwaka za njiani, ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Waheshimiwa Mawaziri wawili, ambapo majibu yaliyoongezwa na kaka yangu mpendwa Waziri wa Fedha, naomba niseme yafuatayo kabla la ya kuuliza swali langu.

Mhe. Naibu Spika, inaonekana kuna jambo ambalo Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi hakutuonesha kwamba ni maendeleo, ni kuweka barabarani kupitia Manispaa Zanzibar. Hili ni kusema kwamba Wawakilishi wanapoona jema basi husema hili ni jema na wanapoona baya vile vile ni wajibu wetu kusema.

Kwa hivyo, nampongeza kwa niaba ya watu wa Kiwani kwamba Dk. Mwinyihaji kwa niaba ya wizara yake amefanya jambo zuri kuweka taa za barabarani. Lakini naomba kujua kwamba kadiri ya mfumo huu wa *solar power*, tulikuwa tukitumia nishati ya umeme na ilikuwa na deni kubwa kama Mhe. Waziri alivyokiri.

a) Je, deni ambalo Manispaa ya Mji wa Zanzibar walitumia kuendesha huduma ya taa, limelipwa kwa kiasi gani ZECO na kama bado ni kiasi gani ambacho kimebakia na lini litalipwa.

b) Hii ni mpya na imetengenezwa na wataalamu kutoka nchini China. Je, baada ya mradi huu kukamilika ni vipi serikali imewaandaa watu wetu wa ndani kuweza kufanya matengenezo ya taa zile iwapo zitaharibika.

Mhe.Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, kwanza nikiri kwamba kweli Baraza la Manispaa wana deni kubwa la umeme, sikumbuki vizuri, lakini si chini ya milioni 200 ni fedha nyingi sana. Azma yetu ni kulilipa lote kidogo kidogo na tumekubaliana na Shirika la Umeme na wametukubalia, kwa sababu hili deni ni la muda mrefu, sio la jana au juzi ni la tokea nyuma huko. Lakini kama serikali na ilivyokuwa kama Mameya wanabadilika, lakini manispaa iko pale pale, au Wakurugenzi wanabadilika deni wamelirithi na tunachukua ahadi kwamba tutalilipa kidogo kidogo, tumekubaliana nao. Japo sasa hivi ndio tunatumia taa zile za *solar*, hatutokuwa na *bill* nyengine. Lakini deni bado tunalo na hilo tutalilipa Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu mafundi, huu mradi ulipokuja tulitumia mafundi wetu, wamefanya kazi nao. Hivi sasa wapo mafundi wawili ambao wanapatiwa mafunzo maalum ya kutengeneza hizo taa endapo zikiharibika. Mafundi hao wanafundishwa na Kampuni ile inayojenga hizi taa ni Kampuni ya ZTE. Kwa hivyo, mafundi wapo na wamepata mafunzo, hivyo kwa huduma ya kwanza wanaweza, hakuna tatizo lolote.

Nam 67

Ushajihishaji wa Serikali kwa Taasisi Binafsi kuhusu Kudhibiti Mabadiliko ya Tabia nchini

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 43

Tatizo la Ajira kwa Vijana wa Zanzibar

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: (Kny: Mhe. Viwe Khamis Abdalla) – Aliuliza:-

Kwa kuwa tatizo la ajira kwa vijana limekuwa kubwa sana na linaendelea siku hadi siku na vijana wengi wanaendelea kumaliza elimu ya juu Zanzibar.

Je, Mhe. Waziri ni lini Serikali itaacha tabia ya kuwaongezea mkataba wazee ambao wameshamaliza muda wao wa kuitumikia Serikali, wakati vijana wapo ambao wana elimu ya

kutosha kuweza kutumikia Serikali lakini fursa hizo huendelea kupewa wastaafu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 43 kama ifuatavyo.

Kwanza, nakubaliana na maelezo ya Mhe. Mwakilishi kwamba Zanzibar kama nchi nyengine Barani Afrika na ulimwenguni kwa jumla, inakabiliwa na tatizo la ajira na waathirika wakubwa wa tatizo hili ni vijana. Serikali inaelewa hali hii na kwamba hatua kadhaa zinachukuliwa na wizara mbali mbali kulitafutia ufumbuzi tatizo hili.

Pili, nataka nimkumbushe Mhe. Mwakilishi kwamba kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma Nambari 2 ya mwaka 2011 pamoja na marekebisho yake, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeondosha utaratibu wa ajira za mikataba kwa Watumishi wa Umma waliostaafu kazi isipokuwa kwa nafasi ambazo zinahitaji utaalamu, ujuzi na uzoefu maalumu ambazo zitatangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali.

Mhe. Naibu Spika, Baada ya maelezo hayo mafupi, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

Sababu za msingi za kutoa mikataba kwa wastaafu ni upungufu wa wataalamu wenye uzoefu katika baadhi ya sekta. Kifungu cha 8 cha marekebisho ya Sheria ya Utumishi wa Umma nambari 2 ya 2012 kimempa uwezo Waziri anayeshughulikia masuala ya Utumishi wa Umma, kuwa endapo ataona kuna upungufu wa utaalamu au ujuzi katika sekta fulani, atatangaza katika gazeti rasmi kada hizo kuwa adimu kabla ya tume husika kutoa kibali cha ajira ya mkataba.

Kwa hivyo, suala kwamba lini serikali itaacha kuwapa mikataba wataalamu wastaafu, ni hadi pale serikali itakapojitosheleza kwa wataalamu katika fani zote.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri, anaweza kutuambia ni sekta zipi ambazo zimeajiri wastaafu kutokana na kukosekana wataalamu, kwa vile tatizo hilo limekuwa ni sugu mawizarani.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, sekta ambazo zimeajiri wataalamu katika kipindi cha mwaka 2012/2013 ni sekta ya elimu, sekta ya afya, Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ofisi ya Rais Ikulu, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, na mimi kuniona ili nipate kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2012/2013 ni ajira ngapi za mkataba zilitoka.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Arejee swali.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, narudia swali kwa utaratibu kabisa. Mhe. Naibu Spika, naomba kumuuliza Mhe. Waziri kama ifuatavyo. Katika kipindi cha mwaka 2011/2012 na 2012/2013 ni mikataba mingapi ilitoka.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka 2011/2012 mikataba mitano ilitoka ya kuwaajiri wataalamu kwa njia ya mkataba wa miaka miwili. Katika mwaka 2012/2013 mikataba 28 imetoka kwa kuwaajiri wafanyakazi kwa njia ya mkataba na ajira zilizofanyika zilikuwa ni sawa na asilimia 1.1 ya mikataba yote ya ajira kulingana na idadi ya watumishi ambao wameajiriwa katika kipindi cha mwaka 2012/2013.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi tena ya kumuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa hivi sasa Zanzibar tunavyo vyuo mbali mbali ambavyo vinatoa elimu kwa vijana wetu, na kama tunavyowaona hapo juu vijana wetu wako tayari kusoma taaluma au fani yoyote ambayo serikali inahisi kwamba kuna mapungufu ya taaluma hizo kwa taasisi mbali mbali. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, swali langu ni kwamba serikali ina mpango gani wa kuanzisha masomo ya huo utaalamu ambao wazee wanao na vijana hawana, ili kuona kwamba bado serikali inawapa kipaumbele vijana badala ya wazee. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Naibu Spika, ikumbukwe kwamba serikali ilitoa nafasi 2552 kwa ajili ya kuwaajiri vijana wasomi wanaotoka vyuo tofauti kwenye kada mbali mbali kwa taasisi za umma. Kwa kweli mpaka sasa Wizara yangu imeshaajiri vijana 2519, hali hiyo inafanya kuzingatia wingi wa vijana na taaluma walizonazo na

ndio maana tumetenga hizo nafasi na mwaka huu pia itakuwa tumetenga hizo nafasi.

Vile vile kwenye Sheria yetu ya Utumishi wa Umma kama nilivyosema mwanzo inaruhusu pale inapoona kwamba kuna kada adimu, yaani *rare profession* kuzitangaza nafasi hizo na kuweza kuwaajiri kwa mkataba wazee ambao wenye ujuzi na sio kuwaajiri tu, wazee au wataalamu hao wanaoajiriwa wanatakiwa kufuata Sheria ya Utumishi wa Umma wa kufanya utaratibu wa kuwafundisha Uongozi na utaalamu unaohitajika kwa vijana ambao wameajiriwa.

Kwa hivyo, mkakati uliopo wa serikali ni kuweka mpango wa *succession plan* kwa ajili ya vijana wapya ambao wanaajiriwa. Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba hivi sasa kuna vijana 2519, ambao wameajiriwa kutoka vyuo vikuu tofauti hapa nchini na hawa wazee 28, ambao ni sawa na asilimia 1.1 ya vijana wote walioajiriwa kazi yao ni kuendeleza au kutoa mpango wa *succession plan* kuwafundisha vijana wapya wenye taaluma tofauti ambao wameajiriwa katika hizo nafasi ambazo wao tayari wanazifanyia kazi. *(Makofi)*

Nam. 61

Mgogoro Baina ya Msikiti wa Istiqama na Mtoni Chake Chake, Pemba

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Amani na utulivu ni suala muhimu sana, sio tu katika maisha ya kawaida lakini hata maendeleo ya taifa lolote, kwani bila utulivu hakuna maendeleo. Kwa kuwa hivi karibuni kumejitokeza ugomvi mkubwa baina ya Msikiti wa Istiqama Chake Chake na Msikiti wa Mtoni uliopo jirani, kwa ajili ya kugombania kiwanja kinachosadikiwa ni cha Wakfu. Kwa kuwa ugomvi huu umekuwa mkubwa sana kiasi cha kuhatarisha amani ya nchi, eti kutokana na Fat-wa iliyotolewa na afisi yako kwa mashirikiano na taasisi nyengine zilizopo chini ya wizara yako.

(a) Je, ukweli uko wapi katika kadhia hii.

(b) Hivi afisi yako pamoja na taasisi zake, ambazo zinaongozwa na watu wakubwa wanaoheshimika kweli imeshindwa kuridhisha pande zote mbili hizo na kuondoa ugomvi ule.

(c) Wafuasi wa msikiti mdogo wa Mtoni wana imani kuwa fat-wa ya Waziri wa Sheria kuwamilikisha Istiqama ardhi ile ni uonevu. Je, suala hilo ni kweli.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii na kabla sijajibu swali la Mhe. Mjumbe, naomba uniruhusu niwashukuru sana vijana wangu waliopo juu pale nawaombea kila la kheri, ili waweze kumaliza masomo yao ya sheria, kwa ajili ya kuja kuturithi maana yake sisi wengine tumeshakuwa wanasema saa ihda ashara, kwa sababu Mhe. Naibu Spika, mimi *degree* yangu ya mwanzo nilichukua mwaka 1975, kwa hiyo naomba wao waje watupokee mzigo huu.

Baada ya maelezo hayo napenda kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 61 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, amani ni mchakato na jitihada zisizokwisha katika maisha ya mwanadamu katika kufikia mahitaji yake ya lazima. Amani si hali ya kutowepo vita au tabia za fujo tu, bali inakusanya mambo yote yanayoifanya jamii iwe nzuri.

TAARIFA

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri azidishe sauti, ili niweze kumsikia vizuri wakati anapojibu swali langu.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante. Mhe. Waziri sauti haisikilikani na Waheshimiwa Wajumbe, hivyo ongeza sauti kidogo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake Nam. 61 kama ifuatavyo:-

Amani ni mchakato na jitihada zisizokwisha katika maisha ya mwanadamu katika kufikia mahitaji yake ya lazima. Amani si hali ya kutowepo vita au tabia za fujo, bali inakusanya mambo yote yanayoifanya jamii iwe nzuri. Kwa kweli jamii siku zote itakuwa nzuri iwapo kutakuwa na haki. Hivyo, kazi ya haki siku zote ni muhumi na ndio inayojenga amani.

Ni kweli kulitokezea mzozo au ugomvi baina ya uongozi wa Msikiti wa Istiqama na Msikiti wa Mtoni kugombania kiwanja cha Wakfu. Kwa kutambua hilo wizara yangu na taasisi zake zimechukua juhudi kubwa kusuluhisha ugomvi huu ikiwemo kuzungumza na pande mbili na

kuwashirikisha wadau mbali mbali kuleta suluhu, muafaka na maridhiano ili kufikia suluhisho la amani bila ya kukiuka haki na misingi ya sheria.

Baada ya utangulizi huo sasa naomba nijibu swali la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Eneo linalobishaniwa kwa mujibu wa *Wakfu Register* Nam. 6 ramani za mwaka 1962 ni Wakfu wa Nassor bin Khelef Al-Mauly ambalo lilikodishwa kwa *lease* serikalini kwa muda wa miaka 99 kuanzia tarehe 1/11/1915 kwa malipo ya Rupia 60 kwa mwaka na mkataba wa *lease* hiyo utakwisha tarehe 31/10/2014.

Ramani ya Wakfu huo Mhe. Naibu Spika, tunayo hapa, eneo la Msikiti wa Mtoni haliingii katika eneo la Msikiti wa Al-Mauly na eneo hilo ni Wakfu wa Bi Mwajuma wa mwaka 1962 pia ramani hiyo tunayo hapa.

Kwa kweli matatizo haya yote tuliwaeleza wahusika, lakini kuna wengine waliokubali na wengine kwa tamaa zao bado hawajakubali.

(b) Taasisi yangu imechukua juhudi kubwa na njia tofauti lakini suala la kuridhisha pande zote hilo ni jambo jengine. Tukiangalia katika historia hata Mitume mara nyingi hawakuwaridhisha watu wote hasa matamanio ya nafsi yanapowekwa mbele.

(c) Waziri hakuwamilikisha Msikiti wa Istiqama eneo hilo. Aidha *fat-wa* hailazimishi na inaweza kupingwa kwa mujibu wa taratibu za dini na sheria. Kwa hivyo, kama kuna mtu ambaye hakuridhika na maamuzi hayo, basi tunamuomba na sisi tulimuomba katika mikutano hiyo kwamba anaweza kwenda mahakamani.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa Mhe. Rais alipeleka tume ambayo na yeye Mhe. Waziri wa Sheria na Katiba na yeye alikuwemo pale kwa ajili ya kwenda kulichunguza hili tatizo la Mtoni.

Vile vile kwa kuwa kuna taarifa kwamba kulikuwa na *technical advice* ya kwamba ule msikiti uliopo pale usimamishwe, yaani sio kujengwa kwa tofali kuanzia chini, lakini uekewe nguzo ujengwe juu, yaani uwe umesimama kwenye nguzo na sio uanze *foundation* kwa chini. Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa *fat-wa* yao haiku-*regard* kitu hicho na ndio maana juzi kijiji cha Mtoni kikataka kughariki kwa mvua.

(a) Je, haoni *fat-wa* kama hizi zisizozingatia *technical advice* zinaweza kuleta madhara makubwa katika nchi.

(b) Kwa kuwa tatizo hili lilianza zamani na lilipaswa kudhibitiwa pale lilipoanza. Pia kuna msemo kwamba "tone moja la maji kama halikudhibitiwa linaweza kuleta gharika katika nchi".

Je, haoni Mhe. Waziri kuendelea kusema kwamba *fat-wa* hii ambaye hakuridhika apeleke Mahakamani na huku wananchi wakiendelea kulumbana na amani na utulivu itakosekana na litakalotokea pale serikali itabeba lawama. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, napaswa kusema kwamba taarifa ambayo anayo Mhe. Mjumbe si sahihi. Kwa kweli mimi binafsi ni mmoja katika Wajumbe wa Tume iliyoteuliwa na Mhe. Rais akiwemo Mhe. Ali Juma Shamuhuna, Mhe. Mwinyihaji Makame Mwadini pamoja na Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji. Kwa kweli tulitembelea hilo na tukawaita wahusika wote na tukawaelezea. Lakini zaidi ikumbukwe kwamba msikiti huu mkubwa wa Istiqama ulijengwa tokea enzi za Mhe. Dkt. Omar Ali Juma ambaye ni marehemu sasa.

Kwa hivyo, kama kuna kosa ambalo lilitokea kwamba ule msikiti haukujengwa na nguzo na hilo lilitokea tokea wakati huo na hivi sasa kwa hali ya msikiti ulivyo hatuwezi tena kusema msikiti uvunjwe, ili ujengwe msikiti wa miguu.

Jambo gani ambalo tulifanya, kwa kweli tuliwalazimisha Istiqama wachimbe msingi mkubwa ambapo tayari wameshafanya na nina hakika katika mvua hizi za juzi suala hilo halikutokea tena. Mhe. Naibu Spika, wakati huo kulitokea maji hayo katika mvua zilizopita na wala sizo hizi za juzi. Kwa hiyo, baada ya kuchimba msingi mkubwa maji hayo yote yaliopo pale yanakwenda katika maeneo mengine ya baharini na hilo ni la kwanza.

Pili kama nilivyosema kwamba waraka hizi zilizopo Msikiti wa Mtoni ambao baadhi ya watu ndio wanaoleta ugomvi, yaani Msikiti wa Mtoni haukufika kwenye Msikiti wa Istiqama kwa mujibu wa ramani hizi. Kwa maana hiyo, Msikiti wa Mtoni umefika pahala tofauti na Msikiti wa Istiqama, ukizisoma ramani hizi za tokea mwaka 1915 ramani hizi zinaonesha kwamba eneo walilojenga Msikiti wa Istiqama ni eneo la Al-Mauly na eneo lile lilikodishwa kwa serikali kwa *lease* ya miaka 99 na itamalizika mwaka 2014.

Mhe. Naibu Spika, hayo yote tuliwaelezea watu hawa na tukawafahamisha. Lakini kama nilivyosema mwanzo kuna watu wawili hata hapo Chake Chake

sio pao walikwenda tu wakakaa ndio wanaoleta vurugu hili. Sasa wakati tunafanya mkutano basi tulimuita hata Mkuu wa Polisi na yeye Mkuu wa Polisi aliwaambia, kwamba tunajua kwamba nyinyi ndio mnaofanya vurugu ambapo ni Ali Moh'd Ali na Ali Moh'd Khamis hawa ndio wanaoshika bango kuleta uchochezi ambao hauna maana.

Kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Mjumbe atizame au atafute *facts* zilivyo halafu aweze kueleza na sisi wakati tunayaelezea hayo nilikwenda mimi, Mufti Sheikh Saleh Omar Kaabi, Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Sheikh Abdalla Talib na wote wakaeleza misingi ya kidini pamoja na utaratibu wa wakfu hizi.

Kwa kweli wakati huo baada ya kuwauliza walikuwa hawana jawabu lolote, sasa kama baadaye ndio wanasema chokochoko hizo basi mimi sitoshangaa sana kwa sababu watu wenyewe hawa ni watu ambao wameweka tamaa mbele wanataka lazima kile wanachotaka wao kiwe hata kama ni kinyume na utaratibu wa sheria.

Mhe. Naibu Spika, kwa wizara yangu kwa kupitia misingi hiyo hatuwezi kuwamilikisha wao kitu ambacho si chao na wala hawana sheria kwenye suala hili.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

Mhe. Naibu Spika, suala la mgogoro wa Mtoni ni mgogoro mkubwa, ambao kipindi cha katikati kilipelekea kutishia amani ya nchi, kwa sababu hadi risasi pale Mtoni zililia, sasa si mgogoro mdogo kiasi cha kwamba kama Mhe. Waziri anavyotueleza.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa viongozi mbali mbali akiwemo hata Mhe. Rais katika kulitafutia ufumbuzi suala lile walitoa *fat-wa* kwamba kwa vyovyote vile mgogoro ule mwisho wake pande mbili zinazohusika zinufaike katika mgogoro ule ikiwemo msikiti pamoja na wananchi wanaolalamika wanufaike.

Sasa kwa kuwa Mhe. Waziri yeye binafsi pamoja na timu yake kama alivyoitaja wakiwemo Mufti pamoja na watu wengine walikwenda pale kwa ajili ya kulitafutia ufumbuzi suala lile.

(a) Je, ni yepi yaliyokuwa maazimio ya kikao kile kilichomshirikisha Mufti. *(Makofi)*

(b) Ni kwa kiasi gani Mhe. Waziri binafsi amefuatilia utekelezaji wa maagizo ambayo waliyoyatoa katika kikao kile. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, kwanza katika pande mbili zile kuna wakfu wa Bi Mwajuma ambao Msikiti wa Mtoni upo, yaani wakfu wa Bi Mwajuma umetumiwa na watu hawa wa Msikiti wa Mtoni bila idhini na katika kuwanufaisha, kwa sababu huu ni wakfu na wao wengine wamejenga nyumba na mambo mengine.

Sasa katika kuwanufaisha sisi Wizara tutasamehe ule uchukuaji wa ardhi ya wakfu kwa nguvu na tutawamilikisha wao kwa gharama ndogo sana. Kwa mfano, kiwanja leo Mtoni kinaweza kufika milioni 5 au 10, lakini mtu aliyejenga pale ili kumhalalishia apate kutumia kiwanja hicho hapa na apate mambo mazuri huko akhera, kwa sababu akienda kama amechukua wakfu wa watu atapata matatizo. Kwa hivyo, tumesema kwamba bei ile tunaiondoa na itakuwa ni bei ndogo katika kiwanja kile na hicho ni kitu kimoja kizuri ambacho tumefanya.

Pili ni kwamba katika suala hili hakuna maazimio tuliyotoa kuwa wafanye hivi na vile, isipokuwa ni makubaliano na makubaliano hayo ni bahati mbaya Mhe. Mwakilishi alikuwa hayupo, lakini Mhe. Mbunge alikuwepo na yeye alichukua nafasi kubwa ambaye ni Mbunge wake alichukua nafasi kubwa ya kulizungumzia suala hili na Mhe. Mwakilishi aliporudi mimi binafsi nilimuelezea hatua tuliofikia.

Sasa kama kuna watu ambao bado wana matatizo habari hiyo mimi sijaipata na kila nikienda naona watu wanajenga kwa mujibu tulivyowaambia kwamba Msikiti wa Istiqama wanachimba msingi. Kwa hivyo, kama kuna matatizo hilo ni geni kwangu mimi na ninaomba Mhe. Mwakilishi anipe taarifa, ili niweze kulifuatilia. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Naibu Spika, baada ya majibu mazuri sana ya Mhe. Waziri naomba kwanza nitangaze maslahi yangu kwenye eneo lile, kwamba mimi nimeoa pale chini ya ule msikiti ambao unagombaniwa. *(Makofi)*

Kwa hivyo, natangaza wazi maslahi yangu katika eneo lile nisije nikaambiwa nimekiuka utaratibu. *(Vicheko)*

Mhe. Naibu Spika, wakati wowote ambapo mgogoro huu ulikuwa unatokezea mimi nilikuwa nipo kwenye eneo lile ingawa sikuwa ni mhusika wa mgogoro ule, yaani naelewa kila kitu ambacho kilikuwa kikifanyika na wakati

mwengine walikuwa hunionesha zile taarifa ambazo wananchi wa Mtoni wanadai kwa hoja ya msingi.

Mhe. Naibu Spika, wananchi wa Mtoni ambao wanadai ile haki wameandika barua sehemu nyingi ikiwa ni pamoja na kusambaza barua kwa Waheshimiwa Wawakilishi wengi na zipo Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Waziri alisema kwamba wapo baadhi ya watu waliokubali hoja ya serikali kwa upande wa Mtoni. Lakini wananchi wa Mtoni wanathibitisha kwamba hao waliokubali walikubali baada ya kugaiwa vifaa kama vile mchele na mafriji.

(a) Je, Mhe. Waziri anasema vipi kwamba wale waliokubali hoja ile ya serikali ni kwamba baada ya kugaiwa mchele kupitia Masheha wa eneo lile ambapo mimi mwenyewe nilikuwa ni mkaazi wa eneo lile.

(b) Mhe. Waziri anasema kwamba Msikiti wa Mtoni haukufika kwenye Msikiti wa Istiqama. Kwa hivyo, ni vyema akatuambia ni msikiti upi ulioanza mwanzo na Msikiti wa Mtoni una miaka zaidi ya 80 na Msikiti wa Istiqama una miaka si zaidi ya 20, kwa nini ajenge hoja kwa Msikiti wa Istiqama ambao uliojengwa juzi wakati Msikiti wa Mtoni una miaka zaidi ya 80.

(c) Mhe. Naibu Spika, kwa nini kwenye haki kama ile ya kidini serikali itumie vyombo vya dola kuwatisha wananchi na kuwatia ndani wananchi, ambao wanadai haki ya kidini ambapo sheria inawaruhusu katika hili

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Naibu Spika, ni kweli Msikiti wa Mtoni mdogo ni zaidi ya miaka 80 na Msikiti wa Istiqama hauzidi miaka 20. Lakini napenda ajue Mhe. Mwakilishi kwamba Msikiti wa Mtoni ulijengwa katika Wakfu wa Bi Mwajuma na Wakfu wa Bi Mwajuma huu uko kwa mujibu wa ramani ya mwaka 1961.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema wakfu huo au ramani hiyo ninayo hapa. Sasa ramani hii ya mwaka 1961 haikuingia katika ramani iliopo ya mwaka 1915 ya Al-Mauly, ramani ya Al-Mauly kiwanja cha msikiti kimo ndani ya ramani hiyo. Kwa hivyo, hata kama Msikiti wa Istiqama umejengwa jana, basi utakuwa unajengwa kwenye ramani au Wakfu wa Al-Mauly na hawa watu wa Mtoni ambao Msikiti wao ulijengwa zaidi ya miaka 80 ni kweli, lakini haukufika Wakfu huo humo na ramani hizi ni *survey* iliyofanywa miaka ya 1913, 1914 na 1915 na serikali hizi tumezichukua katika ofisi za *survey* ya serikali.

Kwa hivyo, ni uhakika kwamba Msikiti wa Mtoni hauhusiani na Msikiti wa Istiqama, lakini hawa watu wa Mtoni walikuwa hawajui baadhi yao na tulipowapelekea hizi ramani wengi wao wakakubali isipokuwa hawa wawili ambao niliowataja, yaani Ali Moh'd Ali na Ali Moh'd Khamis hawakuzikubali ramani hizi. Sasa sisi tuliwaambia kama hamzikubali ramani hizi ambazo si zetu ni za serikali basi waende mahakamani na hicho ni kitu rahisi kama hicho na wala hawajaenda.

Mhe. Naibu Spika, sisi bado tuliwaambia kama kuna matatizo hayo ya maji, kwa sababu kujengwa kwa Msikiti wa Istiqama kulikuwa na matatizo ya maji, sasa baada ya kujenga wao wakati mvua inaponyesha kwa kuwa kuna milima maji yanatuwama na yanakuwa ni mengi. Kutokana na hali hiyo, tukawalazimisha Msikiti wa Istiqama lazima wachimbe msingi mkubwa, ili maji yale yote yapite yaende baharini na hilo tayari wameshafanya.

Kwa nini vyombo vya sheria vikatumia nguvu. Kwa kweli sababu kubwa ni kulinda amani, kwani huyu Ali Moh'd Ali akishirikiana na Ali Moh'd Khamis waliwashawishi mpaka watoto wadogo kwenda kuvunja pahala ambapo si pao. Sasa Polisi walipoona hivyo ikabidi lazima walinde amani, lakini amani hiyo ilikuwa ni kwa usalama na utulivu wala hakuna mtu aliyedhibitiwa.

Vile vile siku tuliyofanya mkutano pamoja na Ali Moh'd Ali na Ali Moh'd Khamis, Mkuu wa Polisi wa Kusini Pemba na yeye alimwambia kwamba tunajua ushawishi unaofanya kwa watu je tukutie ndani, alinyamaza kimya. Sasa ikifika *stage* mtu kama huyo anawashawishi watu makusudi kufanya fujo na vyombo vya serikali vinasaidia kutatua matatizo hayo, mimi nahisi ilikuwa ni suala sahihi na ni jambo zuri la kufanya haya tuliyofanya.

Mhe. Naibu Spika, nasema kama bado kuna mtu anahisi eneo ambalo amejenga Istiqama si lao, basi aende mahakamani kwa sababu hizi ramani mbili za wakfu zitaeleza mahakamani. Lakini bado nasema Msikiti wa Mtoni haukufika kwenye Msikiti wa Istiqama na hiyo ni kwa mujibu wa ramani hizi za serikali.

Nam. 35

Uboreshaji wa Biashara za Viungo

Mhe. Hassan Hamad Omar – Aliuliza:-

Zanzibar inasifika sana kwa biashara ya viungo hadi kufikia kuitwa (*Spice Island*) na viungo ni sehemu ya mazao ya biashara (*commercial crops*) yanayoongeza fedha za kigeni.

(a) Je, serikali inapata pato kiasi gani kwa mwaka kutokana na kuuza mazao hayo.

(b) Je, zao la pilipili hoho ambalo ni maarufu hapa Zanzibar lina nafasi gani katika kuinua uchumi na pato la Zanzibar.

(c) Je, serikali inayaboresha vipi mazao ya viungo.

Mhe. Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko – Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 35 lenye kifungu (a), (b) na (c) kwa kuanza na utangulizi kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ni suala linaloeleweka kwetu sote kwamba Zanzibar inasifika kwa biashara ya karafuu na viungo vyengine hadi kuitwa "*The Spice Island*". Miongoni mwa viungo ambavyo vinapatikana tukiacha karafuu ambayo sote tunaifahamu ni pamoja na tangawizi, hiliki, mdalasini, pilipili hoho, pilipili manga, na kadhalika.

Mnamo miaka ya 1980 serikali ilifanya mabadiliko ya Sera yake ya Biashara na uendeshaji uchumi, ambapo sekta binafsi iliruhusiwa kushiriki katika biashara na shughuli za kiuchumi. Baadhi ya shughuli za ununuzi wa mazao ya kilimo kama vile nazi, ndimu, pilipili na viungo vyengine yaliruhusiwa kuendeshwa na sekta binafsi isipokuwa zao la karafuu. Ufanisi katika uzalishaji wa mazao hayo, kwa bahati mbaya sana ulishuka na hivyo kuathiri uzalishaji.

(a) Serikali kwa sasa inapata mapato yake kutokana na zao la karafuu pekee.

(b) Bado zao la pilipili hoho ni miongoni mwa mazao ya viungo ambayo yana nafasi ya kuinua uchumi wa Zanzibar. Hata hivyo, kama ilivyo kwa biashara ya viungo vyengine biashara ya pilipili hoho inaendeshwa na wafanyabiashara wadogo wadogo katika soko la ndani na kwa watalii wanaofika Zanzibar.

(c) Serikali kupitia Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko inaendelea na utafiti wa kutayarisha mkakati wa kibiashara utakaowezesha karafuu na bidhaa nyengine zikiwemo za viungo kuuzwa katika masoko ya kimataifa kwa kutumia alama maalum (*Branding*). Alama hiyo ambayo itakuwa imelindwa kwa mujibu wa Sheria za Kimataifa itawezesha kuifanya karafuu na mazao mengine ya viungo kuuzwa kwa thamani kubwa na kudhibiti mwenendo wa biashara.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko naomba kumuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Naibu Spika, kama alivyokiri kama ni kweli Zanzibar ilisifika sana kwa biashara hii ya viungo na kwa sasa tumeona muelekeo unapotea. Je, kama Waziri anayehusika na mambo ya biashara amejipanga vipi kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo katika kuhamasisha zao hili kuimarika zaidi.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, nimejibu katika suala la msingi kwamba Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko tumo katika kutayarisha mkakati wa kibiashara ikiwemo kuandaa hii alama maalum *branding.*

Mhe. Naibu Spika, nakumbuka katika ziara zetu wakati tukitembelea sehemu ya uzalishaji wa mazao ya viungo tumekuta Wizara ya Kilimo kwamba imehamasisha sana wakulima kuendelea kulima mazao ya viungo. Naamini kwamba wakulima wamehamasika na tukifanikiwa katika mkakati huo Wizara ya Biashara katika kuwatafutia soko la uhakika basi Mwenyezi Mungu atawajaalia tutapata soko na mazao haya yataongezeka katika uzalishaji wake.

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza.

a) Mhe. Naibu Waziri katika jibu lake mama alisema kwamba pato linapatikana kwa sasa hivi ni zao la karafuu. lakini je, Mhe. Naibu Waziri unaelewa kwamba sasa hivi karafuu sehemu nyingi inaanza kutoweka.

b) Na jitihada gani zitaanza kufanyika ili karafuu ile iweze kurudi na kuendeleza pato zaidi. ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, serikali inafahamu kwamba mikarafuu mingi imezeeka na mingi imekatwa kwa ajili ya kutengeneza makaa na ndio maana jana wakati najibu swali moja niliulizwa, nilisema kwamba Wizara ya Kilimo inafanya utafiti wa kuongeza uzalishaji wa zao hili la karafuu. Kwa kuwa tunaamini kwamba zao la karafuu linachangia kwa kiasi kikubwa sana katika pato la nchi yetu.
Hiyo ndio jitihada inayochukua na serikali kuhakikisha kwamba mkarafuu unafanyiwa utafiti ili kuongeza wingi wake lakini pia kuongeza uzalishaji wa karafuu.

Mhe. Farida Amour Moh'd: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi na mimi ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali dogo la nyongeza.

Mhe. Naibu Waziri kwa kuwa wananchi wanajitahidi sana katika kilimo cha bidhaa za viungo lakini hukosa ujuzi ya taaluma ya kusarifu bidhaa hizo.

a) Je, ni lini wizara yako itajitahidi kutoa taaluma ya usarifu wa bidhaa hizo.

b) Na lini itafanya maarifa ya kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya usarifu wa bidhaa hizo ikiwa ni pamoja na kupata vifunganisho vya bidhaa hizo muhimu.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, nimesema kwamba Wizara ya Kilimo wakati tunatembelea katika mashamba tumeona jinsi walivyohamasisha wakulima katika kuongeza jitihada za kuzalisha mazao ya viungo. Lakini sote ni mashahidi kwamba bidhaa hizi za viungo zinafunganishwa si vizuri sana, lakini katika utaalamu fulani wa kuvutia sana watalii kwa kuashiria vinawekwa kama kwenye vikapu fulani kuonesha uasilia wa Kizanzibari, lakini kutokana na upungufu wa mazao yenyewe ya viungo ndio maana utaona kwamba viungo hivyo havionekani kwa wingi sana sokoni.

Mhe. Naibu Spika, kwa kulitambua hilo ndio maana Wizara ya Kilimo inaendelea kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa mazao hayo. Lakini kwa ujumla wake Wizara ya Biashara imeshajipanga katika kuwaelimisha wafanyabiashara wadogo wadogo ili mazao yao yaweze kukubalika katika soko la kimataifa, basi miongoni mwa mambo yanayohitajika katika kufikia viwango ni pamoja na suala zima la ufunganishaji unaokubalika wa bidhaa zao wanazozalisha ikiwemo hizi bidhaa za viungo.

Nam. 142

Wafanyakazi wa Majumbani na Kumbi za Burudani Zanzibar

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Serikali kila baada ya muda imekuwa ikipanga viwango vya mishahara ya kima cha chini katika sekta binafsi lakini waajiri wa majumbani na katika nyumba za burudani wamekuwa hawazingatii viwango hivyo vya mishahara.

a) Je, kwa nini wafanyakazi wa majumbani wanaendelea kulipwa viwango kinyume na vilivyopangwa na serikali na wengine mshahara wao ni chakula na usingizi.

b) Je ni waajiri wangapi wamechukuliwa hatua za kisheria kwa kulipa mishahara kinyume na viwango vya mishahara vinavyopangwa na serikali.

c) Kutokana na wafanyakazi wa kumbi za burudani kulipwa mishahara duni, serikali haioni kuwa ndio chanzo cha wanawake kujiuza kutokana na ukali wa maisha.

d) Je, maeneo mangapi ya kazi yamekaguliwa katika mwaka jana kuona haki za wafanyakazi zinazingatiwa vipi hasa kwa wafanyakazi wa majumbani na kumbi za burudani visiwani.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika - Alijibu:-

Mhe, Naibu Spika, kwa idhini yako napenda kumjibu swali Nam. 142 Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo. Kabla ya kujibu vipengele (a), (b), (c) na (d) ya swali hilo napenda kutanguliza maelezo yafuatayo.

Mikataba ya kazi ya kimataifa na sheria zetu za kazi za Zanzibar zinasisitiza juu ya kuimarisha mahusiano mema na majadiliano ya pamoja katika sehemu za kazi kupitia vyombo vya utatu. Vyombo hivi vya utatu vinavyoundwa na wajumbe sawa kutoka serikalini, Jumuia ya Waajiri na Shirikisho la Vyama hivyo vya Wafanyakazi. Kwa upande wa Zanzibar ni pamoja na Bodi ya Ushauri ya Mambo ya Kazi, Bodi ya Ushauri ya Mishahara, Kamati ya Utatu na Kamati ya Usalama wa Afya na Usalama kazini. Lengo kuu la vyombo hivi ambavyo vyote vinakutana kwa mujibu wa sheria ni kutoa fursa ya kujadili matatizo ya wafanyakazi ikiwemo ulipaji wa mishahara na kushirikiana katika kutatua matatizo haya.

Aidha iwapo matatizo hayo yameshindikana kwa utaratibu wa sasa, mlalamikaji anatakiwa kuwasilisha malalamiko yake katika kitengo cha usuluhishi, matatuzi ya migogoro ya mambo ya kazi kilichopo Wizara ya Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika na sio tena Mahakama kama ilivyokuwa hapo awali.

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo napenda sasa kujibu vipengele (a), (b), (c) na (d) vya swali la Mheshimiwa kama ifuatavyo:-

a) Serikali imetangaza viwango vipya vya mishahara kwa sekta binafsi na vimeanza kutumika mwezi wa Februari mwaka 2012. Viwango hivyo vilihusisha pia wafanyakazi wa majumbani ambao kwa mujibu wa viwango vipya wanastahiki kulipwa Sh. 60,000/- kwa mwezi. Serikali haijatangaza kuwa chakula na usingizi ni sehemu ya mshahara wa wafanyakazi wa majumbani.

Mhe. Naibu Spika, inawezekana kwamba bado kuna changamoto katika utekelezaji wa agizo hili la serikali na changamoto hii inasababishwa na mambo mengi ikiwemo kwa waajiri na wafanyakazi hawa wa majumbani ni watu binafsi na sio taasisi kama ilivyo kwa wafanyakazi wengine tukiwemo sisi Waheshimiwa Wawakilishi.

Aidha wafanyakazi wengi hawajajiunga na Chama cha Wafanyakazi kinachotetea maslahi ya wafanyakazi wa majumbani. Mhe. Naibu Spika kama wapo wafanyakazi wa majumbani ambao wanalipwa kinyume na kiwango kilichotangazwa na serikali napenda kuchukua fursa hii kuwashauri wafanyakazi hao kufungua mashauri katika kitengo cha usuluhishi na uamuzi wa migogoro ya mambo ya kazi kilichopo wizarani

b) Jumla ya malalamiko 15 yanayohusiana na madai ya kulipwa kiwango kidogo cha mshahara yameripotiwa katika ofisi zetu za Mikoa na Kitengo cha Usuluhishi na Uamuzi wa Migogoro ya Mambo ya Kazi kuanzia Juni hadi kufikia mwezi Machi mwaka huu. Kati ya malalamiko hayo malalamiko 11 yamemalizika na waajiri kuamuriwa kuwalipa mishahara halisi na tofauti iliyopo kwa mujibu wa sheria na malalamiko manne yanaendelea kusuluhishwa kupitia kitengo cha Usuluhishi na Uamuzi wa Migogo ya Mambo ya Kazi.

Aidha waajiri wawili walifikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Mwanakwerekwe baada ya kukaidi kutekeleza amri waliyopewa na Kamisheni ya Kazi ambayo pamoja na mambo mengine imehusu Malipo ya Mishahara.

c) Si sahihi kwamba mshahara duni unaweza kuwa ni sababu ya wafanyakazi wa kike hufanya mambo yasiyokuwa na maana kama anavyodai Mhe. Mwakilishi. Serikali kwa upande wake imeongeza mishahara katika sekta binafsi, ongezeko la zaidi asilimia 100 ili kuwapunguzia ukali wa maisha wananchi wake. Matatizo haya ya kujiuza kwa wafanyakazi wa kike hususan katika kumbi za starehe pamoja na mambo mengine yanachangia kuporomoka kwa maadili

na kutofuata maadili, silka na utamaduni wetu pamoja na tabia ya mtu binafsi.

Ni vyema Waheshimiwa Wawakilishi tukatumie ushawishi wetu tulionao katika majimbo yetu kwa kuwajulisha wananchi wetu hususan vijana, kuendelea kulinda mila, silka na utamaduni wetu ili vijana wetu wasijiingize katika matendo mabaya yakiwemo haya ya watoto wa kike kujiuza.

d) Jumla ya sehemu za kazi 289 zimefanyiwa ukaguzi wa kazi hadi kufikia mwezi Machi mwaka 2013 ili kuhakikisha kwamba waajiri na wafanyakazi wanatimiza wajibu wao kwa mujibu wa sheria za kazi. Katika ufunguzi huo wafanyakazi wamekumbushwa juu ya haja ya kutimiza wajibu wao wakiwa kazini kuweza kuwajibika ili kuongeza tija. Aidha waajiri nao kwa upande wao wamekumbushwa juu ya haja ya kuzingatia haki za wafanyakazi na wajibu wao katika kuimarisha mahusiano mema kazini kwa mujibu wa sheria za kazi.

Aidha napenda kuwakumbusha Waheshimiwa Wawakilishi kwamba Shirika la Kazi Duniani (ILO) katika kikao chake kilichofanyika mwaka 2011 kilipitisha mkataba Nam. 189 juu ya kazi za heshima kwa wafanyakazi wa majumbani *(Decent work for domestic workers)*. Kupitishwa kwa Mkataba huo inatoa fursa kwa nchi wanachama wa shirika hilo kuridhia mkataba huo ili hatimae kazi za majumbani zitambuliwe kuwa ni kazi za heshima na rasmi.

Hatua hiyo pia itawekwa utaratibu wa kufanya ukaguzi wa kazi katika maeneo ambayo wafanyakazi hao wanafanya kazi ikiwa katika majumba yetu. Naomba tuwe na subra ili nchi yetu iridhie mkataba huo na hatimaye kuanza kutekelezwa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante pamoja na majibu marefu sana ya Mhe. Waziri naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Baada ya serikali kupanga viwango vya mishahara, ni chombo gani kilichosimamia utekelezaji wake kati ya muajiri, Chama cha Wafanyakazi na Serikali.

(b) Kuna faida gani kwa serikali kuendelea kupanga mishahara katika sekta binafsi wakati wahusika hawanufaiki na viwango hivyo pamoja na maslahi mengine kama vile matibabu, fedha, likizo na michango ya mafao yao hasa wafanyakazi wa majumbani.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Naibu Spika, chombo ambacho kinahusika kufuatilia kwa kweli hili ni jambo ambalo kama nilivyosema la utatu, sisi wenyewe kama ni wa Wizara husika, waajiri wenyewe lakini na wafanyakazi wenyewe. Lakini kwa ujumla udhamini na usimamizi mkuu uko chini ya Wizara ya Kazi kwa kushirikiana na waajiri.

Kwa hivyo sote tuna wajibu wa kufuatilia, tumegundua kweli kuna matatizo lakini nimesema kwa sababu jambo hili bado mkataba wake hatujauridhia kwa asilimia 100 mpaka sasa hivi tumo katika taratibu za kuuwasilisha katika vyombo vinavyohusika, tuwe na subra kidogo, hatimae utakapokuwa rasmi tumeshautambua na tumeuridhia mkataba ule basi maeneo yote ambayo yana wafanyakazi wa majumbani watafuatiliwa na kuhakikisha kwamba taratibu zote za kisheria na haki zao wanapatiwa.

Vile vile serikali pamoja na kwamba ina wajibu huo, lakini mtekelezaji wa masuala haya kama nilivyosema sio la serikali peke yake na sisi kama ni serikali tuna wajibu wa kuwafikia wafanyakazi wa majumbani na wafanyakazi wengine. Hili lipo kwa upande wa utumishi wa umma. Pia serikali imetangaza viwango mbali mbali vya mishahara na sisi kwa upande wa sekta binafsi tuna haki ya kufanya hivyo. Kutotekeleza sheria haitozuia serikali isiendelee kutangaza viwango vipya vya mishahara.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Baada ya majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba nimuulize swali la nyongeza.

Kwa kuwa wafanyakazi hawa huanza kazi wakiwa na umri mdogo na baadae huzeeka na wakashindwa kufanya kazi.

(a) Je, utaratibu upi uliowekwa ili wafanyakazi wa majumbani waweze kujiunga na Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (ZSSF) ili wanapozeeka wapate hifadhi ya maisha yao.

(b) Je, serikali kupitia Wizara ya Afya inaratibu vipi ili kuona kuwa wafanyakazi wa majumbani hawanyanyaswi, hawalipwi mishahara midogo na hawaachishwi kazi kiholela.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Naibu Spika, muajiri yoyote kwa mujibu wa taratibu za sheria zetu za hapa Zanzibar ana wajibu wa kujiwekea huduma yake ya jamii au mafao yake ya baadae kwa mujibu wa sheria zetu zilivyo.

Mara sisi suala hili ambalo litakapokamilika taratibu zetu tutahakikisha wafanyakazi wa majumbani na wengine hata wale wanaofanya sekta binafsi basi mafao yao wanapeleka katika taasisi ya Huduma za Jamii.

Suala zima la kupambana na unyanyasaji sikatai kwamba kuna unyanyasaji na kuna kesi ambazo zimewahi kuletwa basi Wizara imezishughulikia kikamilifu kuzifuatilia. Imezifanyia kazi na hazifanyiwi hapa Zanzibar tu hata wale Wazanzibari wanaofanya kazi nje vile vile tumepata kesi kama hizo. Tumechukua hatua za kufaa kushirikiana na Ofisi zetu za Kibalozi zilizokuwepo nje. Kwa hapa Zanzibar zile kesi ambazo zimeripotiwa tumechukua hatua za kufaa.

Na natoa wito kama kuna wafanyakazi majumbani ambao wananyanyaswa, wanatukanwa na pengine kupigwa na hatimaye kufanyishwa kazi kama hizo basi waje Wizarani pale mara moja kwenye kitengo chetu cha Usuluhishi wa Migogoro, hatua zinazohusika zitachukuliwa.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa nimuulize Mhe. Waziri swali la nyongeza.

Kwanza namshukuru sana Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri na amejibu kwa ufasaha na ametueleza kinagaubaga tumefahamu moja baada ya moja. Lakini napenda nimuulize Mhe. Waziri kwa sababu suala kubwa lililokuja la matatizo ya waajiri kutotoa mikataba kwa wafanyakazi. Suala hili tulilizungumza sana Mhe. Waziri akatoa wito kama wafanyakazi wote wajaze mikataba kwa sababu wanapokua hawana mkataba ndio wanakosa haki zake.

Sasa napenda nimuulize Mhe. Waziri kwa sababu suala hili yeye ndiye muhusika mkuu, amepita sehemu ngapi za kazi ameona kwamba waajiri wanawapa mikataba waajiriwa wao. Kwa sababu ilikuwa ni matatizo makubwa na walikuwa hawataki kutoa hiyo mikataba, sasa yeye amefuatilia sehemu ngapi na kuona kwamba mikataba wanapewa waajiriwa.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Naibu Spika, swali lake ni la maana sana kwa sababu mfanyakazi yoyote kabla ya kuajiriwa anahitajika kuwa na mkataba kati ya muajiri na muajiriwa. Kama nilivyosema katika jibu langu la msingi kwamba nakamilisha taratibu za kuuridhia ule mkataba wa haki za wafanyakazi wa majumbani. Mara baada ya kukamilishwa taratibu hizo hata *draft* ya mikataba hiyo tayari tunaanza kuitayarisha ili kuipeleka kwa Mwanasheria Mkuu.

Kwa hivyo suala hilo likishapitishwa rasmi tutahakikisha kwamba mikataba inajazwa kati ya muajiri na muajiriwa kwa mujibu wa taratibu za sheria ambazo serikali itaweka.

HOJA ZA SERIKALI

Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe jana tulikuwa na wachangiaji 13 na tumechangia asubuhi na jioni. Leo tuna wachangiaji 20, sasa tungelipenda tugawane tuweze kumaliza sote asubuhi na jioni. Kwa hivyo mtu asirejee aende kwenye *point* kama shukurani zimeshatolewa nyingi. Mtu aende moja kwa moja ili muda wake autumie vizuri.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Mhe. Naibu Spika, ahsante na mimi kunipa fura hii ya kuweza kuchangia mchango wangu mchache katika hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kuhusu mpango wa maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii lakini pia nataka nichukue fursa hii japo kuwa umesema kwamba tusipongeze lakini haiwezekani Mhe. Naibu Spika, ni lazima tumpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa juhudi kubwa waliyoichukua wakakaa kitako na wakatuletea vitabu hivi visivyopungua vitatu, ni kazi kubwa sana kwa hivyo hatuna budi kuwashukuru sana na kuwapongeza kwa kazi yao hii. Mwenyezi Mungu awajaalie mafanikio mema.

Mhe. Naibu Spika, katika bajeti hii ya serikali kwanza mimi naomba niseme kwamba bajeti yetu ya serikali ina changamoto kwa upande mmoja. Changamoto hii ndiyo inayosababisha kuona kuwa bajeti kuu ya serikali haiwafikii wananchi mmoja mmoja. Kwa sababu Mhe. Waziri anapotuletea kitabu chake cha bajeti ya serikali, akatupangia mipango ya mapato, matumizi ya serikali. Lakini changamoto inayojitokeza ni kuwa fedha hizi hazifiki kwa mawizarani katika mpango mzuri. Hii ni moja ya changamoto ambayo kuwa serikali inawakabili.

Kwa hivyo tungemuomba Mhe. Waziri kile alichokitangaza hapa kwa niaba ya serikali basi kifikie katika mawizara kwa wakati unaofaa. Mnapokwenda katika mawizara Mhe. Naibu Spika, utazikuta wizarani changamoto nyingi za

mwaka jana, mwaka juzi ni hizo hizo haziondoki. Ukiziuliza tatizo ni nini unaambiwa bajeti finyu. Lakini hata hivyo finyu haifiki kwa ule wakati unaokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, niende katika Wizara, utakuta kuna asilimia 45, 50, ambapo tulitegemea angalau tumeshafika katika Wizara asilimia angalau 75. Hili Mhe. Naibu Spika, nimueleze Mhe. Waziri kuwa ni moja ya changamoto ya bajeti ya serikali. Kwa hivyo tunamuomba Mhe. Waziri kila alichonacho au serikali walichonacho wanachokitangaza basi wafanye jitihada za makusudi kuweza kufikia hii asilimia angalau 75 kwa kuziwezesha wizara kufanya shughuli zao za kawaida.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia akumbuke Mhe. Waziri kila wizara ina umuhimu wake na wizara ndizo zinazoshughulikia moja kwa moja kwa wananchi wa serikali hii. Wale watoa kodi wa nchi hii sasa wao tegemeo lao ni kuwezeshwa zile wizara halafu baadae na wao wakapata mafanikio yao kule chini. Lakini sasa kama Wizara haziwezeshwi kwa wakati unaofaa kutabakia kuwa na changamoto nyingi katika mawizara na hatutegemei kufika yale malengo tunayoyakusudia. Hilo namuomba sana Mheshimiwa Waziri alione na alifanyie marekebisho kwa kiasi fulani.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea katika maendeleo haya ya uchumi katika sekta ya viwanda, tumeelezwa mengi katika vitabu hivi, lakini moja ya ukuaji wa uchumi ni sekta ya viwanda ambayo kuwa iko katika uchimbaji wa mawe na kokoto. Ni kweli nakubaliana naye Mhe. Waziri kuwa uchimbaji wa mawe na ubanjaji wa kokoto umeongeza kukua kwa uchumi katika kisiwa chetu. Kwa sababu wewe pale anachokitegemea ni yale makusanyo yake ya kodi ya yale magari yanayopita pale ya kuingia kwenda kuchukua mawe au kokoto na kurudi.

Gari moja inapopita pale ikienda na kurudi ikienda tena inalipia tena, ikirudi ikienda tena inalipia tena. Sasa hapa lazima pawe na makusanyo mengi ya fedha ambazo zinapatikana katika sekta hii ya viwanda.

Nakubaliana naye mia kwa mia kwa sababu ni jambo ambalo limeshamiri katika kisiwa chetu hichi cha Zanzibar na hasa katika maeneo ya Micheweni, Vitongoji, na sehemu nyengine, kwa sababu ndio rasilimali yao waliyonayo.

Mhe. Naibu Spika, mkitaka mjue kuwa hawa wanaofanya shughuli hizi za uchimbaji wa mawe na kokoto wamefanya shughuli hizi kwa kuimarisha uchumi wa nchi. Lakini na wao wakitaka wafikiriwe katika hili, kwa sababu wanayotumia hapa ni nguvu kazi yao ya rasilimali ya uzima wao. Sasa hawa wanaochimba kokoto, wanachimba na mawe katika mazingira magumu.

Nimwambie Mhe. Waziri miongoni mwa hao wanaobanja hizo kokoto basi asilimia kubwa ni wanawake. Kama keshawahi kupita katika maeneo yale ya Wilaya ya Micheweni kule pembezoni wanamopita vijana wanaume lakini nataka nimuhakikishie kuwa nenda maeneo ya ndani ndani ambamo kuna wanawake wanakwenda kujenga vibanda na kutoka majumbani kwao tangu asubuhi mpaka 12 kwa kubanja kokoto hizo kwa nyundo.

Mhe. Spika, ikiwa serikali inaona ni moja ya sekta ya viwanda ambavyo kuwa vinakusanya uchumi basi na wao wafikirie watu hawa, kwa sababu wanaongeza pato la taifa. Na wao wakifikiriwe kwa kuwawekea viwanda vidogo vidogo. Kwa hiyo naomba sana Mhe. Waziri hili nalo alione kwani maeneo yapo mengi ya Zanzibar ambayo kuwa wanatumia rasilimali hiyo, lakini na wao serikali iwaone ili iwawezeshe katika kufanikisha hili.

Mhe. Naibu Spika, wakati huo huo maeneo haya haya yenye rasilimali hiyo kwa mfano wa Wilaya ya Micheweni katika ripoti ya *Care* ndio umeoneshwa kuwa inaongoza kwa umasikini. Kumbe rasilimali wanazo lakini sasa serikali inafurahia yale mapato yao tu wanayowapitishia kwa ajili ya kuingia yale magari na kutoka. Lakini sasa na hawa na wao wanatakiwa wawezeshwe, na kuwezeshwa kwao si lazima kuwa tuwasubiri wawekezaji waende wakaweke viwanda vidogo vidogo, tunatakiwa na sisi wenyewe saa nyengine tujitutumue kupitia wananchi wetu na kuwahitaji na wao wapate maendeleo mazuri. Mhe. Naibu Spika, naomba serikali itumie fursa zilizopo za kisiwa hichi kuwajengea viwanda vidogo vidogo ili kuweza kupunguza wimbi kubwa la umasikini la wananchi wetu.

Jengine Mhe. Spika, ukurasa wa 25 matarajio ya ukuaji wa uchumi katika ukurasa wa uchumi wa mwaka 2013 yanatokana na mambo yafuatayo. Kaeleza mambo ambayo hayapungui 10, lakini moja ambalo nataka niligusie ni kuimarisha uvuvi wa bahari kuu, na ufugaji wa mazao ya baharini.

Mhe. hili miongoni mwa mazao ya baharini moja ni uzalishaji wa zao la mwani. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri alijue kuwa miongoni mwa kuimarisha uvuvi wa bahari kuu na ufugaji wa mazao ya baharini na hilo ni miongoni mwa mazao ya baharini. Na Zanzibar katika wananchi kujiajiri wenyewe moja wamepata fursa hii na rizki hii inayoteremshwa na Mwenyezi Mungu kupanda zao hili la mwani. Kwa hivyo Mhe. Waziri nakuomba hili ulione na serikali ilifanyie utafiti ili wazalishaji hawa wa mwani na wao waweze kupata soko la uhakika, Mhe. Waziri umewasikia wananchi hawa na kusikitishwa bei ya kununulia mwani haikidhi na mahitaji ya mwani ule na shughuli zake zinazofanywa.

Kwa hivyo ni moja ya kujitafutia ajira upandaji wa mwani nao. Sasa kama ni moja ya kujitafutia ajira serikali na wao wasitake tu yale mapato wanayopata kwa kusafirishwa mwani ule na wao wawaone wananchi wao, ndio nguvu kazi yao. Sasa kama wananchi watajituma sana hatimaye faida ya serikali ni nini? Kwa hivyo Mhe. Waziri ninakuomba Zanzibar inazalisha tani 15,000 lakini tani elfu kumi zinazalishwa Pemba na inakadiriwa katika uzalishaji huo tani elfu sita kwa mwaka zinazalishwa katika Wilaya ya Micheweni. Kwa hivyo ni kazi kubwa hii wanaofanya wananchi wetu tuwaonee huruma tusiwaachie makampuni kuja wakiwadhalilisha tu halafu kuwapa bei zisizokuwa na mpango. Ingawa Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda juzi katwambia kwamba uzalishaji wa mwani umekuwa unazalishwa mwahali mwingi lakini hata hivyo wanajitahidi, mbona karafuu mwengine zinazalishwa lakini mnazitaka hawatuachii watu wakauza wanapotaka?

Sasa wasione zile karafuu kama si mali yao lakini nini wakawaambia watu kwa sababu unazalishwa maeneo mengi na mikoa mingi tu ule hatujui kwa kuuza je basi watutafutie soko. Sasa hili Mhe. Waziri nakuomba utakapokuja hapa utupe kauli ya serikali ni vipi mtawawezesha wapandaji wa mwani mtawatafutia soko, mtaununua nyinyi ikiwa ni kuula basi tuule sote.

Mhe. Naibu Spika, jengine niende katika sekta ya kilimo katika kitabu chake hiki Mhe. Waziri kasema kitabu cha pili lakini hapa sekta ya kilimo ni miongoni mwa mihimili mikuu ya uchumi wa Zanzibar ambapo unatoa mchango moja kwa moja katika kujikimu kimaisha na kuimarisha hali ya wananchi walio wengi.Sekta hii inatekeleza shughuli zake sambamba na lengo la Mkuza II. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, katoa maelezo Mhe. Waziri kwa kukiri kuwa sekta ya kilimo ni sekta ambayo kuwa wananchi asilimia karibuni sitini na basi ni wakulima wa Zanzibar. Na ndio maana mwenyewe Mhe. Rais katika hotuba yake hapa akaja akatwambia kuwa kututangazia kuwa kutakuwa na Mapinduzi ya kilimo.

Sasa maana ya kutamka tamko hilo yeye Mhe. Rais anachokitaka ni kusaidia watendaji wake ili wamshauri vizuri wamsaidie kutekeleza azma hii na hasa katika kilimo kinachoelekezwa ni cha umwagiliaji maji. Umwagiliaji maji ni mzuri sana lakini umwagiliaji huu maji na humu katika mipango hii inayoanguka humu miongoni mwao uchimbaji wa visima, ukarabati wa mitaro na mengineyo. Lakini Mheshimiwa nataka nikwambie hapa hivi sasa imeshatokea changamoto katika uchimbaji huu wa visima, changamoto inayojitokeza ni kuwa wananchi hawa wanaochimba visima basi wengi wao walikuwa wanategemea ukulima wa vuli, msimu wa mwaka unategemea mvua na kile wanachotumia kisima wanatumia umeme lakini wao wananchi walikuwa kama wanataka kuyahitaji yale maji ndio waweze kutoa fedha zao kwa ajili ya umeme lakini hivyo sivyo, ni kuwa wao hawakujua kuwa kisima

kile kinatumika umeme kama hawajanunua umeme kama haujafika msimu wa kulima ina maana *service charges,* VAT zinaendelea kuwemo, hata unapofika msimu wa kulima ukulima wa vuli wanachotarajia wanunue umeme wao kuingiza kutaka yale maji basi unakuta madeni yamerundikana. Sasa pale wanaanza kukwaruzana, kufika pahali wameshalima mipunga yao sasa wanataka maji wakaenda kununua umeme pesa zinakatwa, sasa hii ni moja ya changamoto ambayo inajitokeza katika mpango mzima wa visima. Kwa hivyo serikali hili ilijue na iweze kujua itawasaidiaje wakulima hawa angalau basi asilimia 80 wachukue serikali kwa sababu hawatamudu kufikia *stage* hiyo. Kwa hivyo kilimo ni kizuri lakini hiyo changamoto muijue kuwa ipo, wakulima wanahitaji msaada wasaidiwe kupitia hili au mzungumze na Shirika la Umeme wawaachie basi angalau ule msimu watakaokuwa wanalima wao ndio waweze kununua umeme wao na kuweza kutumia.

Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, Sekta ya Afya pia nayo ni miongoni mwa kuimarika kwa huduma za jamii mimi sikatai nakubali moja kwa moja kuwa Sekta ya Afya inaimarika, lakini inaimarika kivipi, majengo mengi kila pahali unapokwenda ukizunguka huku Kituo cha Afya ukipita hapa Kituo cha Afya, lakini ni vituo tu havina madaktari havina huduma yoyote. Na ndio maana mpaka kufika Waziri wa Afya juzi kutangaza kuwa wagonjwa wote wanaelemea Mnazi Mmoja hajui wanachokifuatia pale ni nini? Kwa sababu wanachokifutia pale ni ile huduma iliyopo pale kwa sababu angalau wanaona pale wanakwenda watakuta angalau wale madaktari.

Lakini leo mtu anakwenda vijijini kuna hospitali mwezi mzima anahema anakwenda akirudi anapewa *panadol* hapati ushauri wowote pengine anasumbuliwa na malaria lakini hakuna hata vyombo vya kuweza kumuangalia kwa makini, pengine ana matatizo sugu lakini hayaonekani. Sasa ukuaji huu wa sekta hizi za kudumu bado haijawa nzuri. Ninashukuru kwa majengo inafika pahali mpaka madaktari wengine kipindi cha kutoa dawa za majumbani mimi nilishuhudia kituo kimefungwa hospitali. Yuko wapi daktari amekwenda kutia dawa za majumbani. Sasa hii bado haijawa huduma nzuri kwa jamii, ili pawe na huduma nzuri pawe na vitendea kazi pawe angalau pana daktari anayeweza kujua huyu ana homa ya manjano na huyu ana homa ya malaria. Mhe. Waziri hili tulione hapa.

Lakini pia katika sekta ya elimu na maskuli mengi tunayajenga tele lakini tatizo letu, huku tunajenga huku tunaacha kunavunjika. Sasa tutaendelea kujenga kujenga mpaka lini, skuli zinahitaji zile kongwe ili kile kipya kidumu, basi na kile kikongwe kihifadhiwe kienziwe. Lakini leo tunafika tunajenga maskulini, skuli inakaa miaka 3 serikali haijapata uwezo wa kuezeka. Lakini yale mabanda mengine ambayo kumbe yangewezekana kukarabatiwa yangeweza kuendesha wale wanafunzi wakasoma. Lakini

wanafunzi wameondoshwa katika mabanda yale huku yanajengwa mengine sasa hii mipango gani? Huu mpango wa kujenga ni mpango wa kufanya nini? Tutake wananchi wachangie tufanyeje, lakini zile kongwe hazienziwi hili tatizo Mhe. Waziri. Lazima tunapofanya jambo tufanye jambo kwa njia ya uangalifu.

Lakini la mwisho Mhe. Waziri serikali imeanzisha Mamlaka ya kuzuia rushwa, tunawapongeza sana kwa kuanzisha kitengo hichi lakini Mhe. Waziri naomba tuwe makini sana hasa na wafanyakazi, tusijekuwa tunaanzisha Mamlaka ya kuzuia rushwa hata huko mbele ikaja kuwa Mamlaka ya kuimarisha rushwa, hili tulielewe sana hii ni sekta ambayo ni muhimu sana katika nchi lakini wanatakiwa wafanyakazi wake waenziwe hasa ili wawe ni watu ambao kuwa watatuondoshea tatizo hili.

Kwa hayo machache Mhe. Naibu Spika, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa na mimi kutoa mchango wangu huu lakini ninamuunga mkono Waziri na wananchi wangu wa Wilaya ya Micheweni na wao wanaunga mkono kwa niaba yangu tunaomba majibu mazuri. Ahsante sana.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu aliyetujaalia uhai, uzima tukawepo hapa kutekeleza majukumu yetu kwa maslahi ya taifa letu.

Mhe. Naibu Spika, nikushukuru na wewe kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza name kutoa mchango wangu mdogo katika mada iliyoko mezani wakati huu. Mhe. Naibu Spika, nimpongeze Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri aliotutolea juzi.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea nianze na kusema yafuatayo:

Marehemu Mzee Abeid Amani Karume aliuawa na amezikwa lakini tukasema kilichozikwa ni kiwiliwili chake tu, mawazo, fikra na busara zake zitaendelea kudumu milele.

Baada ya utangulizi wangu huo Mhe. Naibu Spika, sasa niende kwenye bajeti hii ambayo wananchi wa Zanzibar baada ya kusikia kwamba inasomwa walijenga matumaini, walikaa vinywa wazi, masikio wazi, walikaa chini ya vyombo vya habari ili kuweza kuona serikali yao katika 2013/14 nini inataka kuwafanyia. Ni kawaida ya wananchi serikali yao huona ni ibada na bajeti ni sikukuu, hivyo wanatarajia mambo mengi kupitia bajeti ya serikali.

Mhe. Naibu Spika, nianze katika kitabu hiki kuangalia, kwanza nipongeze kwa ongezeko la pato la taifa niseme hivyo, ni kweli kabisa tuna uwezo wa

kuongeza pato la taifa, lakini matatizo katika utaratibu huu tunao bado kuna mapato mengi ambayo yanapotea hayakusanywi na vile vile haikuwekwa utaratibu maalum wa kuona kila pale ambapo pana mapato ya serikali yanakusanywa ipasavyo. Ninaamini kwamba kama utaratibu mzuri utatumika nina imani kwamba tutaongeza zaidi na tutaweza kuwafikia wananchi zaidi kuweza kumudu mahitaji yao.

Vianzio vyote vya mapato vikumbukwe na visimamiwe ukizingatia kwamba tuna mambo mengi au njia nyingi za uchumi ambazo mipango hiyo mengine inagusana na ndugu zetu wa damu. Fedha hizi ni lazima zisimamiwe na tuhakikishe kwamba tunazitumia ipasavyo kwa maslahi ya Wazanzibari.

Mhe. Naibu Spika, sasa nimeona hapa katika kitabu hiki cha bajeti katika ukurasa wa tisa inasema pato la mtu binafsi, hapa Mhe. Naibu Spika, ndipo ambapo niangukie na kuanzia.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri amesema pato limeongezeka na wananchi wameongeza kipato ambacho ukikigawa na kukikasimu kwa pesa za Tanzania ni kusema kwamba kila mwananchi atatumia shilingi 2700 hivi wastani wake. Lakini nikawa ninajiulizia hivi katika hali hii ya ukuaji wa uchumi pamoja na mahitaji ya wananchi nikijiuliza kwamba tuna mpango huu wa kupunguza umaskini na kuongeza kipato, shilingi 2700 kwa mwananchi wa Zanzibar ambaye anahitaji huduma ya elimu, afya na mengineyo anaweza kumudu kuishi? Nikaona kwa mtazamo wangu kwamba 2700 hawezi kuishi mtu yoyote na kwa kweli hili bado limekuwa tatizo, iko haja ya kuandaa utaratibu mwengine mpya ili kuona kwamba vianzio vyetu vya mapato vinaenda sambamba na haja ya matumizi ya Wazanzibari au ya wananchi wote.

Mhe. Naibu Spika ninalinasibisha suala langu hilo nikigusia kwamba tatizo ambalo nimeligusa ni ajira kwa wananchi wetu au kwa vijana wetu. Nina imani kwamba laiti mipango yetu ingelikuwa madhubuti na tukazingatia ile hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar aliposema kwamba sisi wenyewe tulikiri akasema kuna Mapinduzi ya kilimo, lakini dhana ya utalii kwa wote ingelizingatiwa na ikawa inaendelezwa katika utaratibu huu nadhani tungeliweza kuwafikia wananchi wetu kupata neema na hali kuwa nzuri. Pamoja na mipango mingi ambayo imepangwa ikiingizwa Mkuza I na Mkuza II mimi niseme jemedari wa kuanzisha Mkuza I na II ni hayati Mzee Abeid Amani Karume.

Kwa nini niliseme hili, nasema hili kwa sababu hayati Mzee Abeid Amani Karume alianzisha Mkuza I na II kwa kusema kwamba wanyonge wote aliwapatia ekari tatu tatu, hayo ni mafunzo ambayo tuliyapokea kwake huo ni msingi mwema ambao alikusudia kuwanufaisha wananchi wa nchi hii ili

kuweza kukidhi mahitaji yao na kuweza kuishi katika maisha ya neema na furaha na raha katika taifa lao. Hakusita hapo akasema tena kwa kuwaona wanyonge hawawezi kumudu kusoma basi alisema elimu bila ya malipo kwa kuwafikiria wanyonge ambao hawataweza kuliendesha taifa lao bila ya kuwa na elimu. Hakusita hapo akaona hali ni ngumu afya hawawezi kuifikia wananchi akalifanya hili akatangaza matibabu bure. Lakini hakuishia hapo hayati Karume aliendelea kusema jengine, hayati Karume alifanya nini, njia zote kuu za uchumi zitamilikiwa na wananchi wenyewe na hili ndio tatizo ambalo limetukwaza kwamba yale yote ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya taifa letu kiuchumi sasa hivi hayapo ndani ya mikono yetu, hili Mhe. Waziri ni tatizo, ni tatizo, ni tatizo.

Mhe. Naibu Spika, nije hapa kuona kwamba ile dhana ya Utalii kwa wote nimuulize Mhe. Waziri amejiandaa na mpango gani madhubuti ambao utawezesha kuwawezesha vijana wetu kuweza kuzibeba ajira zote ambazo zitaingia katika sekta ya utalii ambazo wana uwezo nazo. Umejiimarisha vipi kuweza kukiimarisha Chuo cha Utalii, kuweza kuwasomesha vijana wetu wakaweza kuingia katika ushindani wa soko la biashara na wakaweza kumudu kuingia katika mahoteli haya na kufanya kazi. Ningeomba kupata hilo, lakini pia nimeona Mheshimiwa kwamba umesema sasa unataka kuingia uvuvi wa Bahari Kuu. Katika hilo nimeona hapa katika kitabu chako cha pili cha muelekeo wa hali ya uchumi na mipango ya maendeleo ya mwaka 2013/2014. Inasema kwamba:

Kuna mradi wa kuendeleza uvuvi wa Bahari Kuu. Mheshimiwa umesema hapa kwamba kazi zinazotarajiwa kutekelezwa kwa mwaka 2013/14 ni kubomoa jengo la ZAFICO na kujenga soko jipya, ikawa ninapata mashaka kidogo. Uvuvi wa bahari kuu nilitarajia utasema kwamba sasa tutaanzisha chuo cha uvuvi ili kuona kwamba tunawaweka vijana wetu *standby* na hatimae kuongokewa katika mipango mengine. Lakini la pili nilisema ni kutoa mafunzo ya uvuvi wa kina kirefu cha maji kwa vijana 30 tu. Mhe. Waziri ni wakati muafaka wa kuelewa kwamba nchi yetu ni kisiwa na wananchi wengi kabisa ni wavuvi na baharini kuna mali nyingi, kuna mambo mengi, iko haja sasa ya kuanzisha chuo hicho, lakini pia kujiwekea mikakati ya kuona kwamba tunafikia malengo hayo. Si haya ambayo nimeyaona mambo mengi ambayo yanaelekea vijana wachache sana ambapo muelekeo wako sidhani kama tunaweza tukafikia hasa hilo lengo la uvuvi wa Bahari Kuu kwa kununua boti mbili.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea niseme kwamba sote tunakiri kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa taifa hili, ikiwa kilimo ni uti wa mgongo wa taifa hili na Wazanzibari wengi waliomo katika taifa hili ni wakulima, hebu niambie ule mpango madhubuti ambao aliutangaza Rais na Mapinduzi ya kilimo umefikia

wapi ule utaratibu wa *Nerica* na *Kificho* ambazo ni mbegu *special*, ambazo tulizichagua kwa kuona kwamba wananchi wetu sasa watakuwa na mbegu imara zinozalishwa umeishia wapi.

Mhe. Naibu Spika, nihoji tena kuhusu ule utaratibu tukijielewa kwamba sisi ni Wazanzibari na chakula chetu kikuu ni wali. Hebu nieleze ule mpangilio ambao tulielezwa mwaka jana wa kusema kwamba tutayafikia mabonde yetu kilimo cha umwagiliaji maji kimefikia hatua gani. Nina imani kwamba laiti tungelikuwa tumefanya mipango, siku zote wanasema watu *mipango si matumizi* laiti kama tungelikuwa tumefuata utaratibu wa kilimo hiki cha uwagiliaji maji sisi tungekidhi haja kwa wananchi wetu kutumia mchele huo bila kuagizia, na ninaamini kwamba hilo linawezekana na hatimae mwengine kuweza kusafirishwa, hili ni jambo linalowezekana kabisa. Wasingelima kwa awamu moja kama sasa kwa kutegemea kilimo cha mvua lakini badala yake wangelilima mara mbili zaidi. Nadhani kwa chakula tu ingetosheleza na pia kujipatia kipato.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu nimeona katika kitabu cha Mhe. Waziri anachosema kwamba moja kati ya jambo ambalo limekuwa na kusaidia pato la taifa ni viwanda. Mhe. Naibu Spika, na viwanda vyenyewe vikaelekezwa, kiwanda cha kokoto na viwanda vya mawe na uchimbaji wa mchanga.

Mhe. Naibu Spika, nasema tusidanganyane, tujielewe sisi ni visiwa ikiwa tumeamua mawe na mchanga na tuviite viwanda nasema hii tunadanganyana, viwanda haviwezi kuwa hivyo, sisi wengine tupo katika historia tunakumbuka vilivyokuwa viwanda ni vipi ikiwemo Kiwanda cha Sukari cha Mahonda ambacho wananchi wengi wa Zanzibar kwa wakati ule wa Mkoa wa Kaskazini walipata ajira zao, waliweza kujikimu kimaisha, kiliweza kutoa sukari ya kutosha.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri lazima aandae mpango madhubuti katika utaratibu wa kuiwezesha Zanzibar kuweza kuweka Viwanda. Hii itatukwamua kiuchumi kupitia vijana wetu pia kupata ajira zao lakini pia kuiongezea nchi yetu kipato na pia baadhi ya mambo mengine yatatupungukia. Sisi tuna matunda mengi Zanzibar lakini tunashindwa kuyasarifu na kuweza kuyasafirisha. Sisi tuna mazao mengi lakini Mheshimiwa kwa sababu inashindikana kuwepo kwa viwanda ambavyo vinaweza vikamudu basi tumeishia hivyo hivyo na hatimae tukajisahau kabisa kwamba nchi yetu ni ndogo mno kiutaratibu, inahitaji kupangiwa utaratibu madhubuti wenye kufaa. Hili nililisema mwaka jana wakati wa bajeti umefika wakati wa kuigawa ardhi ya Zanzibar katika muelekeo wa mambo ambayo yametugusa, tuone eneo ambalo litatufaa kwa kilimo endelevu ambalo linaboreshwa na

kuweza kutoa mazao muafaka kwa ajili ya kuwatumikia Wazanzibari na kutibu shida zao. Lakini tutenge maeneo ambayo yatakuwa yanatosha kwa ajili ya majengo, tuweke maeneo maalum ambayo tunaweza tukajenga maofisi na mambo mengine yanayotugusa tuone tunaacha sehemu kwa ajili ya viwanja vya michezo na mambo mbali mbali ya kuanzisha miji mipya. Nadhani mipango hii kama ingelikuwa imewekwa na utaratibu ukafuatwa Mhe. Waziri leo tusingekaa hapa kuiangalia bajeti hii ambayo inawajenga kuwatia huzuni wananchi.

Mhe. Naibu Spika, nimwambie Mhe. Waziri kwamba yale maeneo ambayo yalitangazwa kuwa huru ya vitega uchumi hebu tukate pua tuunge wajihi sasa, tuweke nia ya kuyafikia maeneo hayo kuyapelekea miundombinu, maji pamoja na umeme ili wawekezaji waje basi mbona wapo kwa muda mrefu. Napata mshangao mkubwa kuona tumekuwa nayo katika kuyatangaza katika makaratasi lakini na kuyasema midomoni lakini vitendo havijaonekana. *Ada ya mja hunena muungwana ni vitendo*. Wazanzibari wamechoshwa, wananchi wamechoshwa na maneno sasa wanataka vitendo, hali si shwari, watu wana shida, wana dhiki, wana njaa!

Mhe. Naibu Spika, nirudi tena kwenye kitabu hiki katika ukurasa wa 45-46 ambao unasema kwamba kuimarisha utaratibu wa utoaji kodi ya mafuta, ikaendelea ikaja 46 ikasema kwamba inapendekezwa kodi ya shilingi 35 ya lita ya diseli na petroli Mheshimiwa ni kuwaangamiza wananchi wa Zanzibar. Kodi hii haitamgusa hata siku moja yule ambaye anaendesha gari, kodi hii itamgusa yule mnyonge wa chini kabisa kabisa. Lita moja kwa shilingi 35 hii ni athari kubwa kwa wananchi na utekelezaji wa kazi za serikali. Una utaratibu gani kwa lita hiyo hiyo ya mafuta ya kodi ya njia itakwendaje kwa wafanyakazi wa serikali au kwa vyombo vya Serikali. Naomba utakapokuja hapa hili nalo unifahamishe au itakuwa ni gari za wananchi wa kawaida tu, ninaamini kwamba kama halikuzingatiwa hili Mhe. Waziri kodi hii ni kuwaumiza wale wale wanyonge. Yule yule mwanamke unayemtaka afanye Shughuli zake za uzalishaji mali, vikundi vya ushirika anahitaji kufuata huduma atapanda gari huyo, akipanda gari na bei ya nauli inapanda na mwenye gari hatosikia Kiswahili hicho ataongeza namna ya kulibeba polo la mchele ambalo linataka kwenda kijijini ataongeza kodi.

Mhe. Waziri nakuomba sana uliangalie kwa kina hili mimi siwezi kuunga mkono na silikubali kabisa kwa kuona kwamba uchumi wenyewe wa wananchi wetu tunaiangalia kithamani kwamba ni 2700 ndio uwezo wa makisio ya Serikali na uwezo huu ukiuangalia kwa kina hasa walio na uwezo kamili ni wachache na *average* hiyo uliyoigawa kwa pato zima ni kusema kwamba wengine hawamudu hata kupata shilingi elfu moja kwa siku, hili lipo. Kwa mchanganuo huo Mhe. Waziri nakuomba sana mzigo huu mzito,

mzigo huu uwaondolee wananchi waweze kupumua kidogo angalau waendelee na hali hivyo ilivyo.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye sekta ya elimu. Taifa letu limefika wakati sasa wa kuwekeza mipango yake katika kuwasomesha vijana wetu wa fani mbali mbali ili tuweze kufikia malengo na matakwa yetu. Taifa maskini linawekeza kwanza kwenye elimu, sisi vijana wetu tuna matatizo kadhaa wa kadhaa ambazo wanashindikana. Kuna ma-*engineer* hapo wa meli hawa wametoka sehemu mbali mbali si Wazanzibari sisi hatuna kwa nini? Tuna madaktari *specialist*, tunawahitaji kwa ajili ya afya za wananchi wetu, hebu nipate taarifa umejipanga vipi kuona vijana wetu tunawasomesha wa kada mbali mbali ukiwaingiza hao ambao watashughulika na uvuvi wa Bahari Kuu. Mhe. Waziri nieleze umewapanga pangaje hawa, ili vijana wapate taaluma hizo. Sisi siku zote tunapanga mipango yetu lakini tulisahau kuwekeza kwenye elimu kwanza, wataalamu mbali mbali ambao wa sekta tafauti tafauti mara nyingi tunawaagizia kutoka nje jambo ambalo linaipa gharama Serikali, laiti tungeliwekeza katika utaratibu maalum wa kuweka wataalamu nadhani tungelikuwa tumefika leo wazalendo wenyewe wangezifanya kazi hizo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri nikwambie ukweli wanawake nasi tunakuuliza mwaka jana Rais alipotoa msamaha wa wazazi kujifungua bure, mara nyingi imefikia mahala tukawa tumeambiwa sisi hatukuingiza kwenye bajeti na tukaenda vituo vyote huduma hizo zikawa hazipatikani, naomba utuelimishe utuambie katika mpango huu fedha zetu zimeingia humo, kama sijaziona Mhe. Waziri mpango huu wa msamaha wa wazazi wanapokwenda kujifungua huduma hiyo basi nitakuwa na mashaka makubwa sana kupitisha bajeti hii.Anayeathirika na mtu ambaye amedaiwa yeye kamzuilia hii inakuwa haipendezi. Mhe. Waziri, nimelikusudia hili niliseme kabisa kabisa wazi wazi katika bajeti yako hii kukuonesha kwamba wanawake wengi baada ya kauli ya Rais walipata tabu sana na kuhangaika kwa sababu Wizara ya Afya ilikuwa haikuingiziwa fedha kwa ajili ya zoezi hilo.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho kabisa Mhe. Waziri, tumepanga mambo mengi, mipango ambayo Wizara husika itakuwa utekelezaji lakini Mhe. Waziri, kuna matatizo makubwa ya upatikanaji wa fedha hizi kiwakati na mara nyingi inafikia pahala katika mizunguko yetu ya Kamati unakuta Wizara hizo hazijaingiziwa fedha na mara nyengine zinaingiziwa mwisho kabisa kabisa ambapo wanashindwa kuzifanyia matumizi. Ningependa Mhe. Waziri, utakapokuja hapa utueleze ni kwa sababu zipi, lakini pia utuambie zile ambazo hazikuingizwa katika bajeti hii zinakwenda wapi, zile ambazo tumeziwekea mipango lakini hatimaye zikawa hazikuingizwa zinaishia wapi. Baada ya kuyasema hayo Mhe. Naibu Spika, Ahsante sana.

Mhe. Abdi Mossi Kombo: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Mhe. Naibu Spika, nikianzia kitabu chetu hiki ukurasa wa 29(43) nakuomba kwa ruhusa yako kidogo ninukuu "mambo yote haya yatafanyika bila ya kupuuza umuhimu wa miundombinu ya msingi kama vile barabara, bandari, viwanja vya ndege, umeme ikiwemo kutafuta vianzio mbadala".

Mhe. Naibu Spika, kwanza ningeomba kwanza viongozi sote tuwe na miundo ya kubadilika. Kitabu chetu kinasema kwamba miundombinu ya barabara hivi sasa barabara tunazo lakini barabara zetu za Zanzibar kutokana na idadi ya magari, idadi ya watu barabara zetu ni nyembamba sana. Mbali ya barabara zetu kuna madaraja hivi sasa mabovu, kwa mfano ukipita katika njia yetu kutoka Nungwi kwenda Mkokotoni, madaraja yaliyopo katika barabara zetu ni hatari tupu, madaraja mabovu tena ni membamba, hivyo ninaomba Serikali bajeti hii tuliyokuwanayo mwaka huu tuhakikishe tunaleta miundombinu ya barabara zenye uhakika.

Mhe. Naibu Spika, kitabu chetu kinasema kwamba miundombinu ya viwanja vya ndege Mhe. Waziri, naomba aje atuambie kiwanja chetu cha Unguja cha ndege mbona bado kingali kile kile kiwanja cha kimaskini hakijakuwa cha kisasa. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, ulimwengu wa kileo tunakwenda na ulimwengu wa sayansi na teknolojia kila kitu kinakuwa safi na kizuri kinavutia, bado kiwanja chetu cha ndege hakijavutia na kwa sababu gani mpaka sasa hivi tushafika katika ulimwengu wa sasa bado viwanja vyetu vya ndege bado ni vile vile havikidhi haja.

Mhe. Naibu Spika, tukienda katika miundombinu mengine iliyotajwa hapa Serikali imetenga shilingi sitini na mbili bilioni elfu saba kwa kuimarisha kilimo. Mhe. Naibu Spika, Zanzibar bado kilimo hakijaimarika, kwa sababu wakulima wetu wengi sasa hivi wanaolima mpunga wanakosa zana za kulimia kwa wakati, pembejeo kama matrekta yanachelewa, wakulima wanapata tabu, ule wakati wa kulima wakati wa kuchimbuliwa mvua tayari ndio mabonde yanachimbuliwa, lakini mkulima ukija ukimuuliza anasema mimi trekta bado halijafika. Kwa hivyo Serikali ninaiomba kwamba itueleze sababu gani mpaka pembejeo za kilimo Zanzibar hazijakuwa za kutosha.

Mhe. Naibu Spika, katika miundombinu ya kilimo, kama Waheshimiwa wenzangu walivyosema kwamba hivi sasa tunahitaji ukulima wa kumwagilia maji lakini bado mabonde yetu yapo ya ukame, hakuna kilimo cha kumwagilia maji wakati mvua zetu za kileo ndio kama tunavyozijua zikinyesha mvua za masika tena hakuna. Kwa hivyo Serikali tunaiomba ihakikishe kwamba wakulima wa Zanzibar wanachimbiwa visima katika mabonde yao ya mpunga walime kwa wakati na wavune kwa wakati.

Ningelimuomba vile vile Mhe. Waziri Serikali inagharimu sana kilimo cha mpunga Mhe. Waziri aje atueleze Zanzibar inavuna tani ngapi kwa mwaka.

Mhe. Naibu Spika, tukienda katika miundombinu hii, hivi sasa Wazanzibari wengi wanalima matunda; embe, ndimu lakini hakujawa na miundombinu ya kusarifu embe zile na matunda yale yakawa watu wa Zanzibar wakawa wanasafirisha hata nje kwa sababu gani. Kwa hivyo ningeliiomba Serikali wananchi wanaolima matunda wajengewe viwanda vya uhakika na wao wasarifu kwa sababu hivi sasa wakulima wanaolima ndimu zinatupwa ovyo, wakati huku wananchi wanaambiwa wajiajiri wananchi lakini wanajiajiri kilimo baada ya kujiajiri kilimo yale matunda yanapotea. Kwa hivyo Serikali naiomba bajeti hii na tutamtaka Mhe. Waziri wa Viwanda atuhakikishie bajeti anajenga viwanda ili wananchi wapate kusarifu matunda yao.

Mhe. Naibu Spika, tukienda katika sehemu za Bandari Serikali mwaka jana ilituambia kwamba itajenga bandari kuanzia Malindi mpaka Mpigaduri ili wananchi wapate ajira, wananchi wapate manufaa. Mimi Mhe. Waziri ningelipenda aje atueleze bandari ile imefikia vipi au wasafiri hawapo tena. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, miundombinu ya bandari ndio itakuza uchumi wetu, kwa hivyo na hili nalo nataka tuje tuelezwe vipi bandari yetu imefikia wapi. Kwa sababu tatizo kubwa la wananchi, tatizo kubwa la vijana katika nchi yetu ni ajira na lazima Serikali iweze kuweka miundombinu ya ajira.

Mhe. Naibu Spika, katika kitabu chetu hiki hapa ukurasa wa 41 unasema Serikali imeweka programu ya kuimarishwa uvuvi wa Bahari Kuu. Mhe. Naibu Spika, Serikali nafikiri bado haijawa tayari kuimarisha programu ya uvuvi wa bahari kuu. Kwa sababu mpaka leo Wazanzibari wanavulia vihori, sasa bahari kuu hii tutaivua kwa vipi. Kwa hivyo Mhe. Waziri namuomba aje atueleze lini uvuvi wa bahari kuu Zanzibar utaimarishwa wakati samaki tunao wengi sana lakini bado samaki wanaibiwa na watu wengine. Sasa lini uvuvi wa bahari kuu utaimarishwa Zanzibar, tukiimarisha uvuvi wa bahari kuu ndipo tutapowapa wananchi wetu maendeleo. Kwa sababu samaki tunao wengi lakini hatuwezi kuwavua kwa sababu hatuna zana. Kwa hivyo naiomba Serikali kwamba ili kuweka miundombinu yote ni lazima Serikali itoe huduma, lazima Serikali iagizie vifaa ili kwa kupata wananchi kufanyia kazi, bila ya vifaa, bila ya elimu hatuwezi kuweka miundombinu ya kitu chochote.

Mhe. Naibu Spika, nisipoteze muda wako. Kwa upande wa barabara kama sehemu katika majimbo yetu mengine bado hayakuwa na miundombinu wa barabara. Mimi katika jimbo langu la Matemwe bado miundo ya barabara haijakuwa mizuri, umeme hakuna, maji hakuna sasa miundombinu ikiwa hakuna wananchi watapata tabu sana.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia naiomba Serikali iwahakikishie wananchi bajeti hii ya mwaka 2013/2014 kuwahakikishia vijana kwamba wanapata ajira ndani ya sekta mbali mbali ili kupunguza tatizo kubwa.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu kwa kuchangia hotuba hii naunga mkono hotuba hii mia kwa mia, ahsante.

Mhe. Salma Moh'd Ali: Mhe. Naibu Spika, nakushkuru kwa kunipa nafasi. Kwanza naomba nikushukuru na mimi kuniwezesha kusimama hapa. Vile vile namuomba aniwezeshe kukamilisha dhamira yangu ya kuchangia hotuba hii.

Mhe. Naibu Spika, pili nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi, lakini vile vile kabla ya kumpongeza Mhe. Waziri naomba nitoe maelezo kidogo ambayo niliwasikia vijana wakiyazungumza kipindi cha bajeti kama hiki mwaka jana. Mhe. Naibu Spika, nilisikia vijana wale Wawakilishi pale wanaposimama Barazani na kumpongeza Mhe. Waziri huwa wanafikiria kama ile bajeti imejibu mahitaji ya wananchi au ndio wanampongeza kwa sababu maneno na maelezo yaliyomo mule yamepangika. Mhe. Naibu Spika, sasa mimi nataka nimpongeze Mhe. Waziri kwa hotuba yake na jinsi alivyoiwasilisha.

Mhe. Naibu Spika, sasa mimi nataka nianze kwa kusema kwamba msingi mkuu wa bajeti ni mapato. Kwa hiyo ningeliishauri Serikali ifanye mkazo katika mambo mawili, kwanza kuibua vianzio vipya vya mapato na hii Mhe. Naibu Spika, hata bajeti ya kwenye nyumba ikiwa huna mapato huwezi kupanga matumizi. Kwa hiyo Mhe. Waziri ni lazima waibue vianzio vipya vya mapato kwa sababu inaonesha vianzio vya mapato tulivyonavyo havitoshi na hasa ukizingatia humu katika hotuba tumeelezwa kwamba uchumi umekuwa, kipato cha wananchi kimeongezeka lakini vile vile haikueleza kwamba umaskini kwa wananchi umezidi. Hivyo ni lazima Serikali ijipange na vianzio vipya vya mapato, na vile ni kuweka utaratibu mzuri ambao utadhibiti vianzio vya mapato ili ukusanyaji wa mapato yasipotee ovyo ovyo.

Mhe. Naibu Spika, hapa nitatoa mfano. Mapato mengi yanatokana na sekta ya utalii, hivyo ni vizuri kuangalia maeneo yanayoingia watalii kama vile uwanja wa ndege na Bandarini. Jana Mhe. Salmin alizungumzia sana suala hili jinsi mapato yanavyopotea *Airport* na bandarini mapato ya *visa*, sasa hili ni lazima liekewe utaratibu mzuri. Pia vile vile katika maeneo ambayo wanakwenda tuweke utaratibu ili mapato ya viingilio hivyo yasipotee. Mhe. Naibu Spika, jambo lolote lile likiwa halina mpangilio hata ukiwa na mkoba kile ambacho umeshakichuma ikiwa mkoba ni mbovu basi lazima yatapenya kile ulichokitia ndani, na vile vile hayo yanayokusanywa ikiwa mkono wako ukiwa hukusanyi vizuri basi hutapata kujaza mkoba wako.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ambalo ni zuri liangaliwe kwa maslahi ya wananchi ni kutowepo mlinganisho wa utoaji wa leseni na kodi, hili ni tatizo Mhe. Naibu Spika. Kwa mfano gari ya abiria 15 inayotoka Darajani hadi kufikia Fumba na gari ya abiria hao hao 15 inayotoka Chake Chake hadi Vitongoji, Mhe. Naibu Spika, gari inayotoka ya Darajani ikienda Fumba *trip* kumi kwa siku, lakini gari ya Chake Chake kwenda Vitongoji itakwenda *trip* mbili kwa siku. Sasa bila ya shaka hapa makusanyo gari iliyokwenda mara kumi itakusanya zaidi kuliko gari iliyokwenda mara mbili. Sasa Mhe. Naibu Spika, hapa mimi nashangaa sana na nina suali hasa kwa Mhe. Waziri kwa nini gari hizi walipishwe leseni ya njia kiwango kimoja na kodi moja ya mapato, pengine Mhe. Waziri atatuambia pengine huyu anakatwa mia tano na huyo mia tano, lakini kodi inayokusanywa mwenye *trip* kumi atakusanya zaidi kuliko wa *trip* mbili, sasa mtu kakusanya elfu kumi na mwenziwe kakusanya laki moja lakini mkato yule akatwe elfu tano na yule elfu tano, sasa hapo sijui hasa Mhe. Waziri atatueleza nini juu ya suala hili au hapa amekusudia wale walio na kiwango kidogo cha kuzalisha wasiweze kuzalisha.

Mhe. Naibu Spika, mfano mwengine ni hoteli ya nyota moja iliyopo Chake Chake na hoteli ya nyota moja iliyopo Mji Mkongwe. Mhe. Naibu Spika, hoteli ya nyota moja iliyopo Mji Mkongwe itapokea wageni wengi ukilinganisha na hoteli ya nyota moja iliyopo Chake Chake, na hata uzalishaji wake itakuwa yule anayepokea wageni wengi itazalisha zaidi kuliko aliyepokea kidogo. Sasa Mhe. Naibu Spika, hapa nashangaa kwa nini hoteli hizi mbili walipishwe kodi moja wakati wanatofautiana mapato, hata kama vyumba vyao viko sawa sawa, ikiwa ile ina vyumba mia na ile ni vyumba mia, lakini ile inapokea wageni kidogo na ile inapokea wengi, na hata kama daraja yao ni moja lakini tutizame yale mapato yao wanayoyapata. Mhe. Naibu Spika, ninamuomba Mhe. Waziri anipe majibu sahihi hapa ili wananchi wanyonge wapate kuridhika.

Mhe. Naibu Spika, vile vile katika ukurasa wa 15 *paragraph* ya 22. Mhe. Waziri katika hotuba yake alimalizia kwa kusema nanukuu "misaada ya kibajeti imeshuka tena hapo akataja hizo hesabu zake na hali hii imesababishwa na kukwama kwa sababu za kiutendaji kwa sehemu ya Zanzibar ya misaada inayopitia katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano". Sasa Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri anifahamishe ni sababu zipi zilizopelekea watendaji kutukwamisha? Na ni hatua zipi walizochukuliwa watendaji hawa ili mwakani wasije wakatukwamisha tena?

Mhe. Naibu Spika, naomba Mhe. Waziri anipe ufafanuzi mzuri kwa sababu ile hadithi kwa vile umetuambia tusipoteze muda wa wale vijana walioiliza bajeti nilikuwa nikitaka kuendeleza azidi kunifahamu lakini naona nitapoteza muda.

Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa wa 26 *paragraph* ya 38 kuna kifungu kidogo cha 6 kinataja kuwa matarajio ya ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2013 ni upatikanaji wa mkonga. Sasa suala langu ni kuwa mkonga huu ambao ulizinduliwa na Mhe. Rais mwezi wa kwanza mwaka huu na hadi leo hii mkonga huu haujaonekana kuanza kutumika, je ni lini mkonga utaanza kutumika ili matarajio ya ukuaji wa uchumi yaweze kufikiwa, na pia naomba Mhe. Waziri anifahamishe kwa kigezo cha mwananchi masikini mkonga utaweza kuinua uchumi wake na kipato chake.

Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa wa 30 *paragraph* ya 44 inataja kwamba mategemeo ya upatikanaji wa meli ya Serikali ni mwezi wa Juni 2015. Mhe. Naibu Spika, kwa hili mimi na kwa niaba ya wanawake wa Chake Chake nimevunjika moyo mno. Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, mwaka jana katika bajeti hii Mhe. Waziri alipunguza vifungu vya Wizara kwa ajili ya kupatikana hizi pesa za kutafutia meli, sasa na leo hii tunaambiwa meli hiyo itapatikana 2015, Mhe. Waziri haoni kwamba huo ni muda mkubwa hasa ukizingatia haipendezi wananchi kutegemea meli za watu binafsi na Serikali yao ipo na huku Serikali eti inasubiri 2015 na bado bajeti wanaiona ikipunguzwa vifungu tokea 2012/13.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia hali ya ajira ni tatizo, tena ni tatizo kubwa na kila siku tunasema tuwaelimishe tuwadhibiti vijana wetu wasiendelee katika kuingia makundi maovu, njia moja ya kuwadhibiti vijana ni kuwapatia ajira. Hivi sasa Mhe. Naibu Spika, kuna vijana wengi waliomaliza Chuo Kikuu lakini hawana ajira Serikalini wala kwenye Sekta Binafsi. Hali hii haileti taswira nzuri ya ukuaji wa uchumi, vile vile vijana hawa wametumia pesa nyingi katika kusoma kwao pesa za walipa kodi, je Mhe. Waziri, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia ajira vijana hawa.

Mwisho kabisa Mhe. Naibu Spika, naomba niseme maneno mawili kwa kweli baba mzuri katika nyumba ni yule anayewatizama wanawe kwa kuona kima chao, uwezo wao na kila kitu wale wanawe anawajua, huwezi kuwa na mtoto aliye na kimo kama Salma ukamwambia kazi yako asubuhi ukiamka ni kunipachikia mapazia, ukamchukuwa mwengine aliye na kimo kama Mhe. Mgeni ukamwambia kazi yako asubuhi ni kuniletea vitabu eti panga vitabu vilivyopo juu ya meza.

Mhe. Naibu Spika, Serikali lazima ione wakati wa kupanga bajeti pale mimi nikiunga kimo kwa jiti hasara inaweza ikatokea pengine nitaanguka, ikiwa nitaweka kibao nivunjike ile kazi ambayo alitakiwa aifanye Mhe. Mgeni itabidi sasa afanye kazi mbili, afanye ya kupachika mapazia na afanye ya kuweka vitabu mezani. Kwa hivyo Mhe. Waziri nakuomba pale mnapokaa na Serikali yote kwa ujumla mukitayarisha hii bajeti muwatizame wananchi kila

mmoja na uwezo wake, huwezi ukamwambia dereva wa gari au mfanyabiashara aliye na gari ya watu 15 ya Vitongoji - Chake alipe sawa sawa na dereva anayefanya kazi pengine kutoka Darajani-Chukwani hiyo haiwezekani Mhe. Naibu Spika.

Mwisho kabisa Mhe. Naibu Spika, nawapongeza wananchi wenzangu wa Zanzibar kwa kushiriki kikamilifu katika utoaji wa maoni ya Katiba Mpya, na pia *inshaallah* nchi yetu itafika pale pahala pazuri tulipopakusudia.Zanzibar iwe na mamlaka yake na Muungano uwe tunaoutarajia. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Naibu Spika, kabla ya yote na mimi nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha siku hii ya leo kufika katika Baraza lako tukufu kwenye hali ya uzima na afya.

Pia Mhe. Naibu Spika, nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Fedha ambaye ametuletea kitabu chake hiki cha bajeti ya mwaka 2013/14. Pia niwapongeze watendaji wake wote ambao walimsaidia kwa namna moja au nyengine ili kufanikisha shughuli zetu za kila siku.

Lakini pia Mhe. Naibu Spika, nimepongeza lakini hakuna kizuri kisicho ila, sasa nitadokoadokoa yale mambo ambayo kwa kweli atufanyie Mhe. Waziri wa Fedha. Kwanza Mhe. Naibu Spika, nakuja Wizara ya Uvuvi na Mifugo.

Mhe. Naibu Spika, wakati tunapitisha bajeti ya wizara hii na hili tabu nimeliangalia tena sasa hivi hili tabu kubwa, sijui ni namna gani wizara au Wizara ya Fedha imewapa fedha maendeleo ya uvuvi pesa ambazo hazitokidhi haja. Namuomba Mhe. Waziri pamoja na mtendaji wake mkuu bado waangalie wizara hii jinsi fedha ambazo amewapa. Shilingi milioni mia moja Mhe. Naibu Spika, itafanya nini na itaacha nini, wakati idara hii ilikuwa ina mradi wa *MACEMP* sasa hivi *MACEMP* haupo tena na tuishukuru *MACEMP* imesaidia sana katika Idara hii ya Maendeleo ya Uvuvi. Je, nauliza suala hili wale ambao wamepata mambo kutokana na *MACEMP* watafanywa vipi kama Idara hii ya Maendeleo ya Uvuvi imepewa shilingi milioni mia moja. Namuomba Mhe. Waziri akija hapa anipe majibu sahihi au ndio tunaacha halafu wale ambao wameshajiendeleza tuwaachie tena waanguke chini tuje tuanze alifu kwa ujiti. Hilo moja.

Lakini Mhe. Naibu Spika, nije katika ukurasa huu huu wa 26 ambao umesema kwamba: “Kuendeleza kwa utekelezaji katika kuimarisha miundombinu hasa ya barabara na viwanja vya ndege”. Mimi nitazungumzia Viwanja vya Ndege Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, siendi kwenye Kiwanja cha Unguja watajijua wenyewe mkorogovyogo ulivyotokea, nakwenda kwenye Kiwanja cha Ndege cha Pemba. Kiwanja hiki cha Pemba ni mara nyingi tunapiga kelele humu ili angalau nacho kiwe cha kuvutia, lakini kila siku ikija Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na Bajeti hii yanabakia katika vitabu. Namuomba sana Mhe. Waziri kwamba katika mambo yake yote basi kipaumbele kipewe kiwanja cha ndege cha Pemba angalau kwa sababu na sisi sasa hivi kule Pemba kidogo utalii unaaza kujitokeza.

Mhe. Naibu spika, jana nilikuwa na Mhe. Miundombinu na Mawasiliano Pemba, asubuhi ghafla lilitoka wingu kubwa sana la mvua ikawa kiza, tukaona sasa kwa kweli ndege hazitaweza kutua, lakini Mwenyezi Mungu akaleta rehema zake ikanyesha mvua kubwa sana na upepo mkubwa sana. Sasa najiuliza jamani, kuliulizwa suala hapa kuhusu taa za Kiwanja cha Ndege limekomea wapi Mhe. Waziri uje unambie. Hivyo kweli tunakuwa na kiwanja cha ndege Pemba ni kisiwa chengine cha pili kwa sababu hatuna ufanisi, hatuna miundombinu ambayo ya kuhakikisha kwamba kiwanja kile kweli hakipanuliwi lakini angalau yale mambo madogo madogo ya kuonekana kile kiwanja kinaleta sura, tubadilike Mhe. Waziri nakuomba, nakuomba Kiwanja cha Ndege cha Pemba tuhakikishe tunakibadilisha.

Mimi Unguja sizungumzi kwa sababu Unguja kila siku kunatengenezwa, leo kimeshapanuliwa kiwanja cha Unguja hebu jamani turudie ule msemo wa Marehemu Karume, tunapofanya Unguja na Pemba tuanzishe, kitu kikianzishwa Unguja Mhe. Naibu Spika kwa nini hatufanyi na Pemba, tuangalie matunda aliyotuachilia marehemu Karume, akiweka jiwe Unguja na Pemba analiweka jiwe, likinyanyuliwa Unguja na Pemba linanyanyuliwa kuna matatizo gani. Mimi sitaki nizungumze mengi. Kwa sababu uchumi wan chi hii tukiacha utalii unatoka Pemba Mheshimiwa, uchumi wa nchi hii karafuu inatoka Pemba kuna tatizo gani angalau kuangalia mambo baadhi ya mambo muhimu ambayo Pemba yako kwa nini tusiyafanye? Mhe. Waziri nakuomba na watendaji wakeo mnapopanga mipango yetu muhakikishe miradi Pemba nako inatekelezwa ipasavyo.

Nikiondoka hapo Mhe. Naibu Spika, nije katika Mfuko wetu wa *ZSSF*. Wenzetu kule Bara wamebadilisha wameweka mipango yao mizuri, namuomba Mhe. Waziri *ZSSF* na sisi tupange tubadilishe sheria, kwamba tusiweke ile miaka 60. Kuna watu Mhe. Naibu Spika, washafariki hawana watoto, hawana jamii, pesa zao azionekani. Namuomba sana Mhe. Waziri jambo jema tuliige na huu Mfuko wetu wa *ZSSF* hapa basi tuwaachie wenyewe wafanyakazi na uhuru wao, mtu kama kafukuzwa kazini anaambiwa hupati chako mpaka ufike miaka 50 au 60, hebu Mhe. Waziri ukija nieleze kidogo suala hili kwa sababu watu wanalalamikia snaa Mfuko huu.

Namuomba Mhe. Waziri ate atufafanulie vizuri kama kuna sera, kuna sheria, kama kuna vifungu vyovyote vile basi aje atueleze.

Nikiondoka hapo Mhe. Naibu Spika, na mimi niingie ingawa yameshazungumzwa lakini si vibaya. Mhe. Naibu Spika, mimi niwapongeze sana wakulima wetu wa Zanzibar, jinsi wanavyojituma na jinsi sasa hivi unavyoona matunda mengi sana yanapatikana Zanzibar lakini kutembea tunatembea, tunakwenda India, China, Marekani, Seychelles tunaona kuna tatizo gani la kuchukua lile zuri ambalo la viwanda vidogo vidogo kuja kuangalia matunda yetu tumemuachia Bakhressa peke yake. Sasa hivi embe huinunui inaaza kununuliwa ndani ya mwembe wakati mauwa nitageuka jamaa zangu wa Ole watanisamehe, wakikodi maembe hukodi ule mwembe wenye mauwa mengi sasa wakati embe zimeshaanza kutokeza unakwenda unafagiliwa yale mauwa yote yanawekwa chini ya mwembe kisha unaambiwa, "weye kunnunua mauwa hwenunua embe, embe ni zangu mwenyewe weye kunkuja kodi mauwa. Sasa haya yalipukutika maua yote ni yako haya".

Sasa natoa mfano huo watanisamehe jamaa zangu lakini natoa mfano huo, wenyewe wananitizama hapa, watanisamehe kwa sababu dhamira ya serikali ni kuhakikisha wananchi wake wanaondokana na umasikini. Namuomba Mhe. Waziri afanye mbinu za makusudi Pemba tuna mabungo ambayo ni juisi pekee *international* hebu tuisambaze huko nje, Pemba ina embe, ina ndizi nyingi sana, Pemba ina mazao mengi Mhe. Waziri tuyafanyie mbinu ile Wizara ya Uwezeshaji nayo ijikite kwenye mambo hayo na mambo yote hayo hatujaona miundombinu iliyopangwa humu na serikali kwenye bajeti hii.

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme kwamba tulikuwa na viwanda hapa vingi, hili mimi nitalikumbusha. Viwanda hivi vyote vimefisidiwa hakuna kiwanda hata kimoja. Tulikuwa tuna kiwanda cha viatu hapa kikiitwa mwendo lakini mwendo kweli mana utakuendesha wewe na mguu wako kiatu hakijachanika, tulikuwa na kiwanda cha sigara, sigara zetu zilikuwa zinapendwa kuliko sigara popote pale watu walikuwa wanaagizishia hapa, Kiwanda cha Soda, viwanda vingi tu Mheshimiwa hebu Mhe. Waziri leo unatwambia viwanda vya kokoto jamani kokoto ni viwanda? Unawambia viwanda vya kokoto, viwanda vya mchanga kwa kweli bado Mhe. Waziri tujitahidi ili kuongeza Mfuko wa Serikali ambapo kama vile havipo basi tufanye vyetu kama vile tu wala tusitake makubwa mana uwezo hatuna.

Lakini pia nizungumzie Kiwanda cha Mahonda kulikoni Mhe. Waziri kiwanda hiki! Hebu tuje tuelezwe kulikoni! Kinafanya kazi, kinazalisha nini, naomba aje atueleze ili wananchi wajue matunda yao.

Mwisho kwa kuheshimu wakati wako Mhe. Naibu Spika, mana mtu sadaka hutoa nyumbani kwake kwanza, namuomba Mhe. Waziri na kwanza nimpongeze sana kwamba alikwenda akakiona kile Kituo cha Afya cha Bwagamoyo, nimpongeze na kituo kile ameahidi na amesaidia. Lakini namuomba kupitia kwake tena kwamba kile kituo kiko katika hali nzuri namuomba arudi tena Mhe. Waziri ili tukamilishe kile kituo na wananchi na wao wafaidike na matunda yao ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Baada ya kusema hayo naunga mkono kwa asilimia mia moja bajeti hii ya serikali, ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote naomba nimshukuru muumba wetu Mwenyezi Mungu *Azza Wajalla* kwa kutujaalia kuwa hai na wazima tukakutana tena katika kikao hiki muhimu cha Bajeti ya Baraza la Wawakilishi. Nikushukuru na wewe Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi kutoa mchango wangu.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, naomba uniruhusu nimshukuru na kumpongeza Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo mpiga kura wangu Mhe. Omar Yussuf Mzee kwa kuwasilisha bajeti yake hapa vizuri na kwa ufasaha mkubwa.

Mhe. Naibu Spika, kama tulivyoelezwa katika semina mbali mbali ambazo Ofisi yako imejitahidi kutufanyia kwamba bajeti kimsingi ni Mpango wa Mapato na Matumizi, tunakusudia kukusanya kiasi gani na tunapanga kukitumia vipi. Mhe. Naibu Spika, kama ningeambiwa nifanye mpango mzuri kwa mimi ambaye si mchumi ningesema basi njia zake mbili za kuhakikisha mafanikio, kwanza ni kukusanya na kudhibiti mapato na pili ni kuchunga matumizi, mimi ningesema hivyo.

Sasa Mhe. Naibu Spika, nadhani suala la msingi ambalo litatukabili wakati tunachambua hotuba hii ya bajeti kuu na baadae bajeti za kila wizara ni kwamba yale ambayo Mhe. Waziri ametwambia katika ukurasa wa 16 wa hotuba yake katika kuelezea bajeti iliyopita ya matumizi, kwamba katika kipindi cha tathmini matumizi halisi yamefikia jumla ya shilingi 428 bilioni sawa na asilimia 98.6 ya makadirio ya miezi tisa basi tuione tija yake. Hizi shilingi 428 bilioni fedha za walipa kodi wa Zanzibar tuzione tija yake Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika, lakini wakati nasema kimsingi bajeti inatwambia ni mpango wa mapato na matumizi na nikaitafsiri kwamba madhumuni yake ni kukusanya na kudhibiti mapato kwa upande mmoja na kwa upande wa pili kuchuma matumizi, mimi ningetegemea vile vile ili kufikia kuongeza mapato na kuongeza matumizi kwa faida ya wananchi wa Zanzibar basi bajeti vile

vile iwe inaakisi dira ya nchi. Ikiwa bajeti yetu Mhe. Naibu Spika, itakuwa kila siku ni bajeti ya kupanga tunapata hiki tutakitumia vipi tu, lakini katika kutumia hatuelekezi matumizi yetu katika vipaumbele ambavyo vitatujengea uzalishaji mwengine wa mapato siku za mbele bajeti hiyo itakuwa haitusaidii kitu wala haiwasaidii kitu wananchi wa Zanzibar Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, bajeti sio tu kuwa tuoneshe ukuaji wa uchumi kwa maana ya kuongezeka huduma na rasilimali katika nchi lakini pia bajeti siku hizi kuna dhana inayoambiwa bajeti ya kumsaidia masikini, ukuaji unaomsaidia masikini ionekane hivyo, kwamba kipato cha wananchi wetu nacho kionekane kinaongezeka, huduma za jamii zinazowafikia zinaongezeka na ubora wake pia unaongezeka.

Lakini vile vile bajeti nzuri ioneshe inatengeneza ajira kiasi gani kila mwaka. Tumeambiwa katika semina kule kwamba kuna asilimia 14 tukaambiwa ni kama dola laki moja. Mimi Mhe. Naibu Spika, hiyo naitia walakin, naamini kuna vijana zaidi ya laki moja ambao hawana ajira hapa Zanzibar na hali halisi ukipita tu mitaani inaonesha haitaki hata kufanya uchunguzi unaiona Mhe. Naibu Spika.

Lakini Mhe. Naibu Spika, la mwisho katika *vision* basi bajeti ioneshe kukua kwa utajiri, kama bajeti haituelekezi huko ikawa bado ni mpango tu wa mapato na matumizi kikawaida tu, basi itakuwa yale aliyotwambia Rais wetu Mhe. Ali Mohammed Shein kwamba itakuwa ni *business as usual* kufanya kazi kwa mazowea tunakwenda tukirudi hakuna kubwa ambalo linakuwa. Na tija ya hayo Mhe. Naibu Spika, iwe nini, tija ya haya iwe kwamba hatimae tuone kuwa gharama za maisha kwa wananchi zinashuka lakini kiwango cha maisha kinapanda, tuone *cost of living* zinateremka na *stainable of living* zinakua, hapo tutasema kweli Mhe. Naibu Spika, kwamba bajeti zetu zinahudumia wananchi na tunaona maendeleo katika nchi yetu.

Lakini kuyafikia hayo Mhe. Naibu Spika, umuhimu wa uongozi katika nchi ni jambo kubwa sana, ikiwa uongozi unayumba, ikiwa uongozi hauna dira, ikiwa uongozi unakosa usimamizi, ikiwa uongozi unaogopa kufanya maamuzi magumu Mhe. Naibu Spika, hatuwezi kuyafikia aliyoyataja hata siku moja.

Mhe. Naibu Spika, tukitaka kuangalia uongozi unaleta tofauti gani katika maendeleo ya nchi tuitazame nchi ndogo ya Singapore. Mhe. Naibu Spika, Singapore ilibarikiwa kumpata Bwana mmoja anaitwa Lee Kuan Yew aliyekuwa Waziri Mkuu wake wa mwanzo. Mhe. Naibu Spika, wakati Singapore inapewa uhuru katika hatua za madaraka ya ndani mwaka 1959 wastani wa pato kwa mwananchi wa Singapore ilikuwa dola 400, wakati wa kupewa uhuru Waingereza wakawavungavunga kama walivyotuvungavunga

sisi wakawabandikiza katika shirikisho la Malaysia mwaka 1963, lakini vishindo vikawashinda mwaka 1965 wakatoka wakafukuzwa katika shirikisho la Malaysia kwa sababu walichoka na vitendo vya Malaysia katika kuhudumia Singapore ikawa haipewi umuhimu.

Mhe. Naibu Spika, katika kipindi hicho ndipo Lee Kuan akafanya kazi, leo Mhe. Naibu Spika, wakati Lee Kuan anaondoka madarakani mwaka 1990 wastani wa pato la wananchi wa Singapore ni *total* kutoka US$ 400 alizozirithi mwaka 1959 mpaka likafikia wastani wa US$ 12,200 kwa mwaka. Lakini mpaka alipoandika kitabu chake hiki, kaandika kitabu kueleza uzoefu wake na kuwaambia wengine wajifunze kwake anakiita *From Third World to First: Singapore and The Asian Economic Boom* mpaka anakiandika hiki mwaka 1999 basi wastani wa pato la mwananchi wa kawaida wa Singapore limeongezeka sasa limekuwa US$ 22,000 kwa mwaka.

Lakini Mhe. Naibu Spika haitoshi, jana nimekwenda kuangalia katika mtandao na ninayo hapa kutoka katika *Website* ya *CIA* wanaweka kila nchi pale. Mwaka 2012 wastani wa pato la mwananchi wa Singapore limefikia US$ 61,400 kwa mwaka, hiyo ndio *leadership* Mhe. Naibu Spika, ukigawa hili kwa pato la mwananchi utajua kwamba kwa nini wananchi wa Singapore waishi katika maisha wanayoishi pale, dunia imepigwa na mtikisiko wa kiuchumi Singapore haikuyumba kwa sababu uongozi ulikuwa makini, mipango ya uchumi ilikuwa sahihi na usimamizi ulikuwa mzuri.

Mhe. Naibu Spika, mfano mwengine mdogo Qatar. Qatar kabla haijavumbua mafuta na gesi ilikuwa hohe hahe kama sisi hapa, wakipata kusaidiwa saidiwa na jirani zao pale wa Kiarabu. Lakini wamesimamia vizuri, maana kuvumbua gesi na mafuta si hoja. Nigeria wanayo pale vurugu tu, lakini Qatar wamesimamia vizuri. Jana nilipokuwa nikiangalia Singapore nikasema hebu nifungue na ya Qatar. Ninayo hapa Mhe. Naibu Spika.

Qatar wastani wa pato la mwananchi wake kwa mwaka hii ndio *bomb shell* Mhe. Naibu Spika, ndani ya miaka 15 marekebisho yaliyotokezea wastani wa kila mwananchi wa Qatar ni US$ 103,900 mwaka jana, naisoma hapa wanasema *Country position compared to the world is number one*, yaani ulinganisho wa pato hili kwa mwananchi ndio ya kwanza sasa hivi duniani kuliko hata zile nchi tajiri wamewafunika Qatar. Nchi ndogo wastani wa watu unalingana kabisa na wetu, lakini kwetu kunakosekana nini Mhe. Naibu Spika. Mimi nasema *leadership* pia ina *role* katika kutukwamisha.

Nilisema kikao kilichopita wengine wakanuna humu ndani kwamba wakati serikali hii inaingia madarakani imekuta miundombinu ishawekwa vizuri tu, ilikuwa sasa ni kuja mipango mizuri ya maendeleo ya kuja na miradi ambayo

itazalisha ajira na kuongeza kipato cha nchi, bado miaka mitatu Mhe. Naibu Spika, tunapigapiga maneno tu.

Mhe. Naibu Spika, wakati nazitaja takwimu hizo Zanzibar Mhe. Waziri anatwambia katika ukurasa wa 9 wa hotuba yake kwamba wastani wa pato la mwananchi wa Zanzibar ni US$ 638 kwa mwaka, watu wametoka 400, wamepiga 12, wakapiga 22, wamepiga 61 Singapore sisi tunazungumza 600. Singapore hayo yamekuja Mhe. Naibu Spika, katumia vizuri nafasi yake *strategic location* kaja na *style* za kuvutia uchumi uendelee na biashara si haba wamepiga hatua, tena wana ushindani wa nchi kama Malaysia, Indonesia, Thailand zote zina nafasi kama yeye lakini yeye kaja na ubunifu.

Mhe. Naibu Spika, sisi tuna *strategic location* kama walivyo Singapore tungeweza kuwa sisi ndio mlango kama ilivyokuwa historia ya kuingilia na kutokea Afrika Mashariki tukapiga hatua kama walivyopiga Singapore pengine hata na kuizidi Singapore. Tatizo Mhe. Naibu Spika, ubunifu, tatizo uongozi.

Mhe. Naibu Spika, nimeanza na kusema kwamba kimsingi bajeti ningeitathmini kwamba ni kudhibiti mapato na kuchunga matumizi. Kwa hivyo, naomba nilichangie la mwanzo la kudhibiti mapato. Kwa sababu Mhe. Waziri katwambia au niseme tumeambiwa tusiwe tunapiga debe tusaidie mawazo basi. Mhe. Naibu Spika, eneo moja ambalo namuomba Mhe. Waziri aje atizame katika kudhibiti mapato ni haya mashirika na mamlaka wanayoyategemea katika serikali.

Mhe. Naibu Spika, sisi *backbenchers* mmetugawa katika Kamati mbali mbali, tunakwenda kusimamia wizara mbali mbali tulizopangiwa, lakini ukifika katika mashirika ya mamlaka kuna siri kubwa, ukitaka undani unapewa zaidi ule wa idara lakini wa mashirika sijui wenzetu wa *PAC.* Namuomba Waziri alitazame kwa undani hapa wasione ndio tunatia hasara tu wakati pengine kuna watu huko wanatengeneza fedha wanazozijua wao, kwa jumla wapo Mhe. Naibu Spika, tena nataka litizamwe sana hili, sitaki kutoa mfano mmoja mmoja kwa sasa tutakuja katika mawizara tutazungumza moja moja, nitoe mfano mdogo tu Mhe. Spika, kuonesha ya jana.

Leo tuna Mamlaka ya Usafiri Baharini na Zanzibar imeanzisha usajili wa meli tuna taarifa, lakini mpaka mwaka juzi ilikuwa fedha za mawakala wetu wa kusajili meli zinakuja katika kikapu hazina *bank transfer* hazisafirishwi kwa benki. Hapa kama hukudhania kama kuna watu Mhe. Naibu Spika, utafanya nini. Kwa hiyo nimetoa mfano mmoja lakini Mamlaka, Mashirika yanapaswa yatizamwe sana mapato yake tusiwaambie tu wageni wetu hapa ruzuku wakati hatujui mapato yake vipi hilo moja Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, pili kwenye Misamaha ya Kodi. Mhe. Waziri kasema katika ukurasa wa 50 hadi 51 katika marekebisho ya hatua ya kwanza ni marekebisho ya misamaha ya kodi. Kanitajia hatua tatu pale sitaki nizirejee kwa sababu ya muda Mhe. Naibu Spika. Lakini mimi naomba bado atizame tena Mhe.Naibu Spika, watu wanaotumia vibaya sio yale maeneo aliyoyataja yeye na aitizame wizara yake kuna watu wana maswali gani.

Mhe. Naibu Spika, magazeti haya ya tarehe 13/Juni tena yote mawili ya Serikali kuna gazeti hili la kiingereza *Daily News* na la Kiswahili chake Habari Leo, wameripoti la kiingereza limesema kwa kiswahili limetafsiriwa limesema "waagizaji saruji wa nchini waimaliza nchi wapewa makadirio ya nchi ya bidhaa waagiziazo ni kampuni tatu kubwa zajichimbia Dar, Zanzibar; Taifa laingia hasara mabilioni kwa miezi mitatu".

Mhe. Naibu Spika, ningekuwa si kupoteza muda ningeisoma hii taarifa Mhe. Niabu Spika. Lakini kwa kifupi hapa imetajwa Zanzibar imeingizwa tani ishirini na tatu elfu mia tano na thalathini na moja zikiingizwa Zanzibar kutoka Pakstani ile ya Bara siitaji. Lakini kwa jumla katika kuelezwa hasara iliyopatikana Mhe. Naibu Spika, hii naomba univumilie kidogo niisome kwa sababu naona ni muhimu sana ikajulikana na Wajumbe wako.

Mhe. Naibu Spika, anasema anaizungumzia ile ya Kitanzania kwa jumla "kwa kipindi hiki cha miezi mitatu ya Februari hadi Aprili kulikuwa na hasara ya kodi kwenye saruji kama ifuatavyo katika mji wa Dar-es Salaam, Zanzibar na Mtwara tani kumi na moja elfu mia moja sabini na tano zilikadiriwa kodi ya dola 60 baada ya 90 ina thamani ya jumla ya thamani ya dola milioni sita laki sita sabini elfu mia tano baada ya dola milioni kumi elfu tano mia saba na hamsini. Asilimia 20 ya mzigo ulitolewa makadirio ya chini ile thamani halali ingepaswa kuwa dola kumi na mbili milioni elfu sita na mia tisa.

Mhe. Naibu Spika kuna na mchanganuo ya kodi hapa. Mhe. Naibu Spika, huku mnawaachia watu wanatafuna fedha namna kama hii. halafu mnakuja kutwambia tuwaongezee kodi wananchi wetu masikini wa Mwenyezi Mungu wanaoendesha *taxi* hapa, na haya Mhe. Naibu Spika, tunaomba wajiandae vizuri kama si kwenye Bajeti hii basi itakuwa Wizara yake tutataka maelezo, kwa sababu kuna majina yametajwa mpaka wakubwa wazito Serikali sitaki niwataje wananufaika na bili hizo Mhe. Naibu Spika. Nani anae-*facilitate* katika Serikali ili kupewa mbinu za namna hii wakubwa ili kuwaumiza wenzao nani Mhe. Naibu Spika? Huku wananchi wanakamuliwa kila siku. Mhe. Naibu Spika, hilo la pili katika kuangalia mapato.

Mhe. Naibu Spika, kumezungumzwa misamaha ya chakula hapa katika kodi katika kipindi cha Ramadhani tunampongeza Mhe. Waziri, kwa sababu

itawasaidia wananchi wa kipato cha chini. Lakini hapa namtaka Mhe. Waziri alitizame tena hili katika watendaji wake katika wizara yake. Kuna manung'uniko ya wafanyabiashara kwamba kuna upendeleo katika hili kuna watu huwa wananong'onezwa kabla ya misamaha haijafika wakati wa kutangazwa. Kwa hivyo, wanaleta mzigo yule mwenzake hajui ukifika wakati inatangazwa yeye ndio kwanza huwa anapata kivutio anaenda kuagiza akifika inakuwa hauwahi ule muda uliotolewa msamaha, lakini yule anakuwa keshatiwa *tick* mapema huku ameshaletwa kwa wakati ikifika umeingia kwenye kipindi cha msamaha wa kodi, uwatizame tena Mhe. Waziri watendaji wako na wizara yako kwa ujumla katika suala hili.

Mhe. Naibu Spika, jengine ni katika sekta ya kilimo sisi tunatumia utalii sehemu kubwa sana. Lakini utalii huu tumeuunganisha vipi na sekta nyengine katika *economic*. Leo mahoteli mengi mpaka vifaa vidogo vidogo na mazao madogo madogo yakatoke Bara. Tumeisaidia vipi sisi kusarifu mazao yanayozalishwa nyumbani na watu wetu wakapata ajira na wakapata kipato, tunaambiwa matunda yanaozeana Pemba wacha hapa Unguja. Leo aibu Zanzibar ununue *juice* kutoka Dubai kwenye jangwa wakati kuna matunda yanaozeana hapa yangeweza kuingiza mapato haya kwa maana ya kodi na ajira wangelipa kodi wanaopata ajira wangeongeza mapato kwa maana ya kuunganisha sekta moja ya uchumi na sekta nyengine, tutafanya nini Mhe. Naibu Spika.

Lakini eneo jengine ni la kuongeza thamani katika bidhaa, wanazalisha kwa mfano Karafuu namshukuru Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko kwa jitihada kubwa aliyoifanya. Lakini sidhani na katika sekta nyengine ile ile isiishie kwake tu. Mimi namsifu nimekutana nae siku moja akanieleza kiasi gani katika masuala haya ya Matikiti maji yalikuwa yote yakitoka Bara hapa. Kawashajihisha wakulima Pemba leo kiasi kikubwa matikitiki yanatoka Pemba. Akanambia mradi wake mwengine ni wa tungule, tunaweza kufanya mengi katika haya Mhe. Naibu Spika, ikiwa kutakuwa na ubunifu na ikiwa mzigo huo hatoachiwa Waziri mmoja tu tuwe tunafanya kazi kwa pamoja. Kila mmoja katika sekta aje anasimamia akawa anafanya kazi kama hiyo.

Mhe. Naibu Spika, jengine ni Sekta ya Uvuvi. Sisi ni visiwa tumezungukwa na bahari lakini kama tutapima bahari kuu baina sisi na Tanganyika wenye kumiliki bahari kuu hasa ni sisi kama tutagawana mipaka kwa asili ilivyokuwa sisi tuna sehemu kubwa. Leo tumekwenda kuunganisha uendeshaji wa Bahari Kuu hesabu hazikai sawa Mhe. Naibu Spika, mwaka juzi nilitoa mfano hapa Naibu Waziri wa Uvuvi katika Bunge la Muungano katoa takwimu tofauti za mapato ukifanya hesabu haiji asilimia 40 kwa alivyotutajia Mhe. Said Ali Mbarouk alipokuwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Kuna kudanganyana sana Mhe. Naibu Spika katika hili. Sasa tungeweza

kupata mapato mengi kama tungeweza kusimamia uzuri sekta ya uvuvi na hapo Mhe. Naibu Spika, kuna maeneo mengi tu, kuna suala la kusarifu mazao ya baharini, kuna suala la uhifadhi wa bahari, kuna *Marine Park* zinaingiza mapato, kuna maeneo mengi tu, kuna kuvuna rasilimali yenyewe Mhe. Naibu Spika, kote tunaweza kuingiza mapato.

Mhe. Naibu Spika, nilisema mapema kama Bajeti makini ingekuwa inatuelekeza katika kuunda miradi ambayo hatimae ikaifungua nchi kiuchumi. Nchi yetu ni kisiwa lakini asili yake ni bahari ya kuingilia na kutokea, asili yake katika Afrika Mashariki. Lakini kulifikiria hilo kunahitaji Mhe. Naibu Spika, kuwa na mawasiliano ya uhakika ya baharini kwa maana ya Bandari na Kiwanja cha Ndege tumeshindwa, tunaimba tu Mpigaduri miaka mia Mpigaduri hakuna linalokuwa. Mwaka jana mimi na Mhe. Hamza Hassan Juma tulimwambia Mhe. Waziri wa Fedha hapa kwamba kama ikiwa nyinyi mmeshindwa labda mtutume sisi tukatafute mtu wa kuja kufanya *PPP* tupate muwekezaji katika eneo la Mpigaduri. Tumechelewa wenzetu wa Tanganyika wanatupita sana wanatengeneza Bagamoyo wamepeleka mradi ule kwa kina sisi tumetiwa kapuni mpaka leo wanatupenda sana Mhe. Naibu Spika. Lakini *Air Port* ile pale hakuna *vision* kabisa Mhe. Naibu Spika, kwa hiyo nasema haya ni maeneo ambayo nasema lazima tuyatizame. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nimalizie nukta moja katika mapato hili nataka nimtahadharishe Mhe. Waziri wa Fedha aichunge sana. Kuna taarifa kuhusu Kampuni ya *Zantel* ambayo ni mlipa kodi anayeongoza Zanzibar kwamba kuna mkakati wa kumuhamisha hapa kwa sababu ya maslahi ya baadhi yetu. Hapa Serikali kwa mwaka Mhe. Waziri wa Fedha wanapata bilioni 21 kutoka *Zantel*.

Lakini *Zantel* Mhe. Naibu Spika, wanahisa wake ni Serikali ya Zanzibar ambayo ina asilimia 18, Kampuni ya *MECCO* ina asilimia 17 na *Part of Etisalat* asilimia 65. Kwa mujibu wa hati yao wanasema ili ufanye maamuzi unahitaji kuwa na hisa asilimia 75 maana yake na *Part of Etisalat* akijiunga na mmoja tu katika hawa wawili wadogo wadogo waliobakia basi anaweza kufanya maamuzi. Sasa pale palifanyika mkakati Mhe.Naibu Spika, wakitumika baadhi yetu humu humu ndani sikusudii Baraza la Wawakilishi yaani ndani ya Zanzibar, wametumika kutaka kukiuka miko, matokeo yake na yeye sasa anataka kulipiza kisasi kwa Zanzibar kutaka kufanya maelewano na *Part of Etisalat* kufanya maamuzi ya kuihamisha hapa *Zantel* kuipeleka Bara. Ikihamishwa Makao Makuu Mhe. Naibu Spika, na wanao uwezo wa kujiunga pamoja, maana yake hizi kodi zinazolipwa za milioni ishirini na moja zitaishia Tanganyika kwenye udugu wa damu na sisi tutaishia hapa kukamuana sisi wenyewe tu. Nataka nipate maelezo kwa kina kwa sababu naambiwa kwamba hawa hawaridhiki wamemtaja mmoja katika Wajumbe wa

Bodi ambaye wanahisi kama yeye ndiye anawaendea kinyume alipotaka kufanya maamuzi pamoja na *Part of Etisalat* kwa niaba ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, tuambiwe ukweli katika suala hili Mhe. Naibu Spika. Mhe.Naibu Spika, hayo ni katika mapato ya ndani.

Naomba sasa kidogo Mhe. Naibu Spika, nizungumzie mapato mengine ambayo tunakoseshwa. Mhe. Naibu Spika, katika hotuba hii Mhe. Waziri kataja pale kwamba katika Bajeti Fedha za nje *GBS* mwaka huu tumepata bilioni nadhani 20. Kasoro tu ya mwaka jana ilikuwa bilioni 24, sasa wenzangu wamezungumza hapa Mhe. Hija Hassan Hija kwamba kuna kutoingiziwa fedha zetu za misaada ya kibajeti lakini vile vile na kuna zile *PAYE*. Sasa Mhe. Naibu Spika, nasema hebu Mhe. Waziri wa Fedha atwambie kweli Mhe. Mohamedraza Hassanali alitaja na Mhe. Hija Hassan Hija akarejea na sisi tunaendelea kusema kwamba taarifa tulizonazo ni kwamba kwa muda wa miezi mitatu mpaka minne fedha tulioambiwa imeshafika makubaliano kwamba sasa kodi ya *PAYE* italetwa hapa haijaingia tuelezeni ukweli mnatuficha nini? Mnawaficha nini wananchi wa Zanzibar? Au ndio faida ya Muungano na Serikali mbili kuelekea moja Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, katika *GBS* mimi nimeamua kufanyakazi ya ziada Mhe. Naibu Spika, nimekwenda kuitafuta Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha ya Jamhuri ya Muungano nimechukua kurasa tatu tu Mhe. Naibu Spika, ili Mhe. Waziri wetu atufahamu tunachokizungumza. Mhe. Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano ana ripoti katika Bunge Misaada na Mikopo ya Nje ino masharti nafuu. "Anasema katika mwaka 2012/2013 Serikali ilikadiria kupata shilingi bilioni 842.5 kama misaada na mikopo ya kibajeti. Hadi kufikia Aprili 2013 Serikali ilipata misaada ya mikopo ya kibajeti ya shilingi bilioni 645.5 ambazo ni sawa na asilimia 77 ya makadirio ya mwaka. Kwa upande mwengine shilingi bilioni 443.4 zilipokelewa kupitia mifuko ya kisekta ikiwa ni sawa na asilimia 107 ya makadirio ya shilingi bilioni 415.1 kwa mwaka.

Mhe. Naibu Spika, hoja yangu nini? Hesabu ya haraka haraka tu yangu niliyekuwa sijasoma uchumi kama Mhe. Omar Yussuf Mzee kwamba ukichukua zile 645.4 ukafanya asilimia 4.4 ukafanya asilimia 4.5 mambo ya Zanzibar basi tulipaswa tupate 29.043 bilioni. Mhe. Waziri wa Fedha katuripotia tumepewa 20 bilioni, hizi sio zilizokisiwa zilizopokelewa mimi situmii makisio lakini zile alizoripoti kwamba wameshazipokea hadi Aprili tulipanga tupate 29.0 maana yake ni upungufu wa bilioni 9 kwa Zanzibar katika hiki kifungu kimoja, ndugu zetu wa damu hawa mnawatetea tuendelee na mfumo wa Serikali mbili kuelekea moja Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, katika kisekta na hili nimewahi kuliuliza hili kwamba katika *GBS* ile misaada ya kibajeti je kuhusu sekta maana Mawaziri hawa wanaojiita wa Jamhuri ya Muungano katika sekta zisizokuwa za Muungano wakienda nje hawasemi sisi ni Mawaziri wa Tanganyika wanasema wa Jamhuri ya Muungano. Kwa hivyo wanapoomba msaada ukiwa wa maji, ikiwa kilimo, ikiwa mifugo, uvuvi haya si ya Muungano ikiwa ardhi na sisi tunayo kinachotolewa kinaambiwa kuwa ni cha Jamhuri ya Muungano wamepata 443.4 bilioni kama tungepewa asilimia 4.5 walikuwa watupe sisi bilioni 20. 043 ziko wapi Mhe. Naibu Spika. Mhe. Naibu Spika, tungekuwa tunakwenda kujiwakilisha sisi wenyewe tungepata ngapi?

Mhe. Naibu Spika naomba univumilie sana kwa sababu haya ninayoyasema ni muhimu sana kwa wananchi na kwa Mhe. Waziri wa Fedha kuyajua ili tujue mfumo huu uliopo mnaoutetea wengi wenu unatukandamiza kiasi gani.

Mhe. Naibu Spika: Jitahidi zimebakia dakika tano.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Najitahidi Mhe. Naibu Spika, utaniongeza na tano nyengine nimalizie kazi yangu kwa maslahi ya wananchi wa Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, kitabu hiki ukurasa wa 57 Bajeti inayokuja Mhe. Waziri wa Fedha anakadiria kwamba kutoka katika *GBS* anakadiria kwamba bilioni 40 katika ukurasa wa 57. Lakini Mhe. Naibu Spika, hii haiwiani na kile alichokieleza Mhe. Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano katika Bajeti yake ya Muungano. Katika bajeti yake inasema hivi naomba niinukuu ". Katika mwaka 2013/2014 Serikali ilitarajia kupata misaada na mikopo iliyokuwa na masharti nafuu kiasi cha shilingi bilioni 3855.2 maana yake kutoka kwa Mashirika ya Maendeleo. Kati ya hizo misaada ya mikopo ya kibajeti ni shilingi trilioni moja mia moja sitini na tatu bilioni nukta moja na misaada na mikopo katika miradi ya maendeleo ni shilingi trilioni mbili mia moja tisini na moja bilioni nukta sita, na mifuko ya kisekta ni shilingi bilioni 500, ukizigawa Mhe. Naibu Spika, hizo kwa asilimia 4.5 katika hii trilioni moja mia moja sitini tatu bilioni basi Zanzibar ilikuwa tupate 52.3 bilioni. Sasa kwa nini kitabu cha Mhe. Waziri wa Fedha kinatwambia tutapata bilioni 40. Hapa bilioni 12 zimefyekwa na ndugu zetu wa damu hawa wanaotupenda mnaowatetea.

Mhe. Naibu Spika, katika lile fungu la misaada na mikopo kwa jaduweli la Maendeleo mbona wanapokwenda kuomba wanaenda kuomba kwa ajili ya Tanzania ingelikuwa watupe asilimia 4.5 tu katika trilioni zile nilizozitaja hapa mbili mia moja tisini na moja bilioni basi walikuwa watupe bilioni 98.6. Katika hizi bilioni mia tano za kisekta tungepewa 22.5 bilioni kwa jumla Mhe. Naibu Spikia, kama kila mgao huu sio watu wanaotoka mbali hawa

watu wanaotoka nje wanaokwenda kuomba kwa Jamhuri ya Muungano sisi tulikuwa tupate 163.4 bilioni.

Mhe. Naibu Spika, nitoe mfano wa mwisho katika mikopo ya Elimu ya Juu. Mbona katika vipaumbele vya Bajeti ni kuwasomesha watoto wawe wanaelimika wajenge Taifa letu. Mhe. Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano kwa mwaka jana Serikali imetoa mikopo kiasi cha shilingi bilioni 326.1 wanafunzi tisini na sita elfu mia tatu hamsini wa elimu ya juu. Mhe. Naibu Spika, ingekuwa hizi tunapewa asilimia 4.5 tu sisi tulipaswa tupewe 14.67 bilioni mahitaji yote ya Mhe. Waziri wa Elimu ni bilioni 5. Hii tungesomesha mara tatu zaidi.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie yaliobakia, kwa dakika tano nilizokuomba yaliyobakia. Mfano mwengine hai Mhe. Naibu Spika, katika haya mapato nije kwenye gesi na mafuta. Mhe. Naibu Spika, kuna mapato yetu sisi katika mashirika haya *TCRA, TCAA, TTCL, TPC, TPBC,* Posta hao, mimi nimeingia Barazani mwaka wa tatu huu katika Bajeti ya tatu kila mwaka huwa nahoji mapato yetu sisi kiasi gani mbona hayaripotiwi katika vitabu vyetu vya Bajeti. Mara ile hii imeingizwa katika Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi nimemuhoji Mhe. Waziri na nimemuhoji Katibu Mkuu wao wenyewe hawajui, kwa sababu hatupo hatupewi. Lakini katika gazeti limeripotiwa *Vodacom* peke yake Mhe. Naibu Spika, kailipa *TCRA* kodi ya Mashirikia bilioni 36, kuna *TIGO* kuna *Zantel* kuna *Airtel* mbali na mapato mengine ya *TCRA, TCRA* moja tu Mhe. Naibu Spika, kuna kwenye mapato katika *TCRA* kuna *TPBC* huko wametoa vitambulisho vya mafuta miaka yote hiyo hakuna shilingi iliyovuka maji ikaja Zanzibar.

Lakini Mwisho namsifu Mhe. Waziri Omar Yussuf Mzee vile anavyoliheshimu Baraza la Wawakilishi kikao kilichopita hapa alisema kuna safari ya Mkutano wa kimataifa *World Bank* akapeleka watendaji wake. Baada ya mkutano ule Mhe. Naibu Spika, tumesoma katika mtandao, Tanzania imesaini mkataba wa mkopo na Benki ya dunia wa kupewa dola za kimarekani 196.5 milioni kwa ajili ya kukuza sekta ya mafuta na gesi asilia, tumepata kiasi gani sisi na mpaka leo mafuta na gesi asilia haijatolewa katika Muungano tumepata kiasi gani katika kuendeleza sekta hii.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo nasema vyanzo vya mapato tunavyo na tunaposema tunataka Mamlaka kamili, tunataka mamlaka ya kudhibiti vyanzo hivi tuziweke wenyewe mapato haya yaingie katika Zanzibar hatuwezi kukubali kuwa watumwa wa Tanganyika kuwa koloni lao hatukubali Mhe. Naibu Spika, hata siku moja katika hili.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niingie katika matumizi mwanzo nilikuwa naiomba Serikali sasa namuomba Mhe. Rais wangu sana bado mimi nasema katika matumizi moja katika linalotugharimu sana ni ukubwa wa Serikali yetu. Mhe. Naibu Spika, Kenya juzi walipomaliza uchaguzi Katiba yao iliwaambia kuwa wanyama wazuri 18, kuhudumia nchi ya watu milioni arubaini naa, leo sie tuko milioni moja na laki tatu kwa sensa ya juzi tuna mawaziri 19, 16 wenye wizara, watatu wasiokuwa na wizara yoyote wapo tu wanakwenda na kurudi. Huu ni mzigo kwa wananchi wa Zanzibar wanaolipa gharama hizi na hawa kila wizara ukiunda ina na watoto wake huko chini kuna maidara, mashirika kuna Wakurugenzi fedha inakwenda hiyo namuomba Mhe. Rais wangu aliangalie tena hili kama alikuwa na majaribio na Serikali yake yuko kati kati ya kivuli chake wakati umefika tuone tumepata faida gani, hivi vipaumbaele tulivyoviweka vimesaidia nini kwa mwananchi wa Zanzibar Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo nilikuwa nataka kulizungumza liangaliwe ni kwenye maeneo ya rushwa bado kuna mabaya mengi. Sasa hivi muda hauruhusu nitoe mfano nitakuja kuzungumza katika wizara moja moja. Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika, nimalizie maelezo yangu niseme kwamba mimi kwa kifupi sikubaliani na hii viongeza mlivyowapa kuwakamua watu. Mhe. Naibu Spika, watu kama wanaendesha gari za abiria *taxi* na gari za watalii, siku moja nimemwambia mtu aniorodheshee aliorodhesha zile kodi, tozo, leseni 17 kwa ujumla wake halafu unakwenda kumuengezea tena. Kuna Utalii ndio tegemeo letu tunaendelea kwenda kukamua tu Mhe. Naibu Spika, ng'ombe watatoka damu kasema jana Mhe. Salmin Awadh. Vyanzo vya mapato yetu yafuatiliwe.

Mhe. Naibu Spika, katika yote yale pale aliyoyaongezea pale anafikiria kutafuta alivyotwambia katika ukurasa wa 54, 16 bilioni na katika hili pia namuomba akakague hesabu zake isijekuwa kuna mchezo wa kutaka kutuibia hapa Mhe. Naibu Spika. Mimi nimejumlisha ile vyanzo vya marekebisho vyote kuanzia "a mpaka l" nimepata jumla bilioni 21.89 yeye katwambia hapa 16.9 bilioni hizi zimekosewa kujumlishwa wakati zimepita katika mikono mingi au zimefunikwafunikwa wapate kuzikusanya zote halafu zitiwe kwenye mifuko ya watu nilikuwa naomba maelezo katika hilo Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Spika, katika hotuba yake Mhe. Waziri wa Fedha kataja na katika hili nitawaudhi wenzangu lakini mtanisamehe, mimi suala ambalo liko ukurasa wa 36 wa hotuba yake Mhe. Naibu Spika, kazungumzia kuongeza maslahi ya wafanyakazi na Wawakilishi. Mhe. Naibu Spika, mimi siungi mkono kuongezwa maslahi ya Wawakilishi, mimi siungi mkono kuongezwa maslahi ya viongozi wa kisiasa hapo walipofika, tutizame uwiano uliopo mkubwa sana wanaolipwa wataalamu wetu, leo madaktari wanamuhangaisha Mhe.

Waziri wa Afya Mhe. Juma Duni wanataka kuongezewa kiasi kidogo tu hii ni haki kweli kwamba tujiongezee sisi au tuongezewe sisi wakati kuna watu wanatumika usiku na mchana. Mimi siungi mkono Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Malizia

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Naibu Spika, la mwisho kabisa Mhe. Naibu Spikia, nafurahi katika hotuba hii kumezungumzwa vile vile kusherehekea miaka 50 ya Mapinduzi, nasema kama kweli tunataka kuyaenzi Mapinduzi, na kama kweli tunataka kumuenzi Mzee Karume basi la kwanza aloleta Mzee Karume ameleta Mapinduzi ili Zanzibar ijitawale wenyewe chini ya mamlaka yake kamili tuliheshimum hili.
Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo nakushukuru kwa kunivumilia nitaiunga mkono hoja ikiwa nitapata maelezo ya kina kwa hoja zilizotolewa. Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante Mhe. Naibu Spika na mimi kunipa nafasi hii kuchangia hotuba hii. Pili nampongeza Mhe. Waziri wa Fedha pamoja na watendaji wake wote kwa kuandaa Hotuba hii ya Makadirio na Mapato ya Matumizi.

Mhe. Naibu Spika, najua mengi yamezungumzwa na wenzangu nitajaribu kusisitiza na mengine kutaka ufafanuzi. Mhe. Naibu Spika, mimi nitaingia katika maeneo manne. La kwanza Bodi ya Mapato, hali ya uchumi Zanzibar, vipaumbele pamoja na miaka 50 ya Mapinduzi.

Katika kitabu cha hotuba ya bajeti ya mwaka jana ilieleza kuwa Bodi ya Mapato imepangiwa kukusanya jumla ya shilingi mia moja na sitini na mbili milioni ikiwa ni ongezeko la asilimia 35 ikilinganishwa na makusanyo halisi ya mwaka 2011/2012. Ili kufikia lengo mikakati ifuatayo inatarajiwa kutelezwa ikiwemo kwanza hii ni hotuba ya Bajeati ya mwaka jana ukurasa 16:

1 kuhakikisha kuwa wafanyakazi wote wanasajiliwa na wanalipa kodi ipasavyo.
2 walipakodi wanafanya mauzo katika maeneo ya biashara wanatoa ankara za kodi kwani hivi sasa walipa kodi hawa hawatoi stakabadhi wanapofanya mauzo.
3. kuongeza ukusanyaji wa mapato yatokanayo na Sekta ya Utalii kwani hivi sasa kuna baadhi ya hoteli ambazo ziko kwenye kiwango cha juu duniani nyota nne na nyota tano hutumia viwango vidogo sana kulipa kodi ikilinganishwa na hoteli yenyewe.

Mhe. Naibu Spika, katika makusanyo mwaka huu katika Bodi ya Mapato imekusanya asilimia 86 sasa nataka ufafanuzi kwa Mhe. Waziri hii asilimia 86 iliyopatikana wakati lengo lilikuwa ni asilimia mia moja je, mikakati hii imetekelezwa ipasavyo ambayo walisema watakusanya mapato kutoka kwenye hoteli ambazo ziko katika viwango vya juu lakini wanalipa kodi kidogo mbali na kodi nyengine za stakabadhi za mauzo. Kwa hiyo Mhe. Waziri wa Fedha naomba unieleze hapa hii mikakati aliyoipanga kufikia asilimia mia moja imetekelezwa vipi imefatiliwa na kama imefatiliwa matokeo yake yakoje.

Mhe. Naibu Spika, nitakwenda kwenye hali ya Uchumi ya Zanzibar kitabu cha Bajeti *page* 25 na 26. Lakini mimi nitakwenda kwenye kipengele ambacho kinasema Matarajio ya ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2013 yanatokana na mambo yafuatayo. Nitakwenda kwenye kipengele cha 7 ambacho kinasema kuvutia wawekezaji katika kuimarisha maendeleo ya viwanda vidogo vidogo nchini.

Mhe. Naibu Spika, sekta ya viwanda ni sekta muhimu sana katika nchi yetu, sekta ambayo inasaidia kunyanyua pato la nchi inasaidia kuongeza ajira. Kwa hiyo hapa nilikuwa na sisitizo tu kwa Serikali ijitahidi kujaribu kuwashawishi wawekezaji ili waekeze ili wawekeze katika sekta hii.

Pia nampongeza Mhe. Rais wa Zanzibar Mhe. Ali Mohd Shein katika ziara yake China alizungumzia suala zima la uwekezaji na alitoa maelezo kuhusu watu wa china kuja kuekeza viwanda katika Serikali yetu ya Zanzibar nampongeza sana kwa hilo.

Hapo nyuma ilikuwa viwanda haziwezi kuekezwa kwa sababu tatizo kubwa lilikuwa ni umeme. Kwa bahati nzuri umeme sasa hivi upo wa uhakika kwam hiyo sekta ya viwanda ikiimarika nahisi suala la ajira litapungua kidodgo kidogo.

Mhe. Naibu Spika, nitaenda tena kwenye hivi vipaumbele vya Serikali, vipaumbele kwa mwaka huu ni kuimarisha huduma za afya, elimu, ajira kwa vijana kuimrisha ustawi wa jamii, kuimairisha uchumi na kuimarisha Mashirikiano ya sekta binafsi na umma. Mimi nitazungumza suala la ajira najua wengi wamezungumza lakini nasisitiza tu. Suala la ajira katika Serikali yetu ni changamoto kubwa na itazidi kuwa changamoto kwa sababu karibu asilimia 44 ya vijana hawana ajira na katika *GBS* ya mwaka 2010/2011 imeeleza kuanzia mwaka 0 mpaka 19 kuna asilimia 55 hawa baada ya miaka mitatu minne mitano pia wanategemea ajira hawa. Kwa hivyo tatizo la ajira litaengenezeka kuwa changamoto katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, ninachoomba Serikali ijitahidi ijikite sana katika suala hili ili kuwapunguzia mzigo vijana wetu ambao wengi wamevunjika moyo hawana ajira. Kwa hiyo ikijiekeza sana kwenye viwanda itapunguza tatizo kubwa la ajira.

Mhe. Naibu Spika, suala la miundombinu hasa kwa upande wa barabara. Serikali imetumia fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa barabara na baadhi ya barabara hazijakamilika, na naadhi ya barabara nyengine pia zinaharibika kutokana na kutopatiwa fedha ili kukamilisha miradi hiyo. Hapa ni kuiomba serikali hizo fedha ambazo zimekadiriwa kuingizwa katika ujenzi wa miundombinu ya barabara basi ijitahidi izitengeneze, na pia isimamie matumizi yake ipasavyo, ili kuleta maendeleo katika taifa letu.

Mhe. Naibu Spika, nitazungumza suala la miaka 50 ya Mapinduzi. Ni siku adhimu sana katika nchi yetu, siku ambayo tumeikomboa nchi yetu, waasisi wetu Maalim Abeid Aman Karume alitutoa katika hali ambayo tulikuwa tukitawaliwa. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri siku hii ambapo mwakani tutatimia miaka 50, ijitahidi ifanye maadhimisho ya kihistoria ili kuienzi hii siku ambayo ni kumbukumbu kwa watu wote wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, jengine ni suala la elimu. Sekta ya Elimu naiomba serikali ijitahidi, kwa sababu sekta ya elimu ni muhimu, na sekta hii ambayo inategemea kutoa wataalamu bora wa baadae. Kwa hivyo, moja katika vipaumbele ni elimu na afya. Kwa hivyo, zile fedha ambazo zimetengwa katika kuimarisha vipaumbele hivi, naomba serikali ijitahidi sana kuzipatia hizo fedha, izisimamie na kuzikagua ili kuona fedha hizi za serikali za walipa kodi wetu zinatumika ipasavyo.

Baada ya kusema hayo machache Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kupata dakika za majeruhi katika kupata mchango wangu mfupi kuhusu bajeti hii.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianze kusema kuwa Waziri ana lugha nzuri makini ya kuzungumza katika uwasilishaji. Kwa hivyo, ni mtaalamu mzuri wa mazungumzo na namsifu sana. Mhe. Naibu Spika, mimi nianze katika hali ya uchumi wa dunia. Kwa ufupi Mhe. Waziri kazungumza kuwa inapanda kwa wastani wa 3.2 kwa mwaka huu wa 2012 kutoka 4.0 mwaka jana.

Mhe. Naibu Spika, kidogo mimi sikufahamu vyema, kwamba mwaka jana ulikuwa uko juu wastani wa 4.0, mwaka 2012 ni 3.0 lakini bado unaonekana kuwa ni kupanda. Kwangu mimi kupanda ni kwenda juu na kupungua ni kuja

chini. Sasa hapa hiyo 3.2 kwa lugha yao ya kitaalamu ni kupanda, kwa hivyo haijapanda kwa 3.2 kwa sababu kwa ujumla ilikuwa ni 4.0 kwa hivyo ongezeko kama imeongezeka ni kama 0.8 kama ni kupanda au kama ni kushuka. Sasa kutoka hapo imekuja hapo, punguzo ni kasoro ya moja. Sasa kama ni kupanda haijapanda kufikia hivyo ilivyotajwa, lakini imepungua kwa kasoro fulani mpaka imefika hapo.

Hivyo hivyo katika nchi za ulaya, jangwa la Sahara na nyenginezo, zote zinaonesha kupanda, lakini kwa kweli ilikuwa haupandi na ilikuwa unateremka. Sasa nchi hizo za jangwa la Sahara hii imetajwa mwaka 2011 ilikuwa ni wastani wa 5.3, mwaka huu ni wastani wa 4.8 na bado inatajwa kwenye kupanda, lakini kwa mimi imeteremka kutoka ilipokuwa kuja hapo kwa mteremko wa wastani wa 0.5. Lakini kwa kuwa ni lugha ya kitaalamu, ningependa baada ya maelezo yangu Mhe. Waziri aje anifahamishe ili nijue kuwa kupungua nako ni ni kupanda. Hivyo hivyo kwa nchi za Afrika ya Mashariki.

Mhe. Spika, tuje kwenye pato la mtu binafsi ambalo mwaka jana lilikuwa ni 960,000 na mwaka huu limeongezeka ni 1,003,000 huko ni kupanda, kutoka 960,000 kuja 1,003,000 na ongezeko lenyewe imeongezeka kama shilingi 43,000 kwa mwaka. Shilingi hizi ni kama ongezeko la shilingi 3,583 kwa mwezi na ni kama shilingi 120 kwa siku. Kwa hivyo, pato la Mzanzibari limepanda kutoka lilipokuwa kuja ongezeko lake la mwaka mzima ni shilingi 120 kwa siku moja, ni ongezeko, kwa sababu hata kama ingekuwa ni senti tano ni ongezeko.

Mhe. Naibu Spika, tuje kwenye ukusanyaji na mchango wa kisekta katika pato la taifa. Hii iko katika ukurasa wa 9 na wa 10. Tumesema kwamba sekta ya huduma imekuwa kutoka asilimia 8.6 mwaka jana kufikia 8.7 mwaka huu, bali ni ongezeko na ni ongezeko la asilimia 0.1 wala sio ongezeko la kuwa imefika asilimia 8.7, ongezeko ni kasoro ya moja, imetoka ilipokuwa kwenda hapo.

Sekta nyengine ni ya kilimo nayo imeongezeka kutoka asilimia 1.3 hadi asilimia 2.7, hapa lipo ongezeko kubwa kidogo la asilimia 1.4 na sekta ya viwanda imeongezeka zaidi kutoka asilimia 5.8 kufikia asilimia 9.2, hapa imepanda vizuri.

Mhe. Naibu Spika, michango kwa pato la taifa kwa sekta. Hapa inaonekana kuwa sekta ya huduma imechangia vizuri kutoka 40.0 mwaka jana na mara hii mwaka 2012 imechangia 45.3 liko ongezeko. Kadhalika imepungua kidogo katika sekta ya kilimo, lakini sekta ya viwanda ambayo ongezeko lake ni kubwa, lakini mchango wake katika pato la taifa umekuwa mdogo kwa nini.

Kule katika michango imepanda hadi kufikia 9 na zaidi, lakini mchango wake katika pato la taifa umekuwa mdogo, hapa ningetaka kujua ni sababu zipi zilizosababisha kuwa iwe hivyo.

Mhe. Naibu Spika, katika ukurasa wa 12 nataka nizungumzie kifungu cha 18 na cha 19. Kifungu kimoja nataka nikizungumzie pale uliposema kuwa Baraza lako liliidhinisha bajeti ya shilingi hizo, zikijumuisha Tsh 315.8 bilioni kutoka kwa mapato ya ndani. Lakini kifungu cha 19 kinazungumzia hivi, katika mwaka wa fedha 2012/2013 serikali ilikadiria kukusanya mapato kutoka vyanzo vyake vya ndani shilingi 294.3 bilioni haya ndio yalikuwa matarajio ya serikali. Lakini bado mapato haya hayakuweza kupatikana, mapato halisi yaliyokusanywa ni machache mno katika miezi mitatu iliyobakia ya kumaliza bajeti, hili punguzo liliopo litaweza kufikia na miezi hii ni lazima iwe na bajeti.

Mhe. Naibu Spika, ni kitabu hiki cha Mhe. Waziri kina kurasa 62 na imesemwa yaliomo, yametajwa mpaka akafika pahala Mhe. Waziri kataja maandalizi ya Katiba mpya ya Jamhuri ya Muungano na maadhimisho ya miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar. Sasa yote yaliyotajwa humu ni sehemu ya bajeti, lakini baadhi ya watu wanaona kujadili haya ya katiba yako nje ya bajeti. Sasa kama yako nje ya bajeti, kwa hivyo Mhe. Waziri ulikosea kuingiza jambo ambalo halihusiki. Kwa hivyo, mawazo ya Mjumbe yasijibiwe na mtu mwengine isipokuwa ujibu wewe Waziri. Kwa sababu hili sio Baraza la malumbano. Mimi kama *backbencher* nataka nijibu hoja nimpembejee Rais anifanye niwe Waziri ili nijibu hoja.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, mimi niendelee kidogo sana kuhusu hili la Katiba ya Jamhuri ya Muungano. Wazanzibari tumepata fursa tuitumie vizuri na mchango wangu nataka nitoe mfano tu. Mhe. Naibu Spika, mwanachuoni mmoja alifika makaburini akafukua vichwa vitatu, akaokota ujiti akaanza kuvichokora. Akakipitisha kijiti kwenye kichwa cha kwanza, kijiti hakikuingia. Akachukua cha pili akakiingiza kijiti kikaingia hapa kikatokeza upande wa pili, na kichwa cha tatu akaingiza kijiti kikafika katikati hakikutokeza tena nje, hivyo hiki cha tatu alikipongeza.

Kichwa cha kwanza hakuna kiingiacho, hata kikitiwa nini hakiingii. Kichwa cha pili kimeingizwa hapa kimetokeza upande wa pili, hakuna kinachohifadhi na kichwa cha tatu kimeingizwa kilipofika katikati kikasimama, ina maana kichwa kile kinawaza na kuzingatia. Kwa hivyo, nawaomba Wazanzibari tuwe katika hiki kichwa cha tatu tupime, tuzingatie ili tuikomboe nchi yetu kutokana na ukoloni wa Kitanganyika, ahsanteni sana.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, muda wangu wa dakika 15 naomba uje unipe jioni, kwa sababu hizi ni kidogo sana nitazungumza halafu nije nimalizie jioni dakika zangu 15 kwa mujibu wa kanuni.

Mhe. Naibu Spika, baada ya dibaji hiyo naomba niendelee. Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nimuombe Mhe. Rais wetu wa Zanzibar Dk. Ali Mohamed Shein anisaidie mambo mawili. Jambo la kwanza Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Rais katika kulifanya hili Baraza letu la Wawakilishi kuwa madhubuti zaidi, kwamba pale anapokwenda katika safari zake za nje Mhe. Rais asifuatane tu na Mawaziri, aweze kuwachukua na hawa *backbenchers*, ili waweze ku-*study* mambo mengine na kuifanya serikali yake iwe madhubuti na makini zaidi pale watakapokwenda huko. Hilo la mwanzo.

Mhe. Naibu Spika, jambo langu la pili ni kumuomba Mhe. Rais kwamba ili tufanye kazi vizuri huku katika *backbenchers*, basi atusaidie Rais kuwapatia uwaziri baadhi ya hawa wanaotujibu hoja. Kwa sababu sisi huchangia huku tukategemea serikali itatujibu Mhe. Naibu Spika, lakini matokeo yake ndugu zetu hawa wengine wanatujibu huku. Kwa hivyo, awapatie uwaziri awaweke mbele ili watujibu vizuri. *(Makofi/Vicheko).*

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo naomba sasa niende moja kwa moja katika hoja hii. Kwanza niwashukuru wale wataalamu juzi waliotupatia taaluma kule. Walisema kwamba bajeti maana yake ni mwenendo wa mapato na matumizi ya serikali katika mwaka husika. Kwa hivyo unapozungumzia bajeti Mhe. Naibu Spika, lazima uzungumzie sana habari ya mapato, halafu uzungumzie habari ya matumizi. Sasa mimi hizi dakika 15 nitazungumzia habari ya mapato tu, lakini matumizi tukijaaliwa kama utafanya imani yako ili unipatie jioni dakika zangu 15 nitakuja kuzungumzia habari ya matumizi.

Mhe. Naibu Spika, katika hili serikali inapoleta bajeti hapa katika Baraza ni lazima iwe makini sana katika ku-*exhort* vyanzo vyake vya mapato, ili sisi tuweze kuwasaidia tuvijadili, tuvitathmini na kuwasaidia serikali juu ya kuviboresha vyanzo vyao vya mapato.

Mhe. Naibu Spika, inasikitisha sana kwamba serikali hii, mtoto wangu pale Mhe. Waziri Omar Yussuf Mzee hakuvi-*exhort* vyanzo vyake vya mapato. Hivyo vyanzo vyake vya mapato tulifikiria kwamba angevi-*exhort*, hakuvi-*exhort.* Kaleta vyanzo eti viwanda, kazungumzia viwanda vya mawe, kuchimba mchanga. Sasa kama uchimbaji wa mawe kama ni kiwanda, basi mimi Vitongoji ndio naongoza kwa kiwanda hicho cha mawe. Wachimbaji wa mawe kule Vitongoji Mhe. Naibu Spika, wanafanya kazi kubwa sana kama kuchimba mawe ni kiwanda.

Mhe. Naibu Spika, nataka Mhe. Waziri aniambie ni kwa kiasi gani amewawezesha wachimbaji mawe wa Jimbo langu la Wawi kule Makaani Pareni, amewasaidia nini wachimbaji mawe wa Mwambe, amewasaidia nini wachimbaji mawe wa Hanyegwamchana, amewasaidia nini wachimbaji mawe wa Matemwe kama ni kiwanda.

Mhe. Naibu Spika, sasa mimi nadhani katika jimbo langu juzi tu pale alifariki bwana mmoja alikuwa katika machimbo ya mawe, akaangukiwa na mawe akafariki. Sasa mfanyakazi huyo wa kiwanda hicho serikali iliisaidia nini familia yake. Kuna kijana yuko Mkungupigi Vitongoji Kusini aliangukiwa na mawe miezi miwili iliyopita akafariki pale pale. Serikali kama hicho ni kiwanda mfanyakazi wao yule walimsaidia nini. Aniambie Mhe. Waziri atakapokuja kujibu hoja.

Mhe. Naibu Spika, jengine serikali yetu inakuwa na *pantry statement*, Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo anatuambia kuchimba mawe ni kiwanda na kinaongeza mapato, ukienda Waziri Fatma Fereji anatuambia ni kuharibu mazingira.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo mimi nadhani serikali isitufanyie utani bwana katika mambo, ikiwa hawana viwanda watufufulie tulivyovianzisha sisi waasisi. Sisi tulianzisha viwanda vingi hapa, katika awamu ya pili na ya kwanza. Tulikuwa na kiwanda cha buti pale kikitengeneza safari buti za uhakika, tukitengeneza viatu vya jombo na tukitengeneza mambo kadhaa wa kadhaa. Ikiwa hii serikali ya awamu ya Saba haina uwezo wa kujenga viwanda basi vifufueni vile vya zamani. Mhe. Naibu Spika, hata kiwanda cha sukari kipo pale mnashindwa kufufua. Mimi nadhani katika hili Mhe. Naibu Spika, wasituletee mambo hayo, wavi-*invest* vyanzo.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine lililowashinda hawa na linalofanya Zanzibar ikose mapato ni kwa sababu siasa za Zanzibar zinatumikia uchumi. Juzi alieleza pale Mhe. Hija Hassan kwamba uchumi ni haramu kutumikia siasa, uchumi ni haramu kutumikia siasa! Siku zote siasa itumikie uchumi.

Leo hii Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa Waziri alivyotuambia katika kitabu chake cha bajeti, kwamba kwa nchi kama yetu hata ruzuku na misaada kutoka nje ni vyanzo vya mapato. Sasa sisi ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mhe. Raza juzi alionesha jinsi wenzetu wa Tanganyika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanavyochukua misaada kwa jina la Tanzania, wanavyopata mikopo kwa jina la Tanzania, wanavyopata ruzuku kwa jina la Tanzania na sisi tuliopo hapa tudai asilimia yetu mule ndani. Mbona hakutuwekea Waziri hapa akatuambia kwamba hii ni

ruzuku na mikopo iliyotokana na Jamhuri ya Muungano ni katika sehemu ya pesa zetu, kwa nini.

Mhe. Naibu Spika, hebu tuangalie kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nishati na madini ni sehemu ya mambo ya Muungano. Wenzetu wameanza kuchimba *tanzanite* miaka kadhaa, wameanza kuchimba dhahabu kule miaka kadhaa. Mbona Mhe. Waziri katika kitabu chake hiki hatujaona kwamba tumefaidika na *tanzanite* na dhahabu na sehemu ya pesa zetu zikarudi hapa. Kwa hivyo, mu-*exhorts* haya mambo.

Mhe. Naibu Spika, ametuambia katika kitabu chake Mhe. Waziri kwamba kuna sekta hii ya mahoteli na utalii. Nchi yoyote uchumi wake unategemea mahoteli basi inaendesha mambo yake kwa kujaribu na kubahatisha, uchumi wa kutegemea utalii ni wa kujaribu na kubahatisha Mhe. Naibu Spika. Nasema hili kwa sababu zifuatazo. Mtoa mada juzi alisema ikiwa nchi ni *stable* basi uchumi unakua, lakini utalii nchi ukibadilika kidogo upepo basi unakuta utalii haupo, pato la nchi halipatikani. Kwa hivyo, uchumi wa kutegemea utalii ni sawa sawa ukachukua *spirit* ukaweka kwenye *glass* ya wazi ukipita upepo unakuta *glass* imemaliza na *spirit* yote imetoka. Kwa hivyo, hili la utalii katika nchi hii ni tatizo.

Mhe. Naibu Spika, jengine kuhusu sekta ya utalii kuna ghilba kubwa inayofanywa kwenye sekta hii ya Utalii. Kwanza kwenye sekta hii ya utalii kuna hawa wanaotumia *tourism system*, wale wanaikosesha mapato nchi kwa kuteremsha *rate* ya nyumba. Utamkuta mtalii yuko kule na *rate* ya chumba ni dola 1800, lakini akienda Kiwengwa ile kampuni iliyomleta inasema ni dola 300, hapa tumezikosa pesa. Kwa hivyo, serikali hapa iwe makini katika hili, hawa wenye *tourism*, kwa sababu serikali inakosa mapato.

Mhe. Naibu Spika, jengine katika sekta hii ya utalii ambacho tunakikosa, kuna ghilba. Kwa mfano Mhe. Naibu Spika, wanabadilisha majina ya kampuni na kubadilisha *management*, halafu wanapata kuondolewa ushuru, huu ni wizi wanapata serikali. Kwa hivyo, Mhe. Waziri wa Fedha ni lazima uwe makini. Kuna mahoteli kama vile Venta Club, Blue ni hoteli nyingi sana. Kwa hivyo, Mhe. Waziri tunakuomba sana katika hili kwamba uwe makini na mapato yetu, kwa sababu hizo ndio zinazosaidia maendeleo katika hili suala zima la *tourism*, katika hili ni lazima bei za chumba ziwe za uhakika. Sio watu wanawachukua watalii wale wanawalipa kwa dola 1800, wao wanakuja kulipa kwa dola hizi chache.

Mhe. Naibu Spika, kwa haraka haraka naona niende kwenye sekta ya usafiri na usafirishaji. Mhe. Naibu Spika,

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe nakuomba utakuja kumalizia dakika zako jioni. Waheshimiwa Wajumbe, naomba nitoe taarifa kwamba wachangiaji wamekuwa wengi kidogo na kesho tunategemea kumuita Waziri ili kufanya majumuisho na kupitisha bajeti yetu. Sasa asubuhi nilikuwa na wachangiaji 20 nilipoingia hapa, lakini wameongezeka watano, na huyu anayechangia sasa hivi atamaliza jioni ni mtu wa 10. Kwa hivyo, watabakia Wajumbe 15, nategemea wachangiaji 10 tumalize jioni ili watano kesho tukijaaliwa tutapunguza maswali ili waweze kuingia.

Kwa hivyo, natangaza kabisa watakaotangulia watano wa mwanzo jioni ili mujihimu kuja mapema.

1. Mhe. Abdalla Mohamed Ali
2. Mhe. Omar Ali Shehe
3. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa
4. Mhe. Rufai Said Rufai
5. Mhe. Nassor Salim Ali na wengine wataendelea baadae.

Waheshimiwa Wajumbe, baada ya maelezo hayo naakhirisha kikao chetu hadi saa 11:00 jioni leo.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(*Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia*)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tunaendelea na kumalizia Mhe. Saleh Nassor Juma kwa kumpa dakika 10 na baadaye katika orodha yangu waliotangulia ni Mhe. Abdalla Moh'd Ali.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana pale nilikuwa nataka kumalizia kuhusu jinsi sekta hii ya mahoteli ilivyokuwa uchumi wake ni *monopoly* na nilitoa mifano na niliwahi kutaja *Venta Club* hii ambayo iko Kiwengwa ni tatizo Mhe. Naibu Spika.

Kwa kweli ni tatizo kwa sababu uwekezaji wowote lazima unufaishe serikali pamoja na wananchi, lakini inaonekana uwekezaji wa utalii ni tatizo, kwa sababu hii *Venta Club* imefilisika na hii hoteli imekuwa gofu na hivi sasa *assets* zake zinaanza kuchukuliwa na wala serikali pale haipeleki ulinzi wa kulinda zile *assets* na hilo ni tatizo.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa ina jumla ya wafanyakazi 43, ambao miongoni mwao wanne wameshakufa, yaani wale waliokuwa wakipeleka huduma za vyakula pale na wanne wamefariki na wala haki zao hawajapata wanadai *pound* 410,000 wanaidai hiyo *Venta Club* na bado hawajalipwa.

Aidha serikali inadai *land lease* ya *pound* 170,000 na mpaka hivi sasa fedha hizo serikalini hazijafika. Vile vile kuna mishahara ya wafanyakazi *pound* 80,000.

Kutokana na hali hii mimi nashauri serikali katika hili Mhe. Naibu spika, fedha hizi ni nyingi basi huyu bwana kama amefilisika wa *Venta Club*, mali zake ziuzwe, ili hawa masikini wa Mungu waweze kujiendeleza kwa kulipwa madeni yao na hili pato la serikali liweze kuingia katika Mfuko wa Serikali, kwa sababu *pound* 170,000 na serikali ingefanya mambo mengi sana.

Nikiondoka hapo sasa niende moja kwa moja kwenye Sekta ya Usafiri na Usafirishaji. Mhe. Naibu Spika, tunaambiwa sekta hii ya usafiri na usafirishaji imefanikiwa sana na imekua kwa asilimia 19.7 kwa mwaka huu wa 2012 kutoka asilimia 8.6 mwaka 2011. Hii inaonekana kwenye kitabu cha kwanza kuhusu Mpango wa Maendeleo ya Zanzibar.

Sasa katika suala hili la ukuaji wa sekta ya usafiri nianze na usafiri wa baharini. Mhe. Naibu Spika, katika hili kwanza naomba niipongeze serikali kwa ku-*facilitate* wawekezaji katika sekta hii ya bahari. Kwa hivyo, nashukuru sana katika hili kwamba *private sectors* wamewekeza kwenye bahari na usafiri unapatikana.

Vile vile kwanza nataka ni-*declare my interest* mimi sina ajira kwa mfanyabiashara Said Salim Bakhressa na pia sina mtoto wangu kule ambaye anafanya kazi wala sina kipato chochote kile ninachopata, isipokuwa ninachonufaika ni huduma ya Kampuni yake hii ya *Azam Marine*.

Kwa kweli kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Wawi napenda nichukue fursa hii kumpongeza sana mfanyabiashara Said Salim Bakhressa, yaani ametupatia mambo mazuri katika suala zima la usafiri wa baharini. Kwa mfano, juzi nimetembelea pale Malindi kwenye ndani ya vyombo vidogo vidogo, amefanya kitu kikubwa sana ambacho huku katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara nimetembea sana sijawahi kukiona. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kwa niaba ya wapiga kura wangu wa Jimbo la Wawi napenda sana nimpongeze sana Said Salim Bakhressa kwa kujitahidi ku-*facilitate* katika sekta nzima ya utalii na kuna msemo wa Kiswahili Mhe. Naibu Spika, unaosema '*Mcheza kwao hutunzwa'*. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nasikitishwa sana na serikali yangu hii inayoongozwa na Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein kaka yangu na kwamba huyu kijana huyu Said Salim Bakhressa hanufaiki yeye tu katika uwekezaji wake na zaidi tunanufaika sisi. Kwa mfano, amejenga *VIP moles* na *departure* na *arrival* wote wapo katika bandari na wala sijaiona katika sehemu nyingi za hapa karibu. *(Makofi)*

Lakini mtu mwenyewe pamoja na Kampuni yake kubwa anataka apewe sehemu ajenge ofisi anacho kibanda kidogo pale ukiingilia mlango mkubwa katika bandari na ile haimtoshi. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli kutokana na kampuni yake yule jamaa anahitaji pahala pazuri sana, kwa ajili ya kuweza kufanya biashara zake, kwa sababu kampuni yake ni kubwa.

Sasa mpaka leo hii yule jamaa bado hajapatiwa ile nafasi nya yeye yupo tayari hapa kwenye *main gate* hapa na juzi moja aliwahi kuniambia mimi binafsi kwamba ikiwa watanipatia sehemu ya *main gate* kuna ghala pale, kwa ajili ya kujenga na halafu hilo ghala alijenge ghala jengo la kisasa kwa pale nyuma, lakini hadi leo hii serikali kwa masikitiko makubwa haijampatia. Mhe. Naibu Spika, naomba kuishauri serikali kwa heshima kubwa na taadhima ya hali ya juu wakaweza kumpatia nafasi huyu kusudi aendelee kutupa huduma inayohitajika tena ya kiwango kikubwa zaidi.

Aidha jambo jengine linalovunja moyo kwa huyu jamaa ni kwamba anataka kutoa huduma Pemba kama anayoitoa Dar-es-Salaam au Unguja, pia ameomba apatiwe pale Mkoani ama Wete au Wesha kwa ajili ya kujenga, lakini mpaka hivi sasa serikali bado haijampatia. Kwa hivyo, nadhani watu wa serikali hili mulione, kwa sababu na wale wa Pemba nao wanataka wapate hii huduma hususan usafiri kutoka Pemba kwenda Tanga ni tatizo.

Kutokana na hali hiyo, basi ni vyema akapewa Said Salim Bakhressa akajenga mambo yake mazuri pale, basi usafiri wa Wete - Tanga ungekuwepo na suala hili naiomba sana serikali kupitia kwako Mhe. Naibu Spika ijitahidi sana katika hili.

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba niende katika usafiri wa nchi kavu. Mhe. Naibu Spika, usafiri wa nchi kavu nao ni mzuri na unaingiza pato kwa sababu hivi sasa katika Mji wa Chake Chake ambapo mimi ndiko ninakoishi, basi pale kwa kutwa moja zinaingia gari zaidi ya 200 kisiwa kama kile na kila gari ikifanya *parking* inalipa shilingi 500 mbali *road license* na bima, kwa hivyo pato linaingia sana na kodi inakusanywa sana. Tatizo ni kwamba kodi haiwafikii walengwa pale Chake Chake nzima Mhe. Naibu Spika hakuna kapa, yaani gari zinakaa tu pembezoni hivi mara ukwaruzwe na gari wakati madereva wanalipa kodi madereva.

Mhe. Naibu Spika, nadhani kodi wanakusanya kwa madereva lakini hamuwajengei kwa mfano Mji wa Chake Chake kwa nini hauna *stand*, ili waendelee kutupa huduma nzuri hawa madereva na wafanyabiashara ya magari.

Sasa naomba niende kwenye matumizi.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, bado dakika tatu.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, ahsante. Kwa kweli mimi naona kama kuna jambo la uangalifu serikalini basi ni hii *financial expenditure*. Mhe. Naibu Spika, mimi naona kutumia fedha nyingi za walipa kodi wa nchi hii kwa mambo yasiyokuwa na umuhimu sana ni tatizo kubwa sana. Kwa mfano, hivi sasa ukiangalia humu serikali hao Wakurugenzi waliomo ni hatari.

Kutokana na hali hiyo, mimi naona tupunguze kidogo haya mambo na wala sitaki niseme ipunguzwe serikali, lakini kila unapokwenda ni Mkurugenzi nadhani ingefupishwa kidogo haya mambo, kusudi hii *financial expenditure* ikafanyika vizuri.

Sasa naomba niende kwenye suala zima la sherehe. Mhe. Naibu Spika, juzi nilipata taarifa kwamba mara hii tunapata kutumia shilingi bilioni moja kwa ajili ya sherehe hizi za kuadhimisha Mapinduzi matukufu ya Zanzibar ya mwaka 1964. Kwa kweli mimi nayapenda sana mapinduzi tokea zamani na hadi sasa na wale waliokuwa hawapendi basi tuliwalazimisha wapende na wanayapenda. Lakini kwa kweli kutumia fedha hizi shilingi bilioni moja kwa ajili ya sherehe si matumizi mazuri kwa fedha za walipa kodi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, mapendekezo yangu katika hili sherehe hizi tuzifanye kwa miaka minne kimkoa na mwaka mmoja kitaifa ziwe kubwa, lakini tukiendekeza na mimi nakumbuka miaka ya nyuma tulikuwa tukiadhimisha sherehe za Muungano kila baada ya miaka mitano ndio inakuwa kubwa na hizi nyengine tunazifanya sherehe kwa Wakuu wa Mikoa pamoja na watu wake, na kwa nini tusiende huko, kwa sababu *mtu haungi kimo kwa jiti*. *(Makofi)*

Kwa mfano, sisi tunataka kufanya sherehe zote hizo wakati skuli hakuna vikalio, matibabu ni matatizo, kwa nini shilingi bilioni moja tusiitafutie jambo jengine tukaifanyia, kwa sababu Mapinduzi yapo na yataendelea kuwepo na yatadumu milele bila ya kupoteza fedha zote hizo. Kwa kweli katika suala hili wala tusiwe na wasi wasi na mapinduzi Mhe. Naibu Spika, serikali isiwe na

wasi wasi mapinduzi yalikuwepo, yapo na yataendelea kuwepo, lakini kutumia shilingi bilioni nzima katika mambo haya ni matatizo makubwa sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa heshima kubwa mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Wawi bajeti hii ni nzuri na katika kupitisha vifungu tutaendelea kuhoji na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akipenda itapita. Mhe. Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Abdalla Moh'd Ali: Mhe. Naibu Spika, na mimi nashukuru alaasiri hii kwa kunipatia fursa ya kusema machache katika Mpango huu wa Mapato na Matumizi kwa mwaka 2013/2014.

Mhe. Naibu Spika, imekuwa ni kawaida yetu kwamba kila mwaka na katika kipindi kama hichi huwa tunapokea mgeni kama huyu na kwa sisi Waswahili huwa mara nyingi tunao msemo wetu tunasema kwamba '*Mgeni awia mwenyeji apone'*. Lakini kwa mara hii imani yangu ni fupi sana kwamba kuja kwa mgeni huyu basi mwenyeji atadhoofika hatapona. Sasa kwa nini nasema hivyo? Nasema hivyo kwa sababu nimeangalia sheria nyingi zilizotarajiwa kurekebishwa na serikali zinamgusa mwananchi na kwa maana hiyo sina imani kwamba mgeni aliyekuja mara hii ataleta shufaa.

Vile vile katika hilo pia niseme kwamba kuna mshairi mmoja aliwasifia Watumbatu na Wapemba kwamba na wao katika kumkaribisha mgeni wanao ukarimu wao na yeye alisema kwamba 'Ndio kawaida yetu sisi Wapemba na Watumbatu japo kuwa hatuna kitu, lakini basi chai huwa tunampelekea', mimi nitampelekea chai kidogo huyu mgeni wetu.

Mhe. Naibu Spika, ni dhahiri kwamba mwaka jana tulipokea matumizi na mapato wakati tulipokadiria hapa, kusema kweli tumeshaona jinsi gani yalivyokusanywa na yalivyotumika. Lakini mimi nataka nitoe fikra zangu kidogo jinsi gani mwaka huu mapato tuliyokadiria kuyakusanya na kuyatumia tutayatumia vipi.

Mhe. Naibu Spika, kuna mwaka nilibahatika kutembelea sehemu moja inaitwa Taj Mahal, nafikiri ni sehemu moja ambayo kila mtu anaijua kwamba ni ya kihistoria na historia yake ni kubwa na ni moja miongoni mwa maajabu ya dunia.

Wakati nilipofika pale yule mtembezaji alinipa historia ya sehemu ile na aliniambia kwamba aliyejenga sehemu ile alijenga kwa madhumuni ya kumtunukia mke wake, ambaye baada ya kujifungua mtoto wa kumi au wa

nane alifariki. Sasa mwananchi huyu yeye alikuwa ni mfalme na alitumia fedha ya walipa kodi.

Baada ya maelezo yale mimi nilimuuliza bwana wewe umeshanieleza na nimeshafahamu, lakini naomba nikuulize swali wakati ilipokuwa ikijengwa nyumba hii huyu bwana alitumia fedha za wananchi na wakati ule nchi hii ilikuwa ni masikini sana. Sasa wewe kiongozi huyu umemuona vipi ni shujaa au unamuona ni mfisadi, kwa sababu hivi sasa sehemu hii ndio njia kuu ya kupatia mapato ya nchi yenu. Kwa kweli alichoniambia ni kwamba unajua *always the rich are becoming richer and the poor are becoming poorer*, basi nilifahamu.

Mhe. Naibu Spika, mwaka jana au mwaka 2011/2012 serikali ilinyanyua vipato vya wananchi au vipato vya watenda kazi kwa kuongeza mishahara yao. Sasa kwa utafiti wangu mdogo nilioufanya nimegundua kwamba waliofaidika ni hao matajiri na wale masikini wakazidi kuwa masikini, kwa sababu viwango vilivyotolewa havikuwasaidia walioko chini, isipokuwa viliwasaidia zaidi walioko juu na wanaopata viwango vikubwa vya mishahara.

Sasa mwaka huu tulivyosomewa mapato haya tumeambiwa kutakuwa na kasma ya karibu bilioni 17, ambazo hizi zimekusudiwa kuwalipa wafanyakazi wapya na labda kuwaongezea mishahara wale ambao tayari wapo kazini. Mhe. Naibu Spika, kwa msemo ule alioniambia yule bwana kule India basi nina wasi wasi kwamba watakaofaidika ni wale wale walioko juu na hawa wa chini watahasirika zaidi.

Kwa hivyo, mimi ninachokiomba serikali iwe makini katika hili wanyonge ni wengi na watenda kazi wetu tunawajua jinsi wanavyohangaika, kwa maana hiyo kwa mara hii kwa vile bajeti zetu huwa tunaweka *ceiling* na mishahara inawekewa *bar*. Kutokana na hali hiyo, basi ni vyema iangalie wale ambao wameshafikia hatua ya juu kabisa, basi wawekewe *ceiling* na *bar* na mara hii tuangalie zaidi wale wenye kima cha chini na wao wajue kuwa wamo katika nchi hii kufaidi yale matunda tunayosema ya mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, hapa tumeelezwa tena kwamba serikali yetu au kwa hivi sasa tunakwenda katika mfumo wa bajeti *basic program*. Kwa mwaka uliopita mwaka 2012/2013 serikali ilianza majaribio ya wizara karibu tano. Mwaka huu vile vile inatuambia kwamba inataka tena au itaendelea nao mpango huu.

Lakini naomba nimuulize Mhe. Waziri je, katika *program* zilizopita matokeo yake ni nini ya majaribio ya hizi wizara tano, na jee tumepanga kipi tukiendeleze katika hayo matokeo ya *program* ya wizara hizo ambazo

zilikuwa katika majaribio na labda serikali imetenga kiasi gani katika hilo. Kwa nini nasema hivyo?

Mhe. Naibu Spika, hapa tumeweka vipaumbele na tumesema vipaumbele vyetu mara hii ni maji, elimu, kilimo na ajira. Sasa ukiangalia katika kilimo utakuta ni kutoa tu huingizi chengine na ukiangalia katika elimu unakuta ni kusomesha tu huingizi chengine.

Kwa hivyo, sisi tatizo letu kubwa hivi sasa ni ajira na tutazipata vipi, ikiwa hatukuwa na *program* ambayo imeanzia nyuma na kutaka kuendeleza vijana wakitaka kuwapatia ajira vijana na wala sitaki niseme mengi lakini tukija kwenye sekta za wizara moja moja nafikiri kwenye sekta ambayo imesahauliwa tutakuja kuiona ni sekta ya utalii, ambayo kwa mawazo yangu mimi ni sekta ambayo ni tegemezi kwa hivi sasa lakini sioni katika *programs* zetu kwamba kuna endelezo fulani linakusudiwa katika sekta hii ya utalii, ili kuboresha zaidi pamoja na kuwapatia wananchi wetu ajira.

Nikiendelea na mchango wangu sasa niende kidogo kwenye suala la hatua za kuimarisha mapato. Mhe. Naibu Spika, hapa serikali imependekeza hatua tofauti na kama nilivyosema mwanzo kwamba hatua hizi zote au nyingi ya hatua hizi zinamgusa mwananchi.

Kwanza serikali inapendekeza marekebisho ya Sheria ya Leseni ya Njia, yaani barabara ni jambo zuri na najua kwa yule ambaye atakuwa anatumia barabara kwa wingi kwa kuongeza asilimia au senti 35 katika mafuta atakuwa yeye analipa zaidi.

Mhe. Naibu Spika, nishati hii haitumiwi na walio na barabara tu, kama tunavyojua kuna watu kwamba nchi yetu umeme hauna uhakika, basi kuna watu wanaotumia *pump* zao za maji kwa ajili ya kupandisha maji kwa ajili ya kulimia mboga mboga. Lakini kubwa zaidi ni kwamba kuna watu ambao wanatumia nishati hii kwa sekta ya baharini ambao ni wengi sana.

Sasa je, kuongeza asilimia 35 kwa ajili ya kulipia malipo ya barabara na huyu ambaye anatumia kwa kuendesha shughuli zake baharini yeye si atakuwa anafanyiwa udhalilishaji au atakuwa anachukuliwa fedha zake bure.

Kwa hivyo, ninamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Naibu Spika akafanya marekebisho mengine, wale wenye maboti ambao wanatafuta samaki baharini watalalamika na mwisho wake wataongeza bei kwa sababu ni jambo la kila siku. Kutokana na hali hiyo, hebu tuangalie je, tupandishe senti 35 hizi kweli hakutomuathiri huyu ambaye yeye hatumii barabara.

Jambo jengine Mhe. Naibu Spika, katika mapendekezo ya serikali kuingiza mafuta kwa njia ambayo labda tutakuwa na *single importer*. Kwa kweli naomba tusisahau kwamba sera tuliyonayo hivi sasa ni *Trade Liberalization* na wala tusirudi nyuma tena, na kama tunakusudia kwenda mbele basi twende mbele tu huko, lakini tukija na sera hii itakuwa hizo sera nyengine tuzifute kisheria. Kwa kweli hivi sasa haiwezekani tena turuhusu mtu mmoja amo-*monopoly* biashara ya aina moja.

Sasa hii kwa upande mwengine inaleta sura nyengine kwa sababu ni hapa tu ambapo labda wengine wanaweza kutumia fursa hii kwa kuweka zile kamisheni zao kwamba nitakuruhusu wewe tu uwe peke yako, lakini unajua tena. Kwa hivyo, ili yasitokee mimi nasema kwamba tuendelee na sera yetu ile ile ya kusema kwamba sisi tumeweka biashara huru. Suala la kumkaribisha mtu mmoja au kumuweka mtu mmoja kwamba yeye alete mafuta tunayaona. Leo tunapata tabu sana kwa Shirika la Umeme kwa sababu wako peke yao, ukienda nchi za wenzetu kila nyumba unaweza kukutia nguzo nne, tano, sita wote wale wanamsubiri mteja mmoja.

Lakini sisi sote tumelala *ZECO* matokeo yake tunayaona. Sasa hili lisiturudishe tena nyuma tuendelee mbele tuwaruhusu watu walete mafuta, vyombo vya dola vipo na kila siku katika ajira zinazotolewa kwa wingi ni ajira za vikosi. Kwa maana hiyo sasa hivi vikosi tuvitumie kwa sekta kama hizi, kama tuna wasiwasi wa kwamba suala hili litakuwa katika njia isiyo ya uhali ya magendo basi askari tusiendelee tena kuwaajiri.

Mhe. Naibu Spika, pia kuna sheria ambayo inatarajiwa kufanyiwa marekebisho sheria hii tunaiita *PTS* kama ilivyokwishasema Serikali kwamba kwa muda mrefu ilikuwa haitozi kodi hii kwa kuwa walikuwa wanawalea hawa wafanyabiashara wadogo wadogo. Kwa nini sasa wamesha *mature* hawa wafanyabiashara wadogo wadogo kiasi kwamba tuwapatie miguu yao, hebu turudi nyuma tuangalie tukiwawekea kodi hii watakufa au watakuja juu zaidi hapa.

Sekta hii Mhe. Naibu Spika, hivi sasa ndiyo inayo ajira kubwa ya wananchi, wengine wanajishughulisha na sekta hii. Sasa tuwape motisha Serikali hapa imekusudia au imekalia kukusanya milioni 400 nina imani kwamba iko njia nyengine ya kuzitafuta pesa hizi, lakini leo kwamba tutawaendea watu wadogo wadogo tuwaambie toeni, hii ni kuwaua.

Sasa Mhe. Naibu Spika, mimi naiomba Serikali hili iliangalie. Kwa vile kama nilivyokwisha sema mwanzo kwamba wao nia yao ni kuwalea na kuwaendeleza basi iendelee kuwalea hivyo hivyo na kuendeleza. Tukiendelea

kuwatoza kodi itakuwa ni mzigo kwetu. Naomba hii itafutiwe njia nyengine mapato haya ya milioni 400 zilizokisiwa basi zitafutiwe sehemu nyengine.

Mhe. Naibu Spika, naomba nizungumzie ambalo mimi nafikiria litakuwa ni suala la mwisho. Mwaka 2012/2013 dunia ilianza kuhama kutoka kijiji cha Teknohama kinachoitwa *Analogy* na kuingia katika kijiji cha *Digital*.

Kwa bahati tulieleza kidogo tu kwamba na sisi Zanzibar kama ni nchi tunataka kuhama kutoka kijiji hicho na kuhamia kijiji chengine hicho cha *Digital*, niliona mipangilio mingi na matayarisho mengi lakini jee, hebu serikali ituambie kuhama kwetu huku tayari tumeshafikia hatua tuliyoikusudia na labda katika kuhama kwetu huku tumegharamika kiasi gani hata kufikia hatua hiyo. Kwa kweli sijaona chochote katika mpango wa mwaka huu na mwaka uliopita, mpango huu haumo katika matumizi na mapato ya serikali.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, ahsante sana na sasa nafasi tunampa Mhe. Omar Ali Shehe baadaye Mhe. Nassor Salim Ali na ajitayarishe Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujaalia na kutuwezesha jioni hii tukaweza kuhudhuria katika kikao hichi. Naomba nianze kwa kumpongeza Mhe. Waziri kutokana na namna anavyotekeleza majukumu yake ya uwaziri na anavyosimamia wizara hii muhimu sana kwa uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, bajeti hii imekuja wakati muafaka, yaani imekuja wakati ambapo tupo katikati ya kipindi cha uongozi wa awamu hii ya uongozi wa Rais Dkt. Ali Mohammed Shein. Sasa unapofanya jambo lolote lile ukafikia katikati ya kipindi basi ni kipindi kizuri cha kujitathmini namna ulivyoanza na utakavyomaliza. Kwa hiyo, bajeti hii si bajeti ya kawaida, isipokuwa ni bajeti ya kujitathmini kwa uongozi wetu huu tulionao katika kipindi tutakachomalizia mwaka 2015.

Mhe. Naibu Spika, bajeti ina maana, na maana kama tulivyoambiwa na wataalamu ni mpango wa serikali wa kukusanya na kutumia. Lakini hiyo ni tafsiri yetu sasa kwa wengine duniani au nchi nyengine zilizoendelea bajeti inachukuliwa katika uzito wa uhai wa maisha ya wananchi hasa wa kawaida na hata wale matajiri nao huiangalia bajeti katika uzito wao.

Katika kipindi hichi cha bajeti, wananchi wote katika nchi macho yao na masikio yao huyaelekeza katika Mabunge yao, kusikiliza kila mmoja atakavyoguswa na bajeti ile. Tofauti sana na kwetu. Kwetu watu wamepoteza *interest* ya kufuatilia, kwa sababu ya ile dhana kwamba bajeti ni mpango tu wa serikali wa kukusanya na kutumia. Serikali vipi itakusanya yaani itawakamua wananchi na vipi serikali itatumia kwa ajili ya kujiendeshea serikali. Hiyo ndiyo dhana ambayo sisi tunayo hapa kwetu na ndiyo iliyowapelekea wananchi wengi wakakosa hamu ya kusikiliza. Hata wakisikiliza hawana kitu ambacho wao wanadhani kinawagusa moja kwa moja kama wananchi wa kawaida.

Katika nchi nyengine na ambazo na sisi tunapaswa tufanye. Katika kipindi hichi cha bajeti ni vyema tukaiangalia bajeti ni vipi imewagusa wafanyakazi katika sekta ya Umma. Vile vile ni vipi bajeti imewagusa wafanyakazi katika sekta binafsi. Hichi ndicho kipindi chao ama cha kuvuna au kipindi chao cha hasara.

Mhe. Naibu Spika, bajeti inatakiwa iwaguse wakulima kwa sababu nchi yetu asilimia kubwa sana hasa vijijini ni wakulima, wananchi watarajie nini katika bajeti hii. Vipi mwananchi wa kawaida aliyekuwepo Matemwe, Nungwi, Chakechake, Vitongoji na Micheweni, imemgusa bajeti hii.

Mhe. Naibu Spika, nchi yetu imezungukwa na bahari, kwa maana wananchi wengi sana wanajishughulisha na shughuli za uvuvi. Bajeti nayo ilitakiwa itoe jibu juu ya matatizo yanayowapata wavuvi wetu wadogo wadogo tulionao katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, hasa katika miji na vijiji watu katika shughuli zao za maisha kama biashara ndogo ndogo, Zanzibar ni biashara na sehemu kubwa ya wananchi wa Zanzibar wanategemea biashara kubwa na hasa ndogo ndogo. Namna gani bajeti hii imegusa, imetaja au imejibu matatizo waliyonayo wafanyabiashara wetu wadogo wadogo, wafanyabiashara waliopo pale Darajani, wafanyabiashara waliopo Saateni na sehemu nyengine.

Mhe. Naibu Spika, kila kipindi cha bajeti ni msimu wa vijana kuangalia namna ambavyo wameguswa katika suala zima la ajira. Tunapaswa tuangalie bajeti hii imetaja au imejibu kiasi gani suala zito juu ya matatizo ya ajira yanayowakumba maelfu ya vijana wetu wanaomaliza maskuli kila mwaka. Sivutiki sana Mhe. Naibu Spika, mimi binafsi kwa kweli sivutiki sana na ile hoja ya serikali kusimama mbele pale na kusema kwamba tumetenga ajira kiasi fulani katika serikali.

Mimi binafsi naamini na tulishasema mambo haya kwamba sekta ya umma haipaswi kujigambia suala zima la kuajiri kila mwaka. Hapana. Wala si sifa kwa serikali kuja mbele hapa kila mwaka kusema kwamba tunatoa, hiyo sio serikali iliyokuwa makini. Serikali makini hutengeneza ajira hasa katika sekta binafsi na sio katika sekta ya umma.

Juzi katika kuwasilisha ripoti mimi binafsi nilisimama mbele nikatoa mfano hai wa Shamba la Kilombero, wafanyakazi tisa wanaotumia trekta moja. Huo ni mfano mmoja kati ya mifano mingi tuliyonayo katika sekta ya umma. Sekta ya umma ina wafanyakazi waliokuwa hawana kazi. Ni wajibu wa serikali kuandaa mazingira ya kuandaa ajira hasa katika sekta ya binafsi.

Mhe. Naibu Spika, tunapozungumza mambo haya tunategemea bajeti ya nchi itoe majibu sahihi juu ya maeneo ambayo yanaweza yakawagusa wananchi wa kawaida ambao ndio wale walipa kodi, hii bajeti ndio hasa inayowahusu.

Mhe. Naibu Spika, tuangalie sura ya bajeti yetu. Tunapoangalia sura ya bajeti kwanza tuangalie suala zima la mapato ya ndani. Kwa sababu ukusanyaji wa mapato ya ndani ndio msingi mkubwa wa bajeti ya serikali. Makisio ya mwaka huu yanaonesha kwamba makusanyo ya kodi za ndani yataongezeka, kutoka 294 bilioni hadi 324 bilioni ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 10. Mapato mengineyo yanaonesha kushuka hii *trend* ya kuongezeka kwa mapato ya ndani ni *trend* nzuri. Unaposema kwamba kila mwaka serikali inaongeza wigo wa makusanyo ya kodi, hiyo tunasema ni *trend* nzuri, lakini iwe na uhalisia isiwe ni mambo ya kudanganya danganya.

Katika makusanyo ya nje *trend* kila ikiwa ni kupungua mwaka hadi mwaka hiyo inakuwa ni *trend* nzuri, ni *trend* ambayo ni *positive*. Hali inaonesha kwamba makisio ya ukusanyaji wa ndani inaongezeka kwa asilimia 10. Lakini vile vile ukusanyaji wa mapato ya nje au upatikanaji wa mapato ya nje inapungua kutoka 354 hadi 324, hiyo ni *trend* nzuri. Kwa sababu nchi kupiga hatua katika kuondokana na utegemezi, lakini uhalisia kwa sababu tumesema kwamba tunatoka kwenye 294 hadi kwenye 324 uhalisia ukoje?

Katika makisio utekelezaji wa miezi tisa kwa bejeti iliyopita, imeonesha kwamba ZRB ilipanga kukushanya 115, lakini kwa miezi ile tisa ilithubutu kukusanya bilioni 100 tu ambayo ni sawa na 87%. TRA wao walisema walipanga kukusanya 80 wakapata 79, ikiwa ni sawa sawa na 99. Lakini mapato yasiyokuwa na kodi yalipangwa kuwa ni 12.84 walifanikiwa kupata bilioni 8.84, sawa na asilimia 69. Maana yake nini?

Maana yake ni kwamba makisio yalipangwa kukusanywa kwa miezi tisa katika bajeti ya mwaka jana hayakuweza kufikiwa. Naamini kama *trend* ni hii

na ni lazima iwe hivi, naamini kwamba kwa miezi 12 nayo haiwezi kufikiwa. Kwa hiyo ni kusema kuwa uwezo wetu ukichukua kigezo cha bajeti ya mwaka jana ni kusema kuwa uwezo wetu ni kukusanya tungejikisia yale yale makisio tuliyoyafanya mwaka jana. Tusingelipaswa kuonesha makisio makubwa wakati serikali haina uwezo. Maana wakati mwengine si kuandika *figure* tu, wakati mwengine ni lazima ufike pahala ujenge hoja na uoneshe uhalisia. Ikiwa mwaka jana miezi tisa hatukuweza kufikia na naamini miezi 12 yaani kwa mwaka hatuwezi kufikia. Kwa hivyo nadhani tulikuwa tushone nguo kwa mujibu wa kitambaa chetu tulichonacho. Hakukuwa na haja wala si ufahari kusema tutakushanya nyingi wakati uwezo huo ni sawa na kujidanganya sisi wenyewe hatuna wa kumdanganya.

Mhe. Naibu Spika, bado tuna tatizo la ukusanyaji wa mapato ya ndani. Ukusanyaji wa mapato ya ndani Mhe. Spika, una matatizo makubwa naomba nimnukuu Mwalimu Nyerere marehemu alisema hivi:-

"Serikali iliyokuwa haikusanyi kodi ni serikali *corrupt*."

Sifa ya serikali *corrupt* ni serikali iliyokuwa haikushanyi kodi. Kwa hivyo ukitaka kujua serikali ni ya aina gani wewe angalia tu namna inavyokusanya kodi ndio tafsiri yake hiyo. Ikiwa serikali haikusanyi kodi tafsiri yake hiyo ni serikali *corrupt* kwa mujibu wa maneno ya Mwalimu Nyerere. Mimi sitaki niamini hivyo lakini ndio Mzee keshasema madamu Mzee keshasema lazima tuamini hivyo. Changamoto kubwa tuliyonayo ni tatizo la ukushanyaji wa kodi katika nchi.

Mhe. Naibu Spika, Zanzibar tuna kodi nyingi sana ambazo hazijakushanywa wala serikali bado haijataka kuzikushanya kodi hizi. Lakini tatizo jengine ni suala kwamba mapato tuliyonayo si halisi Mhe. Naibu Spika. Nilijenga hoja katika Semina moja na leo naomba nirejee. Serikali hii tuliyonayo ilifika pahala katika kutafuta ukusanyaji wa mapato ililazimika serikali kuchukua mapato katika taasisi nyengine ambazo kwa kweli hazikustahiki kuchukuliwa mapato yake.

Mathalan katika kipindi cha miaka minne nyuma kulikuwa kuna mapato ambayo yanaingia moja kwa moja kwenye Serikali za Mitaa. Kwa mujibu wa sheria tulimega majukumu baina ya Serikali Kuu ina majukumu yake na Serikali za Mitaa nazo zina majukumu yake. Leo mapato yale ya Serikali za Mitaa tukayachukua katika Serikali Kuu, kilichotokea kwamba Serikali za Mitaa sasa hivi zime-*paralise*.

Serikali za Mitaa sasa hivi hazitekelezi majukumu yake. Na kwa kuwa sasa hivi serikali ina mpango wa kufanya marekebisho ya sera naamini kwamba

kuna siku mapato yale tuliyoyachukua kule tutalazimika kuyarejesha kule, tutakapofika katika hatua hii nadhani suala hili la Bajeti ya Serikali litaathirika.

Lakini vile vile tuangalie kama sheria ilivyoeleza kwamba kuna kodi ambazo zilitakiwa zibakie katika mambo ya utalii, kodi zile tumezichukua tumezileta serikali kuu. Leo taasisi ambazo tulizipa mamlaka kwa ajili ya kuendesha utalii zimebakia zime- *paralise*

Mhe. Naibu Spika, vile vile kuna kodi ambazo zilitokana na Uwanja wa Ndege, kodi zote zile zilistahiki zibakie pale, tulizichukua wakati ule ambapo ile ilikuwa ni Idara ya Serikali, leo ile sasa ni Mamlaka ambayo inatakiwa iwe na mapato yake. Tutafika pahala kwa kweli na wao watachachamaa na lazima mapato yale tuwape. Ninavyosema hivi ni kwamba mapato tuliyonayo katika Serikali Kuu sio mapato halisi, nina hofu kwamba siku moja tutakapoimarisha taasisi zetu tutalazimika vyanzo hivi vya mapato tuvirejeshe katika taasisi zinazohusika na hapo sasa serikali ndipo itakapotafuta namna ya kujitegemea. Ni wakati sasa serikali itanabahi na itafute njia za kuongeza mapato yake katika serikali.

Mhe. Naibu Spika, changamoto nyengine inayotupata katika suala la ukusanyaji wa mapato ni kwamba bado tuna vyanzo vya mapato havijaguswa katika nchi yetu. Tumekuwa tukilizungumza hili mara kwa mara lakini utekelezaji wake ni mdogo. Kuna suala zima la uvuvi wa Bahari Kuu inakuwa sasa ni hadithi ya kawaida katika Baraza hili. Naamini miaka mitano hii itamaliza na hakuna chochote.

Mhe. Naibu Spika, leo inakuwa ni aibu kubwa kwa serikali kufika pahala wakasema kwamba wameshindwa kusimamia na kudhibiti magendo ya mafuta. Ikiwa serikali waliweza kudhibiti magendo ya karafuu, leo serikali inashindwa kudhibiti magendo ya mafuta yanayouzwa hapo Mikunguni yanauzwa katika vidumu kila mmoja anayaona. Hapana, viongozi mnahusika na hili.

Lazima tufike pahala sasa tuambiane kweli. Viongozi katika hili hatuamini kama hili linawashinda ni mipango tu ya baadhi ya watu wanaopelekewa magendo hawakubaliki katika nchi hii. Na mimi katika hili sikubaliani kabisa na kodi iliyopangwa kutozwa kwa ajili ya *petrol*, haiwezekani. Kwanza kama ikiwa muko *serious* nendeni kazuieni magendo ya mafuta ambayo yanauzwa majumbani mwenu, kwa majirani zenu, nendeni kazuieni. Vyenginevyo kwa kweli hili hatuwezi kukubaliana.

Hatukubali kuwakamua wananchi wanyonge, wanaotoa 500 au 1000 kwa kila siku kuja kuhemea mjini kuja kutafuta kijio leo mkasema muwakamue tu, haiwezekani. Kwanza zuieni magendo ya mafuta ambayo yanauzwa *haadhiri nnaadhiri* katika mitaa yetu.

Mheshimiwa vyanzo vipya vya mapato ambavyo vyenye uchumi mkubwa kama nilivyosema bado hatujavigusa. Lakini Mheshimiwa tukavyozungumza masuala haya kadiri mtakavyokwepa au kadiri tutakavyokwepa mfumo tulionao wa Muungano ni tatizo kubwa sana. Wenzetu katika nchi mbalimbali duniani na hata sisi Zanzibar ilitukumba, tulipounganisha nchi hizi katika kipindi kile cha vita baridi. Hatujuti na hatutojuta kwa sababu Muungano ni kitu kizuri. Lakini lazima sasa tufike pahala tubadilike.

Kwa sababu kipindi kile Muungano ilikuwa ni muungano wa kisiasa wakati ule. Lakini sasa hivi muungano ni uchumi, ni lazima sasa hivi tuuzungumze muungano katika hali hiyo ya uchumi. Hakuna tena muungano wa kisiasa sasa hivi. Naomba sasa hivi tutanabahi. Sasa hivi pamoja na yote yanayokwenda Uingereza katika *European Union*, Waingereza wanakwambia hapana suala la *pound* hapa sitoi pamoja na kutaka kwangu muungano wa Ulaya lakini hapa sitoi.

Kwa hivyo tutanabahi Waheshimiwa tuuzungumze Muungano katika mtindo wa kiuchumi ikiwa una manufaa kiuchumi tuuchukueni au kama kwa vyovyote vile hauna maslahi ya kiuchumi tuukataeni. Hatukatai muungano lakini lazima muungano upewe *benefit* ya kiuchumi kwa upande wetu wa Zanzibar. Tumepata fursa nzuri ni jukumu letu Wawakilishi na wananchi kuona kwamba fursa hii muhimu na adhimu hatuipotezi wakati muafaka utakapofika.

Mhe. Naibu Spika, nikija kwenye matumizi kwa sababu tulisema kwamba bajeti ni mapato na matumizi. Matumizi ya serikali yanaonekana kupanda na narudia kusema kwamba hii sio *trend* nzuri. Serikali zote zile makini hujaribu kupunguza matumizi kila mwaka. Tuangalie Kenya alikuwa na *cabinet* ya mawaziri 48, kapunguza Mawaziri wake hadi sasa hivi ana mawaziri 14 sijui ni asilimia ngapi. Maana yake nini? Maana yake ni katika kujaribu kubana matumizi ya serikali.

Kwa hivyo *trend* ya kuongeza matumizi ya serikali kila mwaka hili ni suala ambalo halikubaliki. Ni lazima tufike pahala tujiulize hili ongezeo la matumizi hasa linatoka pahali gani. Kwa sababu hata juzi tulikaa sisi katika Baraza hili, tukasema kwamba Serikali ni lazima ifikirie katika kubana matumizi na matumizi yasiyokuwa ya lazima. Tukamshauri Mhe. Waziri kwamba lazima afanye *adjustment* katika mwahala mwingi ili wabanebane

matumizi. Leo kuambiwa matumizi ya serikali yanaongezeka lakini ukiangalia mapato, leo tunafika pahala Mhe. Naibu Spika, mapato yanakuwa ni madogo kuliko matumizi ya serikali. Hata katika biashara ya kawaida hiyo haikubaliki. Haiwezekani wewe faida unayoipata ni ndogo lakini kula yako katika duka, halichukui hata wiki duka litakufa.

Kwa hivyo na sisi vile vile tuondokane na *trend* hii. Tufike pahala tuangalie mapato na matumizi liyonayo tuyafanye matumizi yasizidi mapato. Ndiyo mambo yanavyokwenda hivyo.

Mhe. Naibu Spika, tulivyoangalia utekelezaji wa matumizi katika bajeti iliyopita, angalieni sasa. Katika kipindi cha miezi tisa mapato yaliyopangwa kutumika katika matumizi mengineyo yalipindukia kwa 100%. Hii ndio pahala pekee kwamba kuna *seriousness* katika matumizi lakini mwengine mote mapato hayakufikia lengo na sehemu nyengine, lakini katika matuzi tu, hasa matumizi mengineyo yote yalipindukia lengo. Huu sio utaratibu mzuri.

Mhe. Naibu Spika, matumizi ya maendeleo vile vile nayo ni kizungumkuti. Tumekuwa tukijidanganya sisi wenyewe. Serikali inaona ufahari wa kusema mwaka huu imeongeza bajeti ya matumizi ya maendeleo. Lakini sio kweli, kwa sababu kama ukiangalia miradi ya Waheshimiwa utabaini kuwa miradi ya tangu mwaka 2005 mimi naingia katika Baraza hili, ni miradi ipo. Ipo kwa sababu moja tu, kwa sababu ya kuweka *figure* ili ionekana kwamba bajeti ya maendeleo inakuwa ni kubwa. Tangu nilipoingia kwenye Baraza hili ukifanya tathmini mtaikuta miradi hiyo, ningekuwa nina muda ningeliitaja kwamba mradi huu na huu upo tangu mwaka 2005 mpaka leo. Na kila mwaka hauingizi, upo pale kwa sababu sisi tuone kwamba serikali inatenga fedha nyingi kumbe si kweli katika hilo. Serikali inatenga fedha kidogo sana katika miradi ya maendeleo na wakati huo sasa hatuwezi kujenga uchumi katika mtindo wa aina hiyo.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu ya muda wako naomba niseme la mwisho kwamba tatizo letu kubwa tulilonalo ni uchumi. Lazima sasa tufikirie kujenga uchumi miaka hii miwili iliyobakia kama itawezekana. Mimi napendekeza Mhe. Naibu Spika, kwamba serikali iende kutumia rasilimali tulizonazo. Tuna rasilimali, serikali iandae *program* ya kutumia rasilimali tulizonazo. Zanzibar sio masikini, Zanzibar matajiri na kila akili Mhe. Naibu Spika, hudhibitiwa mapato ya ndani. Mapato tunayo, lakini hayo kidogo tuliyonavyo yanavuja, tunatumia fuu tomo, mapato yanavuja. Wala wanaokula mapato hawachukuliwi hatua. Serikali inakuwa kibogoyo katika hili, hili haliwezekani.

Jengine Mhe. Naibu Spika, bado hatujawa na mipango inayotoa vipaumbele. Kuwa na vipaumbele ni jambo muhimu sana katika kujenga uchumi wa nchi. Inaonekana sisi tunadakadaka tu hatuna pahala maalum ambapo tunashika. Tunakwenda na utaratibu wa kujingikiwa tu kitu ambacho si kizuri.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ambalo nataka niliseme, tulisema hapa kwamba serikali ifike pahala kwa kweli tuimarishe sekta binafsi, bila ya kuimarisha sekta binafsi inakuwa siku zote ile PPP sasa inakuwa ni POPOPO hamna chochote kilichomo. Serikali hebu itujie na majibu sahihi ya namna ilivyojipanga katika kuimarisha sekta binafsi. Kwa sababu sekta binafsi ndio mkombozi wa uchumi wa nchi yeyote duniani pamoja na nchi yetu ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, naheshimu muda wako, nakushukuru sana.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi hii ndogo kuweza kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Fedha. Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kukupongeza wewe pamoja na Baraza lako tukufu na Spika wetu kwa maendeleo ya mabadiliko ya Baraza letu katika masuala ya usafi.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli tokea tuanze kwa kikao hichi Baraza letu limekuwa safi na linavutia kwa hivyo naweza kuchukua fursa hii kukupongeza wewe pamoja na Spika, kwa usafi huu ambao upo katika Baraza letu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya pongezi hizo pia nichukue fursa hii kumpongeza na kumshukuru sana Rais wetu wa Zanzibar Dokta Ali Mohammed Shein kwa uongozi wake mahiri katika kutuongoza kuleta maendeleo kwa kufuata ilani ya Chama cha Mapinduzi katika uongozi wake kwa kuutetea muungano wetu ambao Januari 2014 utakuwa umefikia miaka 50.

Mhe. Spika, baada ya hayo nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake katika kuandaa bajeti hii ambayo kwa mafunzo ambayo tumeyapa kule Kiwengwa, kwa kweli sote vichwa vyetu tumeelewa na tumefahamu mikakati ya maendeleo ya serikali yetu ambayo inaongozwa na Dokta Ali Mohammed Shein.

Mhe. Naibu Spika, nije katika masuala ya kipaumbele. Katika Bajeti hii kuna masuala ambayo yamewekwa kipaumbele yakiwemo masuala ya maji, elimu, afya, ajira kwa vijana. Suala la matatizo ya maji ambayo yapo katika nchi yetu hususan katika Mkoa wetu wa Mjini Magharibi na Wilaya yetu ya Mjini.

Nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa kuweza kutenga bilioni 55.4 katika kutatua matatizo ya maji.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli tatizo la maji ambalo lipo katika Wilaya ya Mjini au Tuseme Mkoa wa Mjini ni kubwa na tukizingatia juzi tu wataalamu kwamba walitueleza katika Tanzania Mji ambao unaongoza kwa watu wengi ni Dar-es-Salaam na Mji wa Pili ni Zanzibar. Zanzibar inaongoza kwa kuwa na watu wengi hususan katika Mkoa wa Mjini Magharibi. Kwa hivyo hili tatizo la maji ni tatizo ambalo linaukabili sana Mkoa wa Mjini Magharibi, hususan katika maeneo ya Jimbo la Rahaleo, Jimbo la Kikwajuni, Kwahani, Mpendae na majimbo mengine.

Mhe. Naibu Spika, ningemuomba Mhe. Waziri kwa kushirikiana na Waziri wa Ardhi , Maji, Makaazi na Nishati kwa kutumia fedha hizi zilizotengwa bilioni 55.4 kuhakikisha kwamba fedha hizi zinatatua matatizo ya maji katika Mkoa wetu wa Mjini na Zanzibar kwa ujumla.

Mhe. Naibu Spika, Mamlaka ya Maji ya ZAWA bado kuna matatizo ya baadhi ya watendaji kutotenda kazi kwa maadili katika kutatua matatizo haya ya maji. Kwa hivyo ipo haja Mhe. Waziri wa Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo pamoja na Mhe. Waziri wa Maji, Ujenzi, Makaazi na Nishati, kuhakikisha kwamba ushirikiano unakuwepo ili kuweza kutatua matatizo ya maji katika Mkoa wetu wa Mjini Magharibi.

Mhe. Naibu Spika, nikija katika suala la kilimo, juzi nilipata maelezo ya kina na kufahamishwa kwamba masuala ya kilimo yamepungua sana katika kuchangia pato la taifa. Hili ni tatizo, ukiangalia kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa taifa letu. Kwa hivyo ipo haja kuhakikisha kwamba tunaongeza nguvu katika suala la kilimo ili wananchi wetu waweze kuondokana na umaskini halkadhalika nchi yetu iweze kupata ongezeko la kuongeza pato la taifa katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, yapo maeneo ambayo yamevamiwa kama vile maeneo ya Bonde la Mwera, Fuoni, Maeneo ya Kijichi kule, nadhani ipo haja ya kuunda sheria kuweza kuyalinda maeneo haya ya kilimo, tukiweza kuyaachia tu maeneo haya yakaweza kuvamiwa ndiyo yanayoweza kuleta matatizo ya masuala haya ya kilimo.

Mhe, Naibu Spika, nikija suala la elimu. Bajeti hii imezungumza masuala ya kipaumbele haya masuala ya elimu. Suala la elimu ipo haja kwa serikali kuhakikisha inalivalia njuga na kutekeleza yale ambayo yamo katika bajeti, isiwe kila mwaka tunazungumza kipaumbele masuala ya elimu. Kuhakikisha kwamba yale yanayozungumzwa yanatekelezwa.

Mhe. Naibu Spika, wananchi wamekuwa wakijenga mabanda ya elimu lakini la kusikitisha kwamba serikali au Wizara imekuwa haitii mkono kuwaunga mkono wananchi wale na kuweza kukaa zaidi ya miaka 20 kwa mabanda yale ya maskuli bila ya kuezekwa na bila ya kumaliziwa majengo yale ili watoto wetu kuweza kuyatumia majengo yale ili kuendeleza masuala ya elimu katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, katika bajeti hii imezungumza masuala ya vijana, ajira, michezo, nadhani ipo haja ya kuhakikisha kwamba tunaelekea katika miaka 50 ya Mapinduzi matukufu ya mwaka 1964, Suala la michezo katika nchi yetu limeshuka kwa kiwango kikubwa sana. Suala la michezo ni suala ambalo linaleta umoja na mshikamano na upendo na udugu na kuleta afya kwa binaadamu.

Mhe.Naibu Spika, nadhani huko tunakokwenda tuhakikishe kwamba tunatenga fungu la kuweza kuiendeleza michezo. Kwa sababu michezo inawaweka vijana katika hali njema, katika afya njema na wanafanya kazi katika mazingira bora zaidi. Lakini wapo watu wa masuala haya ya michezo utakuta kwamba vijana wetu wanaingia katika masuala ambayo siyo ya msingi katika masuala ya madawa ya kulevya na masuala mengine ambayo hayana maadili mazuri kutokana na desturi na mila zetu za Zanzibar.

Kwa hivyo ipo haja kwa serikali kuhakikisha kwamba inaendeleza na kudumisha masuala ya michezo katika viwanja na vile vile kushiriki katika masuala ya ajira ili vijana wetu waendelee kujenga mazingira mema na wakatupeleka katika hali ambayo ya amani na utulivu.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, mimi naiunga mkono bajeti hii kwa asilimia 100 na nina imani kwamba Waheshimiwa wenzangu humu ndani tutaungana kwa pamoja kwa sababu Mhe. Naibu Spika, kule Kiwengwa tumepata maelezo ya kina kabisa, tumepata mafunzo ya kina kabisa na tumeelewa hali halisi ya nchi yetu ilivyo ya kiuchumi. Kwa hivyo nadhani kwamba hapa ni wajibu wetu kupitisha bajeti hii na kujipanga katika bajeti inayokuja ili kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: *Bismillahi Rahmani Rahim*, Mhe. Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwenye wingi wa rehema na mwingi wa utukufu, vile vile kuweza kutufikisha siku hii ya leo tukawa pamoja hapa kwa mara nyengine katika kuendeleza majukumu yetu ya kila siku ambayo hatimaye kuweza kufikia malengo tuliyojiwekea.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hatua hiyo sasa vile vile napenda kuchukua fursa hii kumshukuru ndugu yetu Waziri wa Fedha Mhe. Omar Yussuf Mzee, yeye pamoja na wataalam katika Wizara yake kwa kazi kubwa na nzito ambayo wameweza kuifanya na hatimaye leo hii tukaweza kupata *document* au kitabu hiki cha bajeti ambacho leo tunakijadili hapa.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hapo pia ninawashukuru Wawakilishi wote ambao wamo humu leo na wale ambao hawajafika kwa kuweza kuendeleza majukumu ambayo tumepangiwa kwa salama na amani.

Baada ya hapo Mhe. Naibu Spika, sasa nianze kwanza kwa utangulizi. Mhe. Naibu Spika, nilipokuwa nachangia katika bajeti kuu ya mwaka uliopita nilisema maneno haya naomba kuyanukuu.

"Mhe. Spika, katika suala la kukua kwa uchumi vile vile kuna eneo ambalo linategemewa sana juu ya suala la uzazi na vifo". Katika bajeti ambayo imesomwa hapa na Mhe. Waziri eneo hili hatukuliona hapa ni eneo muhimu ni eneo ambalo linaweza kutoa picha na dira halisi ya kuweza kujua wananchi pamoja na watu ambao wapo katika nchi yetu, pamoja na taarifa ya sensa ambayo tayari imekwisha kuwasilishwa kwetu. Sensa hii iliwasilishwa katika mwaka 2010 lakini sasa hivi tuna miaka mitatu ya ziada kama ripoti ya vizazi na vifo ingelikuwa iko hapa tungeliweza kuwa na takwimu sahihi za kuweza kujua mustakbali wa bajeti yetu na uchumi wetu katika nchi yetu ya Zanzibar. Ningelimuomba Mhe. Waziri basi atakapokuja hapa atuelezee ni sababu zipi zimesababisha hata ikabidi taarifa hii muhimu ikawa hamna wakati ni moja kati ya viashiria vinavyoweza kuleta muelekeo wa uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo naelekea katika muelekeo wa mpango wa maendeleo kwa mwaka 2013/14. Mhe. Naibu Spika, katika kitabu chetu hiki ambacho kilikuja kuwasilishwa hapa na Mhe. Waziri alitwambia hapa muelekeo wa mpango wa maendeleo utazingatia zaidi utekelezaji wa Dira ya Maendeleo 2020, mkakati wa kukua kwa uchumi na kupunguza umaskini Mkuza II , utekelezaji wa mpango wa miaka 5 wa Mkuza II, malengo na maendeleo ya *millenium* ya mwaka 2015 na ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mhe. Naibu Spika, katika ilani ya Chama cha Mapinduzi inatuelekeza kwamba hadi utakapofika mwaka 2015 pato la taifa letu lilitakiwa liwe kwa kila Mzanzibari mmoja ana uwezo wa kumiliki shilingi 824,000. Sasa hivi katika maelekezo ambayo Mhe. Waziri ametupa hapa yanatueleza kwamba pato la taifa na idadi ya watu tulionao kwa sasa 1,300,000 kwa Zanzibar kwa wastani pato la kila mtu limeongezeka limekuwa 1,003 kutoka 960. Ina maana kwa mujibu wa malengo ya pato la taifa ambayo yamewekwa na ilani ya Chama cha Mapinduzi yamepindukia na yameweza kwenda mbele zaidi.

Mhe. Naibu Spika, sasa nikiondoka huko nakuja katika jaduweli, wenzangu walikuja kulizungumza jaduweli hili ambalo ni mfumo wa bajeti mwaka 2013/2014. Wajumbe wenzangu ambao walichangia wamepita katika maeneo mengi sana lakini kuna eneo ambalo Mhe. Waziri utakapokuja hapa tunapenda kupata maelezo zaidi hususan katika kodi ya mapato kwa wafanyakazi wa SMT. Hapa naona katika mwaka 2012/13 pana ziro ziro, bila shaka patakuwa pana namba hapa sasa tunaomba ufafanuzi wa maelekezo kama kuna pahala imewekwa au vipi ili iweze kutusaidia katika mchanganuo huko mbele tunakokwenda.

Lakini tukiondoka hapo sasa nakuja katika bajeti yenyewe. Mhe. Waziri alipokuwa anawasilisha hapa maelekezo kuhusu bajeti alisema thuluthi moja ya bajeti imepelekwa katika vipaumbele vitano na kwa asilimia 37. Ukiangalia asilimia 37 ya bajeti yetu kwa vipaumbele vitano huku tukibakisha thuluthi 3 ya bajeti hapa inabidi tunaomba maelezo zaidi ili Mhe. Waziri tuweze kumfahamu zaidi hii asilimia 63 inakwenda katika maeneo gani hasa. Hili katika bajeti hii na katika maelezo haya tungependa vile vile kufahamu ni namna gani tutaweza kuendeleza uchumi wa nchi yetu, hususan ukiangalia kwamba kile ambacho kitakuwa kinakusanywa ndicho kile ambacho kitakuwa kinatumika. Sasa namna gani ya kuweza kukua uchumi katika utaratibu huu ningependa Mhe. Waziri atakapokuja hapa asaidie vile vile kutueleza.

Vile vile vipi huu mpango tulionao hivi sasa wa kwamba wafadhili wale wa maendeleo ambao tulikuwa tunawategemea sana kusaidia kwa asilimia zaidi ya 30 sasa hivi wamesitisha misaada yao ile tuweze kufahamu sababu zao zilikuwa ni nini vilevile.

Mhe. Naibu Spika, vile vile ukiangalia katika sekta ya afya bajeti hii imeelekeza zaidi katika ununuzi wa madawa, wakati tayari kuna mfuko ule wa *global funds* sijui utaratibu wake uko vipi na wao pia wapo katika *position* gani katika kutusaidia hususan katika maradhi ambayo yapo nchini kwetu kwa wingi ambayo haya mara nyingi husaidia katika suala la ukimwi na tiba.

Vile vile Zanzibar ina matatizo ya wagonjwa wa kisukari na malaria pia haijamalizika katika maeneo ya Zanzibar. Tungependa kupata maelezo nini kitafanyika katika serikali hii juu ya matatizo haya ambayo bado yanaonekana yapo.

Vile vile katika sekta ya elimu bajeti hii inaelekeza nguvu zake zaidi katika elimu ya juu, wakati msingi hasa wa elimu ulitakiwa zaidi katika elimu ya maandalizi. Sasa Mhe. Waziri atakapokuja hapa tutaomba atusaidie mikakati inayopangwa katika bajeti hii juu ya suala zima la kuendeleza elimu ya maandalizi.

Lakini nikiondoka hapo nikija katika suala la sherehe za Mapinduzi ambazo zitakuwa zinatimiza miaka 50 ya maadhimisho yake. Mhe. Naibu Spika, mimi kwa upande wangu pamoja na matayarisho haya ambayo yapo hapa tunayaona na katika buku kubwa huko tumeona katika Mawizara namna walivyojipanga. Lakini pia mimi niulize tu kwa upande wetu sisi Wazanzibari sasa hivi tunataka kusherehekea mwaka 2014 miaka 50 ya uhuru wa Zanzibar, lakini bado hatujawa na kielelezo cha historia ya Mapinduzi yenyewe ya Zanzibar. Naomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze mikakati gani iliyopangwa ili kuendeleza historia ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar.

Baada ya hapo sasa Mhe. Naibu Spika, nikija katika mtandao wa ajira kwa vijana. Mhe. Naibu Spika, pamoja na maelezo ambayo yamo humu juu ya suala la kuwasaidia na kuwawezesha vijana hususan katika eneo la uwezeshaji bado tunamuomba Mhe. Waziri mipango hii ambayo imepangwa haijajitosheleza kwa ajili ya kuwasaidia vijana hususan kuwasaidia kutokana na matatizo ambayo yanawakabili juu ya ajira. Tungependa kufahamu zaidi mikakati gani ya ziada ambayo itakuwa inapangwa na serikali yetu kuhakikisha kwamba vijana wanasaidiwa na kuona kwamba wanaondokana na utaratibu wa sasa wa kukaa katika vijiwe wakawa hawana kazi za kufanya hali ya kwamba miaka inakwenda tu siku hadi siku.

Suala jengine mimi naipongeza bajeti hii na nasema kwamba tukiangalia tulikotokea tulipo na tunapotaka kwenda ni bajeti ambayo inasaidia kwa maslahi ya nchi yetu na inasaidia kwa mtazamo wa maisha yetu na hali yetu ya kiuchumi ndani ya Zanzibar yetu.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, mimi naunga mkono hoja kwa asilimia mia. Ahsante sana.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Naibu Spika, na mimi sina budi kutoa shukurani za dhati jioni hii kupata nafasi ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ambayo imewasilishwa kwetu ili na sisi tuingize nyalio katika hotuba hiyo.

Mhe. Naibu Spika, kwa upande wangu mimi naomba mchango wangu nianze katika kifungu cha 30 ukurasa wa 20 hati 21. Mheshimiwa hapa tunazungumza sensa ya watu na makaazi. Mhe. Naibu Spika, kwa maelezo ya takwimu ya sensa na makaazi ya Tanzania 44,928,923 ni hatua moja kubwa kwa kweli iliyofikiwa. Lakini pia kwa upande wa Zanzibar kutokana na sensa hii inajionesha kwamba wapo watu 1,303,569.

Mhe. Waziri katika kitabu hiki pia alisema kwamba pamoja na kupungua kwa wananchi kiasi chetu cha ukuaji wa idadi ya watu kutokana na asilimia hiyo

3.1 kwa mwaka baina ya sensa iliyopita, lakini hapa Mhe. Naibu Spika, ukiangalia sensa wakati ulipofika kutaka kuhesabiwa watu, lakini pia ilielemewa na mambo mengi mazito. Kuja kwa sensa kuliingia na mpango wa uandikaji wa Katiba, haya maoni yalikuja vibaya upande mmoja haukushirikishwa, kwa hivyo Wazanzibari wakaanza kuleta hoja zao kutokubali kuhesabiwa. Kwa hivyo hapa ilikuwa ni changamoto kubwa na watu wengi wakakataa kuweza kuandikishwa.

Kwa kweli mimi naamini kwamba idadi hii iliyotoka ya Wazanzibari 1,300,000 naamini kwamba Wazanzibari wanapita idadi hii. Lakini kutokana na wananchi walivyokuwa na maoni yao, kwamba baadhi ya maoni yao yalikuwa yanasema kwamba vijana wengi hawana ajira, lakini kuhesabiwa wanafuatwa mpaka maeneo yao, lakini kutafutiwa ajira inakuwa ni kikwazo kwao. Kwa hivyo kama hawajapatiwa ajira hawatakuwa tayari kuweza kuhesabiwa hilo lilikuwa ni dai moja.

Dai jengine wananchi wengi walikuwa wanadai kupatiwa vitambulisho vya ukaazi, hili limekuwa ni kikwazo kwa wananchi kutopatiwa vitambulisho, kwa hivyo wakasema kama hawajapatiwa vitambulisho hawawezi kuingia katika hesabu. Kwa hivyo haya ni madai na mengine kadhalika walikuwa wananchi wanatoa. Kwa hivyo ukiangalia takwimu tuliyonayo wazanzibari laki tatu na hawa wananchi wanaodai basi inaonesha kwamba ni kweli kwamba wananchi wengi hawakujiingiza katika hesabu.

Lakini sasa katika changamoto hizi Mhe. Naibu Spika, utakuta serikali itapanga maendeleo yake lakini itafika pahali itatokea matatizo hasa katika maeneo ya afya na elimu. Afya pengine serikali inaweza kuagizia madawa hapa karibuni kwa mwezi elfu hamsini lakini ukiangalia haufiki nusu mwezi huduma hii ya madawa imekatika njiani kutokana kwamba hesabu tuliyokuwa nayo ya takwimu ya watu ni ndogo kulikoni wale watu ambao hawakuingia katika hesabu. Kwa hivyo ni vyema serikali ikawa na tahadhari ya suala hili kwamba wasije wakaona kwamba hii ndio idadi halisi ya Wazanzibari ambao wamo katika sensa.

Lakini pia Mhe. Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa sensa ni vyema unapofika wakati wa sensa na yakatokeza mambo mengine basi serikali huwa karibu kuzima lile joto la wananchi ili wananchi waingie vizuri katika sensa kwa sababu sensa ni kitu muhimu katika nchi yoyote, sensa ndio inayojua mahesabu ya watu, wakaazi, nyumba na mambo mengine mbali mbali. Kwa hivyo hili lazima serikali inapofika miaka mengine yakitokea mambo ambayo wananchi hawayaungi mkono katika sensa ile basi wawe karibu sana na waweze kuwasikiliza matatizo yao.

Mhe. Naibu Spika, pia Mhe. Waziri wa Fedha katika kuwasilisha amesema kwamba miji hii mikubwa kama Dar es Salaam na Zanzibar wananchi wengi wanahamia zaidi katika maeneo haya kulikoni maeneo mengine. Hili Mhe. Spika, mimi nasema kwamba serikali yenyewe inachangia kuwalazimisha wananchi watoke katika mikoa mengine na wilaya wahamie katika miji hii mikubwa. Kwa nini? Kwanza vipaumbele vyote vya maendeleo vipo katika Mkoa wa Mjini Magharibi au Dar es Salaam pale. Utakuta serikali iko pale, mawizara yapo pale, ma-*ngo's* yapo pale na wananchi wanachotafuta ni ajira. Kwa hivyo kama ajira zote wamezichukua wamezipeleka mjini basi aliyekuwepo shamba Kizimkazi atatoka atakuja kuhamia mjini kwa sababu anatafuta ajira.

Lakini kama serikali ilitoa njia mbali mbali wakawa kule Mkoa wa Kaskazini kuna mambo ya serikali, kuna *ngo's*, kuna mawizara kule, basi wananchi wangekuwa wanapata ajira kutokana na Mikoa yao. Lakini siku zote unapozichukua taasisi zote za serikali ukaziweka pahali pamoja bila shaka unawaambia watu wahame katika maeneo yao wakahamie katika maeneo ambayo ajira inaweza kupatikana. Na bila shaka itakuwa siku zote maeneo haya yatakuwa mafupi yatakuwa madogo, kwa sababu nyenzo zote za maisha umezilazimisha kuwepo pale. Hivi sasa tuna sera kwamba Zanzibar ni ndogo, mimi nakataa kwamba Zanzibar si ndogo ama Mjini Magharibi kweli padogo lakini Zanzibar sio ndogo. Ukielekea upande wa mashariki ya kati huku utakuta kuna maeneo mengi makubwa mazuri hayana mtu wa kuishi kwa sababu hapana nyenzo pale.

Lakini si kweli kama serikali wanachukua baadhi ya miundombinu na wakaipeleka katika maeneo hayo. Wananchi moja kwa moja wanaweza wakafuata kule kwa sababu itakuwa ajira zinapatikana, lakini mambo yote yamewekwa hapa. Kwa hivyo ni kweli kwamba Mkoa huu utakuwa mdogo na utazidi kuwa mdogo.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo nakuja ukurasa wa 46 kuna maeneo ya kipaumbele. Mimi Mhe. Naibu Spika, katika hapa kuna *program* hii ya mageuzi ya kiuchumi, katika mageuzi ya kiuchumi Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri alitaja maeneo mengi hapa lakini mimi nataka nilizungumzie eneo moja, tena hapa naomba nipatiwe maelezo ya kina kabisa ili niweze kufahamu nini alichokielezea. Kwa sababu katika hotuba yake hapa hakutoa ufafanuzi. Mhe. Naibu Spika, naomba anieleze Mhe. Waziri namna gani ataimarisha sekta ya utalii, biashara, viwanda na kilimo. Naomba nipate ufafanuzi hapa katika kifungu hiki kwa sababu hapa hajatuwekea ufafanuzi wa kutosha ili niweze kuridhika na hoja hii.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nizungumzie suala dogo tu suala zima la utalii, suala hili la utalii kwa kiasi fulani wawekezaji wameitikia wito maeneo mengi katika fukwe zetu utakuta mahoteli yapo ya kutosha kabisha. Ukianza Kaskazini ya Mashariki hadi Kusini, Kaskazini ya Magharibi hadi Kusini ya Magharibi mahoteli yameenea. Na kwa kweli hawa ndugu zetu wamekuja kuitikia wito wa Serikali ya Zanzibar. Lakini sasa Mhe. Rais wa awamu ya tano alifanya jitihada kubwa ya kuweza kuwakaribisha wageni na kwa kweli wageni wakaja wakawekeza katika nchi yetu.

Lakini Mhe. Naibu Spika, huu uwekezaji kwa kweli ninamuomba Mhe. Waziri ajaribu kuzitizama sheria hizi ili zirahisishe zaidi huu uwekezaji kwani inaelekea kwamba baadhi ya sheria zimekuwa ni kikwazo. Lakini mara nyingi Mhe. Naibu Spika, najiuliza hizi sera za sheria za utalii na kadhalika kwa nini ikawa hawa wawekezaji wanapata vikwazo hivi na sisi ndio wahitaji. Kwa hivyo wakati sisi ni wahitaji ni lazima tuweke kitu ambacho kinamtoa mtu nje anakuja hapa lile analokusudia linaweza kupatikana kwa haraka.

Mhe. Naibu Spika, kuna muwekezaji huyu amekuja hapa nchini huu ni mwaka wa 5 kama kuwekeza na kwa kweli uwekezaji wake si mdogo, katika barua yake hii aliyopeleka ZIPA, sisi tulipokuwa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo tuliwahi kutembelea hili eneo. Huyu muwekezaji malengo yake ni kujenga hoteli ya nyota sita katika maelezo yaliyomo, lakini huu ni mwaka wa sita hajapata kibali cha mazingira. Kakusudia kuwekeza shilingi milioni 15 *dollars* katika nchi hii hapo Mhe. Naibu Spika, ni kiasi gani cha fedha ambacho kiingie katika nchi yetu, ni fedha nyingi. Lakini badala ya sisi kumtayarishia vizuri muwekezaji huyu ameshindwa hadi leo. Pengine sina uhakika ile asilimia kumi watu hawajapewa likawa ni tatizo. Sasa ukiona watu wanaangalia zaidi maslahi yao binafsi kuliko maslahi ya nchi siku zote tutakuwa tunawaonea wananchi wetu wadogo kwa kulipa kodi, kumbe watu wa kulipa kodi na kutoa ajira wapo lakini sisi wenyewe bali ndio tunawazuia.

Hapa Mhe. Naibu Spika, ninukuu tu kauli ya Rais wa Kwanza Tanzania Mwalim Julius Nyerere alisema, "Wazanzibari uchumi wanao lakini wameukalia" na ndio kama hivyo Mhe. Naibu Spika, muwekezaji katoka nje na mabilioni yake ya *dollars* kaja nayo hapa kwetu Zanzibar mwaka wa sita kashindwa kupewa kibali cha kuanzisha uwekezaji huu, huku ni kuukalia uchumi. Sasa tumesema mlango uwazi lakini katika kusema mlango uwazi kumbe nyumba yetu ina geti, mlango huu wa geti ndio ulio wazi lakini mlango wa pili umefungwa kwa makufuli mazito mazito. Kwa hivyo si rahisi muwekezaji kuweza kuwekeza. Mimi ninamuomba sana Mhe. Waziri wa Fedha hizi sheria ambazo zinawakwaza hawa wawekezaji ni lazima tuziangalie na tuzifanyie marekebisho ili wawekezaji wetu waweze kuwekeza na nchi iweze kuingiza mapato.

Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, huyo muwekezaji yupo Paje, muwekezaji huyu tayari ameshajenga hoteli, hoteli tayari analaza wageni, lakini wakubwa wa nchi hii hii, akaanza kulipa kodi, mwaka wa pili katakiwa kodi asilipe na tayari anazalisha pale. Kumbe sisi wenyewe pia hatuko tayari hii nchi kuiletea maendeleo. Hili Mheshimiwa ni tatizo, kwa hivyo muwekezaji mambo yake yamekamilika yeye anataka kulipa anaambiwa asilipe na sisi tumekwenda tukaliona hili, Hoteli ya *Spice Islander* ambayo iko Paje pale amezuia mwaka asilipe tunafanya nini, tunaacha nini Mhe. Naibu Spika. Kwa hivyo nasema hili ni tatizo ni lazima sheria zilizopo kwa yule ambaye ishafika wakati wa kulipa kodi basi aendelee kulipa kodi na hali kama hii ikiendelea hivyo tunaona kwamba kuna watu wanajinufaisha matumbo yao. Haiwezekani sheria inamruhusu wewe ukamwambia kwamba usilipe, alipe nani? Aje alipe mama ntilie, aje alipe mpika visheti, aje alipe mtu mwengine yeyote dhaifu hatutafika Mhe. Naibu Spika. Kwa hivyo ningeomba sana Mhe. Waziri haya mambo yafuatiliwe. Mimi naamini kuna watendaji wana hamu ya nchi yao iende vizuri lakini pia naamini kuna watendaji wa kujinufaisha matumbo yao. Hasa kama hapa hatutasimamia ikawa serikali inabakia katika maeneo ya ofisi tu hawafuatilii katika maeneo mbali mbali hatutofikia malengo Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo nije katika ukurasa wa 38 mpaka 51 kifungu cha 56 pale katika kurasa hizi zimesema habari za kodi, lakini mimi napenda kuzungumzia kuhusu mapendekezo ya hatua za kuimarisha mapato. Kuna mapendekezo mengi pale Mhe. Waziri ameyatoa, mimi Mhe. Naibu Spika, naunga mkono yale mapendekezo kama tutakuwa wakweli na wasimamizi nchi yetu inaweza ikapiga hatua. Lakini tatizo ni usimamizi waswahili wanasema Mhe. Naibu Spika, "*jambo haliwa likita msimamizi*" mwishowe wakamalizia "*na majaliwa"*. Lakini hili majaliwa tuliache tuchukuwe usimamizi. Nchi yetu ina matatizo ya kusimamia mipango yake tukitaka tusitake hivi ndivyo ilivyo, tunazaa mipango mingi kabisa lakini kuisimamia ni tatizo na siku zote Waheshimiwa tunaenda katika semina mbali mbali watu wanafanya makosa halafu tunasema ah! Kwamba huyu ni mjomba sijui shangazi lake, sijui mama yake mdogo, hasa habari kama hizo tuna maana gani Wazanzibari kuweka vyombo vya ulinzi kuweka Mahakama ni ya nini? Kuweka polisi ni ya nini? Wakati sisi ni mjomba na shangazi, tumewekwa kwa sababu tufuate taratibu za sheria na katiba, lakini mtu anafanya makosa tunasema huyu mtoto wa Rais, ni mjukuu wa Rais Mstaafu, sijui nani hatutafika. Sasa ni lazima tusimamie mambo yetu, tukishasimamia mambo yetu majaliwa yatakuja. Lakini tutakapokosa kusimamia Mhe. Naibu Spika, nakuhakikishia majaliwa hayatokuja hata siku moja na tunaona hivyo tokea mwaka wa 1950 hakuna ithibati yoyote ile ambapo tukasema hichi ni neema ya Mapinduzi hatuna, sisi tunakwenda tu. Sasa naomba sana Serikali

isimamie mipango yake na tutakapoisimamia hiyo mipango basi tutapiga hatua kubwa kabisa katika maendeleo ya nchi.

Mhe. Naibu Spika, kwenye ukusanyaji wa kodi. Hizi kodi wananchi wanatoa, wafanyabiashara wanatoa lakini usimamizi ni mbovu, nchi hii kila sekta kila eneo watu wanakusanya kodi kama *ZRB, TRA*, BARAZA LA MANISPAA na kuna maeneo mengine mbalimbali. Lakini pia Mhe. Naibu Spika, nimuombe Mhe. Waziri, mubadilishe huu mfumo wa kukusanya kodi, isiwe kila pahali kunakusanywa kodi hivi mapato yanapotea. Tuwarahisishie wafanyabiashara wetu lakini kila mtu unamtaka wewe anufaike baada ya kunufaika Serikali hapa haitonufaika na badala yake watanufaika hao wanaokusanya. Mimi nikuombe sana Mhe. Waziri, tuanzisheni mfumo mwengine tutoke katika mfumo tulionao.

Mhe. Naibu Spika, katika mapato haya ni lazima Serikali iangalie hasa ndugu zetu madereva, hawa madereva baadhi ya njia biashara zao ni nzuri, lakini baadhi ya barabara nyengine biashara zao ni mbovu. Kuna barabara wana zamu A na B lakini kutokana na upungufu wa wasafiri inalazimika zile zamu zake zigawike tena mara mbili, kama mtu kwa mwezi alikuwa anakwenda siku 15 sasa anakwenda siku 7 au 8 anahitaji kulipia gari, kununua mafuta na kujilipia yeye katika maisha yake, sasa kile kipato anachokipata ni kidogo mno. Mimi namuomba sana Mhe. Waziri, haya maeneo ayaangalie, isiwe barabara zinazokuwa na watu wengi kodi yake ni sawa na barabara zenye upungufu wa watu. Kwa hivyo hapa ninakuomba sana Mhe. Waziri, uje utufafanulie kodi hii ya barabara.

Kwa kumalizia Mhe. Naibu Spika, tuseme kwamba kuna wafanyakazi wetu madereva, madereva ndio wanaoendesha viongozi wa Serikali hii, lakini dereva anakupeleka safari yako kwa wakati unaoutaka, akuweke ofisini anakusubiri mpaka uondoke pengine mpaka inafika saa 3 au saa 4. Lakini Mhe. Naibu Spika, mishahara yao hautoshi ni mdogo mno na hiki ni kilio cha madereva wetu, kwa nini hawaangaliwi hawa, yeye anakufurahisha wewe lakini kilipo unachomlipa hakimtoshi kwa siku, tunafanya nini tunaacha nini? Nakuomba sana Mhe. Waziri, hawa madereva wetu tuwaangalie angalau wewe ukifurahi na yeye afurahi ili safari yako iweze kwenda salama.
Mhe. Naibu Spika, kwa hayo machache mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Tumbe tunaunga mkono hoja hii. Ahsante.

Mhe. Asha Abdu Haji: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa fursa hii ya kuchangia bajeti hii iliyoko mbele yetu. Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema jioni hii.

Mhe. Naibu Spika, nampongeza Mhe. Waziri, na watendaji wake kwa kukaa na kupanga bajeti hii ingawa ina mapungufu makubwa mno kwa wananchi wake.
Mhe. Naibu Spika, nije katika muelekeo wa hali ya uchumi, jadweli ukurasa wa 4. Mhe. Naibu Spika, bajeti ya mwaka 2012/13 katika afya ya uzazi, jinsia na kupunguza umasikini ilikuwa shilingi milioni ishirini na mwaka 2013/14 bajeti hii makisio ni shilingi milioni mia moja na arubaini je suala Mhe. Waziri, ni sababu zipi zilizopelekea kiwango hiki cha fedha kupanda kiasi hicho.

Mhe. Naibu Spika, uimarishaji wa uvuvi Bahari Kuu. Kipindi kilichopita bajeti ya mwaka 2012/13 makisio yalikuwa shilingi milioni mia tatu lakini kipindi hiki 2013/14 imekisiwa au kutenga shilingi milioni mia moja, je kweli mmekusudia hasa kuimarisha uvuvi wa Bahari Kuu na ni lini hasa tutafikia malengo ya uvuvi wa bahari kuu na kupata faida na ajira kwa wananchi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu mwani, mwani ni zao kubwa ambalo wananchi wameliitikia sana na hususan wanawake ambao wamepata ajira kwa kujiajiri wenyewe. Mhe. Naibu Spika, lakini zao hili ni zao ambalo Serikali bado kabisa hawajalitilia maanani kama karafuu. Mwani ni zao ambalo wananchi wameliitikia sana tokea mwaka 1988 watu hawa bado hawajapata tija kuhusu zao hili, na zao hili lina kazi kubwa na wenzetu wageni wanasema kwamba zao hili lina mambo mengi linaliwa, linafanyiwa rangi za nguo na kadhalika, lakini bado Serikali haijalitilia maanani bado wananchi wanateseka na kilo ni shilingi mia nne na hivi sasa mwani unaharibika kilo shilingi mia tatu, je Serikali hailioni kwamba hili ni tatizo kwa wananchi wake. Ningeomba Serikali kwamba tatizo hili ilitizame kama tunavyoitizama bei ya karafuu na hili liangaliwe ili lichukuliwe mikononi mwenu ili wananchi wake wafaidike.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu kodi ya *VAT* ningeiomba Serikali kodi ya *VAT* ambayo wananchi wake watumiaji wa umeme na hususan umeme wa majumbani watumiaji wadogo wadogo. Ningeiomba Serikali watumiaji hao wanatumia kwa shilingi elfu ningeiomba Serikali iangalie tatizo hili na liwaachie wafanyabiashara wakubwa wakubwa ili kuwapunguzia ukali wa maisha wananchi wake.

Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja mia juu ya mia.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi nikaweza kuchangia. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia jioni hii na mimi nikaweza kuchangia. Nampongeza Mhe. Rais Dkt. Shein kwa utekelezaji wake wa Ilani ya CCM na kuiongoza

nchi yetu kwa amani na utulivu. Pia nampongeza Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo na watendaji wake wote kwa kutuletea bajeti hii.

Mhe. Naibu Spika, bajeti hii ni muhimu kwa maendeleo ya watu na ustawi wao. Bajeti hii iende na matokeo ya sensa ya watu ya mwaka 2012 ili kujua idadi ya watu na kupanga mipango bora ya maendeleo kulingana na wingi wa watu hasa katika sekta za elimu, afya na maji safi na salama. Mfano Mkoa wa Mjini Magharibi kuna watu 593, 678 ambao ni karibu nusu ya wananchi wote. Bajeti hii ni nzuri sana ya maendeleo kwa mwaka 2013/14. Sasa nitaanza na Wizara ya Afya.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Afya katika mradi wake wa malaria imetengewa milioni mia tatu na tano toka fedha za Serikali na Wahisani. Mhe. Naibu Spika, mradi huu kusema kweli umefanya vizuri sana tena mimi nawapongeza, naipongeza sana Wizara ya Afya kwa jitihada yao hii ili waendelee kutokomeza maradhi ya malaria. Lakini ili waweze kufanya kazi hiyo inatakiwa hizi fedha walizokuwa wamepangiwa wapewe kwa wakati.

Mhe. Naibu Spika, nije katika Hospitali ya Mnazimmoja ambayo tunatarajia kuwa Hospitali ya Rufaaa kuhusu *incinarator*. Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri, alituambia kwamba *incinarator* ipo na mimi ni Mjumbe katika kamati ya Wizara hiyo ni kweli ipo lakini mbovu. Sasa kwenye kitabu cha bajeti niliona kwamba wamepangiwa kuhusu *incinarator*, sasa naiomba Serikali kupitia Mhe. Waziri wa Fedha, hizo fedha walizokuwa wametengewa wapewe kwa haraka kwa sababu ni hatari, sisi kama Kamati tulienda kule tukaenda tukaoneshwa taka zinatupwa pembeni mwa bahari, maji yajae ndio zile taka zichukuliwe ziende kwenye bahari, hivyo hili ni tatizo. Sasa Mhe. Waziri, jitihada zako zote hili la *incinarator* ulione.

Mhe. Naibu Spika, nakwenda katika Wizara ya Elimu. Wizara ya Elimu imepangiwa jumla ya bilioni thalathini na tano na milioni mia tano na arubaini na saba zimetengwa kwa Wizara ya Elimu ili kuimarisha huduma za elimu ikiwemo ujenzi, madarasa, upatikanaji wa vitabu na madeski, pamoja na kuwaajiri walimu wapya. Wizara hii ya Elimu ijipangie vizuri fedha hizo ili waweze kutekeleza yale malengo waliyoyakusudia wafanye vizuri.

Mhe. Naibu Spika, labda tatizo hili la wanafunzi wengi katika maskuli, tatizo hili ni tatizo zito hasa katika Mkoa wa Mjini Magharibi, katika Mkoa huu kuna darasa mwalimu mmoja wanafunzi mia, sasa naiomba Serikali iliangalie tena suala hili ione itafanya nini ili kupunguza hawa wanafunzi.

Mhe. Naibu Spika, naenda Wizara ya Wanawake na Watoto. Wizara hii naipongeza Serikali kwa kuangalia kwa jicho la huruma kwa kuwapangia

shilingi milioni mia moja na hamsini na sita kwa kukuza usawa wa jamii na kuwainua wanawake milioni mia mbili na thamanini na nane zimetengwa katika programu ya pamoja na kuimarisha hifadhi ya watoto, na shilingi milioni mia tano na ishirini kwa mradi wa haki za kisheria kwa watoto, sasa miradi hii kama itatekelezwa ipasavyo italeta tija nzuri.

Mhe. Naibu Spika, ni kweli Wizara hii ina kazi kubwa hasa kwa wanawake na watoto. Mhe. Naibu Spika, tumewaona watoto ambao wamejikusanya pamoja kusaidiana wenyewe kwa wenyewe kupitia pesa zao wanazopewa za skuli. Sasa naiomba Wizara kama watoto hawa walivyokuwa wamekusudiwa basi Wizara iwaone ili kuwasaidia, kwa sababu sijaona mtoto akapewa pesa yake ya skuli shilingi mia akaenda kumchangia mwenzangu kumsaidia mabuku ili arudi tena skuli.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa pamoja na juhudi za Serikali katika uchimbaji wa visima lakini tatizo la maji bado hasa katika Mkoa wa Mjini Magharibi. Mhe. Naibu Spika, kipindi kilichopita bajeti ya 2012 mimi nilichangia kuhusu maji katika Mkoa huu na kipindi hicho nilichangia ilikuwa karibu na kufika mwezi wa Ramadhani nikalisema suala hilo lakini bado maji hatujapata.

Mhe. Naibu Spika, mimi naunga mkono kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Mjini Magharibi naunga mkono mia kwa mia.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi niunge mkono wenzangu waliotangulia kwa kutoa shukurani kwa kupata nafasi hii ya kuchangia bajeti au hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba kukubaliana na Mhe. Waziri, kwa kutoa pongezi kubwa kabisa kwa uchaguzi uliofanyika katika Jimbo la Bububu baada ya kutangulia mbele ya haki aliyekuwa mwenzetu Mhe. Salum Amour Mtondoo na Mhe. Hussein Ibrahim kuibuka kuwa mshindi, na uchaguzi wenyewe Mhe. Waziri amesema kuwa pengo limezibwa na limezibwa vyema. Lakini pia natoa pongezi kwa uchaguzi uliofanywa juzi katika Jimbo la Chambani baada ya kifo cha aliyekuwa Mbunge Ndugu Salum Hemed na nafasi yake kushikwa na Mhe. Yussuf Khamis. Kimazingira uchaguzi wa Chambani ulikuwa ni mzuri hakukuwa na vurugu na natoa pongezi za dhati kwa jeshi la polisi kwa kuweka amani na utulivu katika uchaguzi huo. Kwa vile si jambo la kulizungumza tena tukiangalia katika mazingira ya chaguzi hizi mbili ikiwa Bububu pengo limezibwa vyema, ule wa Chambani je Mhe. Waziri atatoa msimamo gani katika uzibaji wake, hilo naomba jibu.

Mhe. Naibu Spika, la pili imezungumzwa katika bajeti hii ni sensa ya watu na makaazi. Tuliambiwa kuwa katika Tanzania nzima watu waliohesabiwa idadi yake ilikuwa ni milioni arubaini na nne lakini tisa na ishirini na nane na mia tisa na ishirini na tatu, kati ya hao milioni moja laki tatu na alfu tatu na mia tano na sitini na tisa ni Wazanzibari, na kwa hivyo milioni arubaini na tatu laki sita na ishirini na tatu ni watanzania bara.

Mhe. Naibu Spika, hapa nataka ufafanuzi, tunajua na ninataka ufafanuzi kutokana na umuhimu wa watu katika kupanga bajeti. Tunajua katika kisiwa cha Zanzibar kuna msemo kwamba *Zanzibar ni njema atakaye aje*, lakini kwa bahati mbaya watu hawaingii kwa utaratibu. Tumeshuhudia nchi hii haina *passport*, tumeshuhudia kuna watu wanatoka kila sehemu wanaingia hapa kwa wingi kiasi wamejazana mpaka Mkoa wa Mjini Magharibi unapigiwa makelele kwa watu walivyokuwa wengi na wanaendelea kila siku kuongezeka bila ya kuweko na utaratibu. Kwa sababu Mhe. Waziri, katika hotuba amesema kwamba hii hali inatisha na inahitaji kudhibitiwa, na kwa sababu nchi hii hata *passport* haina na kwenye idadi ya watu ndipo utakapoweza kupima mipango yako ya maendeleo, Mhe. Waziri ana ushahidi gani kuona hii hali imethibiti ikiwa ni pamoja na watu sasa wajulikane waliopo Zanzibar wanaoingia na kutoka na kwenda wanaoingia na kuhamia maisha ili hesabu yetu iwe ya uhakika.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri anaweza kuniambia katika sensa hii kwa sababu sensa inahesabu wa kila aina ni Wazanzibari wangapi wamepatikana katika sensa hii, ni wangapi ni watanzania lakini bado hawajawa wazanzibari, ni wangapi ni wageni, ili tuweze kujua kama takwimu hizi ni sahihi kwa ile siku iliyotolewa, na tokea hapo ilipomaliza takwimu ya sensa hii na mpaka hii leo wameshaingia wangapi mpaka akaweza kupanga mipango hii ya maendeleo na akatoa pato la kila mtu.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo naomba kuzungumza ni kuhusu pato la taifa. Mhe, Naibu Spika, kwa taarifa yake Mhe. Waziri amesema kuwa pato la taifa limeongezeka na kukua kwa asilimia 7 kwa mwaka 2012 kutoka asilimia 6.7 kwa mwaka 2011, na Mhe. Waziri amesema kwamba miongoni mwa mambo yaliyochangia ukuaji huo ni pamoja na sekta ya viwanda. Mhe. Naibu Spika, mara tu baada ya Mapinduzi muasisi wetu Mwenyezi Mungu azidi kumpa maisha mazuri huko aliko aliingiza nchi hii kwa viwanda na kuwa viwanda vya kweli kweli. Kulikuwa na kiwanda kikubwa tu cha sukari na tukipata sukari sote tena nzuri pamoja na mambo mengine yanayotokana na hayo, kulikuwa na kiwanda cha viatu, kulikuwa na kiwanda cha sigara, kulikuwa na viwanda vidogo vidogo, kulikuwa na kiwanda cha nguo, kiwanda cha makonyo Pemba, kiwanda cha soda na vingine nilivyovisahau, vyote vimekufa na vilikuwa ni viwanda kweli sio masihara, leo tumebakiwa

na viwanda vya maji ati na viwanda vya mawe, ambapo mimi viwanda vya mawe hata sijui ni vile viwanda vinavyosaga kokoto na kadhalika na maendeleo yanapatikana ati watu kwa kujenga majumba na kadhalika.

Mimi Mhe. Naibu Spika, haingii akilini kuwa viwanda vyote vizuri tena madhubuti vilivyokuwa vikifanya kazi na kuzalisha katika nchi hii vimekufa vyote na kuna viwanda vichache viliopo tena vidogo ambapo rasilimali yake haina tija kiasi hicho tukaambiwa kuwa tumekuwa kwa viwanda, yaani viwanda vimekuwa kwa asilimia 9.12 kwa 2012 si kama ilivyokuwa mwaka 2011 ambapo ilikuwa asilimia 5.8. Ningeliomba kujua ni viwanda vipi hasa vya maana vilivyopo vinaingiza nini kuliko vile vya zamani na idadi ya watu waliokuwepo mpaka tukasema uchumi wetu umekuwa, naomba nifahamishwe hapo.

Mhe. Naibu Spika, lililozungumzwa kuchangia maendeleo ya Kilimo. Tunajua hapa Zanzibar ni nchi ambayo hali ya hewa yake na mazingira mengine yalivyo ni nchi yenye rutuba sana na ni nchi iliyo katika sehemu ya dunia ambayo miti inaota na kunawiri vizuri sana, miti mikubwa, miti midogo na miti ya mboga mboga, viungo na kadhalika, ni nchi ya maajabu kwa kweli, hapo zamani hata tambuu ilikuwa ikiuzwa na kuingizia pesa na popoo. Sasa Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa taarifa yake Waziri amesema kuwa hali ya kilimo imeshuka na mchango ambao umechangiwa na kilimo umeshuka vile vile kama alivyoeleza katika bajeti yake. Ameeleza kuwa sekta ya kilimo ilikuwa kwa asilimia 1.3 na hivyo kasi yake ilishuka kutoka asilimia 2.7 ya mwaka 2011. Na vile vile kilimo hicho kilichangia asilimia 30.2 mwaka 2012 kutoka asilimia 32.2 mwaka 2011, hapa nilivyofahamu mimi ambapo sina utaalamu huu ni kuwa kilimo kimekuwa kidogo na pato limekuwa kidogo na watu wameongezeka kuliko kawaida katika nchi hii, hivyo ukuaji hapa wa sekta hii ya kilimo ilikuwaje mpaka ukazungumziwa kuwa umesababisha kukua kwa pato la taifa.

Halikadhalika Mhe. Naibu Spika, viwanda navyo ambavyo vilikosa kufikia asilimia 9.2 mwaka 2012 kutoka asilimia 5.8 mwaka 2011 imechangia asilimia 11.7 mwaka 2012 kutoka mchango wa asilimia 12.0 mwaka 2011, na hivyo viwanda pia ambavyo kwa takwimu ninazoziona hapa na ndivyo ilivyoandikwa ni kuwa viwanda tunaambiwa vimekuwa lakini uzalisaji wake umekuwa ni mdogo kulinganisha, sasa ukuaji huu wa uchumi kutokana na viwanda ulikuwa vipi naomba nifahamishwe.

Mhe. Naibu Spika, jengine kwa ruhusa yako tunajua ili nchi iendelee tunahitaji kuwa na mapato, na tuwe na vianzio vingi tu vya kukusanya mapato, kuna mapato yaliyokuwa si ya kodi na kuna mapato ya kodi na mambo mengine na kadhalika.

Katika nchi hii ndogo yenye watu 1,303,569 kwa hesabu ya sensa ina wakusanyaji wawili wakubwa wa kodi, kuna *TRA* na *ZRB*. *TRA* ni ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na *ZRB* ni ya Zanzibar na wanaokusanyiwa kodi ni Wazanzibari na vyombo hivi viwili vikubwa na kila kimoja kinakusanya kodi na kuweka makadirio yao ili yafike hapo wanapokusudiwa na wanaotoa kodi ni Wazanzibari wanyonge.

Sasa mimi naomba niwekewe wazi, hivyo kweli kumepangwa mipango ambayo *TRA* inajua mipaka yake na *ZRB* inajua mipaka yake kwa sababu nilipokuwepo kule Wete nilipata malalamiko ya wafanyabiashara wadogo wadogo ya kusema kuwa kila mmoja anachukua kodi katika sehemu ile au kuna kodi maalum za mtu yule yule hizi za kwenda *TRA* na hizi zinakusanywa na *ZRB*. Naomba nipate ufafanuzi huo kwa sababu ni vigumu kodi mbili kubakia katika nchi moja.

Halafu jengine hebu na tukae tujiulize Zanzibar ilikuwa ni sehemu tu ya Jamhuri ya Muungano lakini sasa katika Katiba mpya Zanzibar ni nchi na mipaka yake. Kwa hivyo, kama ni nchi kuna mambo lazima tubadilike. Hivyo, hii *ZRB* ingelipewa uwezo wa kukusanya kodi zote kwa namna ambayo inaonekana na kwa mujibu wa Katiba na Sheria isingeliweza kufanya kazi hiyo mpaka na *TRA* ikusanye kodi, wakati hasa kutokana na wengine walivyozungumza jana ni kuwa hii kodi inayokusanywa na *TRA* yote baadae inaletwa hapa hapa Zanzibar. Kwa hivyo, nataka nijue kwanza hizi fedha kuna ulazima gani wa kuweka vyombo hivi viwili vya ukusanyaji na kwa nini, kwa sababu hii ni nchi yetu na tuna chombo chetu kinachohusiana na kodi kwa nini *TRA* haiachiwi Bara ikafanya shughuli zake na hapa *ZRB* ikajitumisha na kufanya kazi kwa maslahi ya uchumi wa nchi hii. Hii itasaidia pia kwa vile ni chombo chetu kusaidia namna ya kuzungumza, kwa sababu kwa mujibu wa Katiba ni kuwa sisi hatutakiwi kuzungumzia chombo ambacho ni cha Muungano.

Jengine ilikuwa kuwaje kama *TRA* inafanya kazi vizuri kweli kukawa na *ZRB*, na hii naomba nipate maelezo. Halafu mimi ninavyohisi pamoja na serikali kuwa inajitahidi sana kukusanya mapato lakini mapato haya ambayo ni mengi na serikali hivi sasa inajiimarisha kutokana na mapato ambayo yatakuwa ya uhakika yale itakuwa hakuna kupanda na kushuka mapato yaliyokusanywa, lakini kodi hizo masikini za Mungu ni wananchi wa nchi hii. Nchi hii ambayo ni visiwa, nchi hii iliyozungukwa na bahari, nchi hii iliyo na samaki ambao nasikia wengine wanapazwa, hivyo miaka 50 hivi sasa tunajitunisha na kusema kuwa tutasherehekea sherehe za Mapinduzi za miaka 50 katika sherehe ya aina yake na serikali imejiandaa, hatuoni kuwa miaka yote hiyo 50 kukaa mpaka leo katika visiwa hivi na rasilimali ya bahari tuliyonayo ikawa hatuna hata kiwanda kimoja cha kusindikia samaki ni kama kushindwa

kufanya kazi zetu. Kama ingelikuwa tuna viwanda mfano kama cha samaki Mhe. Naibu Spika, na ninaamini kingelikwenda kwa kuzalisha, rasilimali ipo ya kutosha na tungelipata faida kubwa, hatuoni kuwa watu wetu wengi wangelipata ajira na nchi hii ingelinufaika na hata kwa kupata lishe bora. Kwa sababu samaki ni *first proteinous* hata kuliko nyama yenyewe inashindwa na mboga mboga tu.

Mhe. Naibu Spika, tuna matunda ya kila aina, kuna ulazima gani wa kuagizia *juice* kutoka Arabuni wakati matunda yaliopo hapa hata hayako huko, hatuwezi kuwa na viwanda hivyo, hatuoni kuwa tukiwa na viwanda vyetu wenyewe vinavyozalisha kwa wingi wakati rasilimali zipo tutawapunguzia kodi wananchi wetu kwa watu hawa milioni moja wakaweza kujiendesha vilivyo, tutaweza kuitunza elimu, tutaweza kuendelea na mambo yale yale ya muasisi wetu marehemu Mzee Abeid Amani Karume kuwasomesha watu bila ya malipo, tungeliweza kupata matibabu ya hapa bila ya malipo na kadhalika mambo yote yametushinda kwa sababu hatukuwa *creative* na tukaweza kuliendesha taifa hili vilivyo. Naomba radhi kwa haya ninayozungumza Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, serikali ni ya Mhe. Rais na Mhe. Rais anagawa serikali katika wizara ili kazi ifanywe ipasavyo. Mtendaji au Msimamizi Mkuu wa wizara ni Mhe. Waziri, uwezo wa Waziri ni muhimu katika wizara hivyo hebu tuangalie, samahani sana Mheshimiwa kwa sababu nasema kwa nia safi kwa sababu naumia, Wizara kama ya Kilimo na Maliasili ambayo ndio tegemeo letu kutuletea maendeleo tukilima vizuri, tukivuna vizuri tutapunguza kuagiza chakula kutoka nje na uchumi wetu utakua hatuoni kuwa ipo haja Mhe. Rais kuweka mtu anayefaa badala ya kumuweka mgonjwa ambaye hawezi kufanya kazi tukamuachia Wizara Naibu Waziri na watu anao tele hivi tutaendelea kweli.

Kwa hivyo, pamoja na hili natoa indhari kwa Mhe. Rais afanye *researching* ya Wizara kwa kuona kuwa na mtu anayeweza kuendelea kwa maslahi ya nchi hii. Mhe. Naibu Spika, nashukuru.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti iliyopo mbele yetu. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima wa afya lakini pia kwa kutuwezesha kukutana hapa na kujadili mambo ambayo yanahusu taifa letu la Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, na mimi niungane na wenzangu kwa kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuiandaa hii bajeti lakini pia kwa kufika umri wa miaka miwili na nusu sasa. Mhe. Naibu Spika, moja kwa moja nikiingia katika bajeti hii nitajaribu kuangalia baadhi ya vipaumbele ambavyo Mhe.

Waziri ameviainisha katika hotuba yake ya bajeti pamoja na hivi vitabu vyengine viwili.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuanzia ningelianza na kipaumbele cha Programu ya Ajira kwa Vijana. Mhe. Naibu Spika, kama tunavyojua katika nchi yetu tuna tatizo kubwa sana la ajira hasa kwa vijana. Mhe. Waziri ametuonesha katika kitabu chake cha pili miradi mbali mbali ambayo inalenga kuwasaidia vijana ili wajinasue na tatizo la ajira, kwa bahati mbaya miradi mingi imo lakini fedha zilizotengwa shilingi 1.1 bilioni ambazo zinalenga kuwasaidia vijana 1,180. Tukiangalia uhalisia hasa uliyooneshwa wa ukosefu wa ajira kwa vijana ni vijana laki moja hawana ajira katika nchi yetu hii ya Zanzibar. Kwa hivyo, mimi ningeliomba Mhe. Waziri akaliangalia tena upya kutokana na ugumu wa ajira za vijana wetu kwani kuwasaidia vijana 1,180 kwa mwaka ambapo jumla ya vijana wote ni laki moja ambao hawana ajira. Hivyo Mhe. Waziri ningelimuomba sana hapa tukaangalia tena katika hili tukaongeza angalau kidogo vijana nao wakaongezewa katika hizi ajira ambazo zinategemewa kupatikana.

Mhe. Naibu Spika, suala la pili ambalo limepewa kipaumbele ni suala la elimu. Katika bajeti iliyopita suala hili nalo pia lilikuwemo ambalo kwa mwaka huu limetengewa jumla ya shilingi 32.8 bilioni. Mimi ningeliishauri serikali hasa kupitia hii Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwamba fedha hizi zilizotengwa zaidi zingelilengwa katika kuwapa uwezo wanafunzi ambao wanasoma katika skuli za msingi. Kwa sababu tunaona kwamba matatizo makubwa hasa ya elimu ya Zanzibar yako katika msingi. Wanafunzi wetu wengi wanapofika kiwango cha sekondari wanakuwa hawana uwezo kabisa, tumeshuhudia mara kwa mara miradi mbali mbali inayoendeshwa katika nchi yetu hii inahusu katika elimu ya maandalizi na elimu ya msingi, lakini bado wanafunzi hawajaweza kubadilika. Kwa hivyo, serikali ingelibuni mbinu mpya namna gani ya kuweza kuwasaidia wanafunzi hasa wa msingi ili waweze kukabiliana na masomo ya sekondari.

Mhe. Naibu Spika, vile vile serikali kwa kutumia fedha hizi ingelijaribu kuimarisha zaidi elimu za ufundi. Kwa sababu kama tunavyoona tatizo la ajira ni kubwa, kwa hivyo endapo serikali itajikita zaidi huku basi tatizo la ajira lingelipungua kutokana na kwamba vijana wengi wangeliweza kujiajiri wenyewe baada ya kupata masomo mengine ya ufundi.

Mhe. Naibu Spika, suala jengine ambalo limepewa kipaumbele katika bajeti hii ni Usambazaji wa Maji. Mhe. Naibu Spika, programu ya usambazaji maji kila siku inapewa kipaumbele lakini kipaumbele hiki naona hakifikii malengo yoyote. Mwaka jana vilitajwa vijiji kadhaa ambavyo viliambiwa vitanufaika na mradi wa maji lakini matatizo haya bado ni makubwa sana katika vijiji

vyetu. Fedha nyingi zinatengwa kwa ajili ya usambazaji maji lakini maji yenyewe hayaonekani. Kwa hivyo, baadhi ya Waheshimiwa Wawakilishi waliopata fedha za Mfuko wa Jimbo zinazomaliza muda wake hivi sasa wametumia angalau shilingi milioni kumi na ile jitihada yao imeonekana katika usambazaji wa maji, lakini miradi mingi mikubwa inafanywa wanatumia fedha nyingi na hakuna linalowezekana kufanyika. Kwa hivyo, serikali ingelibuni mbinu nyengine mbadala labda katika ugavi wa pesa hizi ili ziweze kufanyiwa yale yaliyokusudiwa na wananchi wetu wakaepukana na tatizo la maji.

Sasa hivi tuna miaka 50 ya Mapinduzi ya Zanzibar lakini tatizo la maji hatujaweza kulitatua. Kwa hivyo, hii ni hatari kabisa na haioneshi kwamba hiki kitu kimepewa kipaumbele kama kilivyoandikwa katika vitabu vyetu.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka kwa haraka haraka nije katika vyanzo vya mapato ambavyo Mhe. Waziri ametuonesha ni vingi vile tumeviona, lakini vyanzo vya mapato hivi vyote vinamgusa mwananchi mwenyewe ndio achangie vyanzo hivyo. Kwa hivyo, hili litatuongezea ugumu wa mafuta, hivyo serikali ingekaa ikabuni mbinu nyengine mbadala.

Juzi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamekwenda nchi za nje huko na kwa taarifa tulizopewa kwamba wamesema Zanzibar kuna uwezekano wa kupatikana gesi nyingi sana na wakashauriwa kwamba ikiwezekana waanze taratibu za uchimbaji wa gesi hizo. Mimi nadhani serikali katika bajeti ijayo ingeelekeza zaidi katika masuala ya kula gharama lakini tuhakikishe kwamba kunapatikana uchimbaji wa gesi, ili itupunguzie tatizo la ajira kwa vijana wetu lakini pia katika kuongeza kipato ambacho hakitotokana na kodi ya moja kwa moja kutoka kwa wananchi.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho tukiangalia vitabu vyetu hivi kuna mapendekezo ya hatua za kuimarisha mapato. Miongoni mwa hatua ambazo Mhe. Waziri ametueleza katika kitabu chake hiki ni kufanyiwa marekebisho kwa sheria mbali mbali. Hii ni nzuri na naipongeza jitihada hii, ila ninavyoamini mimi kwamba sheria zilizopo hazitoshi lakini zinakidhi haja kwa kiasi kikubwa katika kuimarisha mapato. Tatizo liliopo na hili si jambo la kuficha kwamba mapato mengi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar yanaingia mifukoni mwa baadhi ya watendaji ambao si waaminifu, na bado serikali haijakubali kuwawajibisha watu hao na sisi hatujui ni kwa sababu gani, fedha zilizotengwa kwa bajeti ya mwaka huu ninavyoamini mimi kama zitasimamiwa zidhibitiwe kwa watu waliokuwa sio waaminifu basi mara mbili yake fedha hizi zingelipatikana. Lakini serikali siku zote tunaiambia, wanaelekezwa, wanaoneshwa bado hawajakubali kabisa kubadilika wao na

kuwawajibisha baadhi ya watu ambao wanavuruga fedha za wananchi pasipo na sababu zozote za msingi.

Mhe. Naibu Spika, mimi naona bora nimalizie hapa naona ulinihimiza katika muda wako naunga mkono hoja iliyopo mbele yetu.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nami nakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuweza kutoa mawazo yangu katika kuchangia bajeti hii ya serikali. Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijaalia kusimama katika Baraza lako tukufu katika kuchangia bajeti hii.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kwa hotuba yake nzuri aliyoiwasilisha siku ya Jumatano, tarehe 12/06/2013. Mhe. Naibu Spika, hotuba hii ni nzuri inatuonesha mwanga wa matumaini na mafanikio makubwa mwaka huu kwa Wazanzibari wanyonge wanaotegemea majaaliwa ya Mungu na serikali kusaidia kufikisha utoaji wa huduma kwa wananchi wake.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea katika mchango wangu huo kwa vile mimi ni Mwakilishi ambaye natoka katika jamii ya wavuvi wa Zanzibar, na kwa sababu wavuvi nao ni sehemu ya nguvu kazi ya taifa wanaochangia pato la taifa, wanahudumia wananchi katika masuala mbali mbali ya maendeleo na ustawi wa jamii sitoacha kugusa eneo hilo.

Mhe. Naibu Spika, kama ilivyozungumzwa katika ukurasa wa 26 ambapo kitabu hiki cha bajeti kinazungumzia katika kuimarisha uvuvi wa bahari kuu na ufugaji wa mazao ya baharini. Mhe. Naibu Spika, jambo hilo ni zuri hata bajeti ya mwaka jana ilizungumzia, kutoka katika uvuvi wa kienyeji kuelekea katika uvuvi wa bahari kuu. Lakini Mhe. Naibu Spika, mpaka hivi sasa nazungumza jambo hili sioni matarajio mema, sioni kama kuna muelekeo wa kuweza kufikia huko tulikokusudia. Kwa nini nikasema hivyo? Ninasema hivyo kwa sababu za msingi, tumejaribu sana hapa kuwachukua wananchi wetu ambao ni wafugaji wa mifugo ya samaki na kuwapeleka China kwenda kupata taaluma, lakini inasikitisha sana Mhe. Naibu Spika, kwa kweli ukitembelea mabwawa yanayofugwa samaki imebakia zile kuta tu, hakuna chochote cha kuweza kuleta maendeleo.

Mhe. Naibu Spika, tumetumia gharama kubwa kuwapeleka wananchi wetu huko na wala wanaokwenda kujifunza wakirudi hapa hatuwatembelei tukajua maendeleo yao yamefikia kiasi gani. Hili ni jambo ambalo linaturejesha nyuma siku hadi siku.

Mhe. Naibu Spika, asubuhi hapa mama yangu Mhe. Asha Bakari Makame alizungumzia kwamba bajeti ya Idara hii iliyotengwa ni shilingi milioni mia moja, ni jambo la kusikitisha sana. Mimi niulize hivi tunakusudia kuwanyanyua wavuvi au kuwakandamiza? Kwa nini nikasema hivyo, nina sababu za msingi, shilingi milioni mia moja tuna wavuvi wasiopungua laki mbili utaweza kumsaidia nani. Hili ni jambo la kusikitisha sana, ukiiangalia sekta ya uvuvi nadhani ni sekta binafsi ambayo ni sekta mama kabisa. Sekta hii imebeba mambo mengi sana, imebeba ajira binafsi kwa watu wengi wakiwemo wavuvi, wachuuzi wenyewe, wafanyabiashara ndogo ndogo za kila kitu mpaka kutengeneza samaki lakini mnachukulia kama jambo la masihara.

Mhe. Naibu Spika, kujipanga katika kuelekea kwenye uvuvi wa Bahari Kuu nadhani tunaweza kuleta meli moja tu na meli moja haizidi mabaharia 30 au 32, wavuvi wetu ni wangapi. Kwa hivyo, mimi nadhani kwanza tuimarishe wavuvi wadogo wadogo haya ndio tuliyoyazowea na ndio yanayotuletea tija na kuchangia pato la taifa.

Mhe. Naibu Spika, nakwambia katika wavuvi wangu wa Kisiwa cha Kojani ushuru unafikia shilingi milioni moja kwa miezi miwili, hii hata ukitakiwa ushahidi nitaleta risiti zao lakini ni watu ambao hawapati msaada wowote katika Idara ya Uvuvi au katika kuwajenga wavuvi. Sasa kama kweli tumekusudia huko basi lazima tuwe tumejipanga vizuri kweli kweli kuweza kuwasaidia wavuvi wetu na kufikia huko tulikokusudia. Mimi nadhani tuna boti zetu pale ambazo ni mraba hizi za kawaida tu, hazipungui watu 70 wanakwenda baharini, *Alhamdulillah* ukifika msimu kila mtu anapata riziki yake ya kwenda kujiendeshea maisha yake lakini bado hatuwajali, hatuwaboreshi tukawajenga vizuri wakafanya kazi.

Kulikuwa na Mradi wa *MACEMP*, mradi huu ulikuwa ukikandamiza wavuvi tu haukuwajenga wavuvi, ulikuwa unawadhibiti wavuvi. Leo mvuvi unasema unataka kumboresha unakwenda kutia nyavu zake moto huyu unamboresha au umemuumiza kabisa, haipendezi kabisa lazima katika kujipanga tuangalie. Mimi hii siipigi sana hapa leo nitakuja kuizungumza siku ya bajeti ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi, nitakuja kuwafahamisha vya kutosha hapa wajue twende sambamba na wakitaka kwenda sambamba na sisi tutajua. Kuna wataalamu waliosomea uvuvi lakini kuna wazoefu wa uvuvi ambao ndio sisi. Hilo moja.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo nakwenda katika Sensa ya Watu na Makaazi katika ukurasa wa 20 na idadi ya watu. Tumefanya sensa na Rais wa Jamhuri ya Muungano katoa takwimu ya sensa hii, Tanzania ina watu wasiopungua 44,928,923 milioni, Zanzibar kuna watu 1,303,569. Watu wanaoishi Unguja ni 896,721 na watu wanaoishi Pemba 406,868. Mhe. Naibu

Spika, katika hesabu hii ina ukweli gani ukizingatia kwamba Watanzania wengi hasa Waislamu waligoma kujiandikisha kwa sababu zao za msingi.

Mhe. Naibu Spika, watu wengi walikosa kujiandikisha kwa sababu zao za msingi kwa kukosa tu kile kipengele cha kuingiza dini basi watu wengi walirudi kujiandikisha na wengine kukosa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi ilikuwa ni *issue* kwa kukosa kujiandikisha na kukosa haki zao za msingi. Sasa hapa nadhani tumejifundisha mengi kutokana na huko tunakokwenda. Mimi nasikitika sana Mzee wa watu Mhe. Mwinyihaji Makame anatusakama ndani ya Baraza la Wawakilishi lakini watendaji wanaopewa vigezo hivi hawatumii haki za msingi. Ni juzi tu tulipokuwa *Zanzibar Beach Resort* hapo, katika kujenga uelewano watendaji pamoja na muhimili huu wa Baraza la Wawakilishi, sasa kutokana na hapa kuwa tunatafuta maendeleo sote tubadilike kama alivyosema Rais, kama hatujabadilika hatufiki popote.

Mhe. Naibu Spika, kama hatutoondoa ubinafsi basi katika safari zetu zote tunazozunguka tutazungumza hapa, tutakula fedha za wananchi na hatutofika popote. Sasa niwaambie rasimu tayari imeshasomwa na Mhe. Jaji Warioba, rasimu hii imeelezwa na ina mambo mengi mazuri yanayokubalika na mengine mabaya ambayo hayakubaliki. Wazanzibari tuna msemo tunasema kuwa tuwe na mshikamano, utulivu na amani. Mimi nadhani tunao lakini tusije tukatengana kwa hili, kama kweli Wazanzibari tuna mshikamano hapa ndipo pahala pake pa kushikamana katika hatua tuliyofikia, kama si hivyo tutakuwa tunatwanga maji katika kinu hayakai. Tushikamane tuitetee nchi yetu tupate mamlaka kamili ya nchi ili tuweze kujiendesha wenyewe. Kuna mambo mengi tunakosa ambayo ni ya msingi kabisa katika nchi hii, hizi ni nchi mbili huru zilizoungana hatuangalii wingi wa nchi tunaangalia nchi na nchi, tukifika hapo tutakuwa Wazanzibari tumejikomboa vya kutosha.

Mhe. Naibu Spika, hali ya uchumi tumesema inakua, tunategemea kukua kwa asilimia 7.5 katika mwaka 2013, ukiangalia kutoka ukuaji wa asilimia 7.0 mwaka 2012. Lakini katika kukua kwa uchumi unaangalia na vigezo, hivi tuseme uchumi wetu umekua tunaangalia hali ya wananchi wetu iko vipi, ukiangalia mwananchi wa kawaida mlo wa mara tatu hautimizi ni tatizo halafu tunajidai na kujinasibu kwamba uchumi umekua. Hilo ni tatizo. Tukiangalia makaazi ya wananchi wetu si mazuri, uchumi katika nchi unaokua basi hata makaazi ya wananchi wao yanakuwa mazuri lakini sisi ukiangalia ni *dhofu-lhali* kabisa.

Mhe. Naibu Spika, tukiangalia katika sehemu za uchumi hakuna mshikemshike, lakini angalia leo tunatoa matabaka mabaya katika wafanyabiashara wa Darajani jambo ambalo linatia uchungu sana. Baada ya

kuwapa elimu na kuwafahamisha vya kutosha leo tunawatengea askari wa vikosi wanakwenda kuwafukuza pale Darajani na wakiingia tu wanatoka mbio na wakitoka mbio mali zao zinachukuliwa zinafilisiwa, hatujui mali hizo zinapelekwa Mahkamani au vipi. Mimi nadhani wanagawana wenyewe kwa wenyewe tu hii ndio sera iliyoko, na ni wengi tu mali zao zimechukuliwa. Sasa hii inamuandaa mwananchi au inamuumiza.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu muda hautoshi na mwenzangu anataka apate angalau kidogo na muda unakwisha naomba niishie hapo na mimi nasema naunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Nashukuru Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi hii kuchangia bajeti hii. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa kutuletea Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2013/2014. Kwa mwenendo huu wa uchumi wa Zanzibar nawapongeza sana hawa ndugu zetu wa *ZRB* kwa kazi nzito yenye changamoto nyingi.

Mhe. Naibu Spika, nije kidogo kwenye pato la taifa letu, pato letu kubwa limeongezeka hasa kutokana na uwekezaji hawa kwa hawa wenye hoteli za kitalii. Imekuwa ikiongeza pato kubwa la taifa hili la Zanzibar kufikia asilimia 6.7 mwaka 2011 na asilimia 7.0 mwaka 2012 katika kitabu hiki cha bajeti ukurasa wa 8.

Kama unavyojua Mhe. Naibu Spika, roho ya nchi yetu hii ni Sekta ya Utalii, lakini sasa kuna matatizo kidogo kwa wananchi wetu ambao tuwaangalie upande huu na upande mwengine hasa kuangalia hawa wenye mahoteli makubwa kama *five star hotel.* Kwa kweli Mhe. Naibu Spika, hawa hawalipi kodi inavyotakiwa hasa na kuweza kufikia makadirio yetu. Kodi wanayolipa ni ndogo wanaangalia sana kubajeti kodi wanayotaka kulipa wao wenyewe. Wawekezaji wetu hawa wadogo wadogo wa hoteli ndogo ndogo hizi unakuta wanalipa kodi karibu na hawa wa *five star hotel.* Kwa hivyo, naomba hawa *ZRB* wajitahidi sana kuwaangalia wawekezaji wakubwa kwa sababu wanakuja hapa kuchuma fedha za kigeni kwa ajili ya maslahi yao na wananchi wanyonge wa nchi hii wanashindwa kupata mahitaji muhimu.

Mhe. Naibu Spika, suala hili sijui serikali imefikia wapi, kwa nini kodi hizi zisilipiwe kupitia benki, isiwe kwenda pale kwenye ofisi kulipia hizi kodi iwe mambo ya mtandao hata kama watu wana fedha kwenye simu zao sasa hivi. Kwa hivyo utaratibu maalum wa kulipia kodi yetu hii kwa kupitia *slip* ya Benk ili waende pale kama mmeshalipia kodi ambayo ili kupunguza upotevu wa fedha.

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme mfano mdogo tu hapa mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano na tumekwenda *Airport* na Kamati yetu na tumeona upotevu wa fedha pale ule utendaji wa kupiga muhuri. Kwa hivyo inakuwa hazijulikani zile fedha uhakika hasa inakuwa vipi. Kwa hivyo, ukitizama pia Shirika moja hili juzi juzi tu *Precision Air* limefungiwa na *ZRB* kutokana na kodi hawalipi ipasavyo kwenda kwa Serikali. Kwa hivyo *ZRB* ikawafungia ofisi zao pale na ukienda mpaka hivi sasa ni aibu Mhe. Naibu Spika, hawa *Precision Air* wanalipa kodi wanachukua pesa zao za mauzo mbali unakwenda ndani sasa kulipa kodi ile ya Serikali tunarudi nyuma sasa upya. Kwa nini wasichukuliwe hatua za kisheria kama wanadaiwa na hawalipi kodi ipasavyo kwa sababu kodi wanachangia wananchi.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye suala la risiti kama tunavyojua risiti ni tatizo kubwa kwa wafanyakazi wetu hawa wakubwa wakubwa. Saa nyengine wanakwambia hivi hivi kama unataka kulipa *VAT* basi sikupi risiti utakuwa hulipi *VAT*. Lakini utakuta hawa wafanyakazi wetu wadogo wadogo unakwenda pale lakini wanalipishwa kodi ipasavyo. lakini wafanyakazi wakubwa wanawalipisha wateja wao kwa kupitia ile risiti ambayo wanaitaka wao, naomba hili pia lichukuliwe hatua zaidi nzuri kwa hawa wafanyabiashara wakubwa wakubwa waangalie zaidi vizuri. Ni kama mfano wetu wafanyabishara wengi wadogo wadogo wamehama hapa Zanzibar wamekwenda kufungua biashara zao Tanzania Bara na wamefaidika na sasa hivi wako mbali sana.

Pia tuushukuru Muungano huu wa Serikali zetu mbili hizi kuwaweka hawa vijana wako kule wanafanya biashara zao na sasa hivi wanapata riziki zao kikamilifu na Mwenyezi Mungu aujalie Muungano wetu huu uendelee na udumu maisha. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nasema hivi hawa wafanyabishara wadogo wadogo wapunguziwe kodi juzi juzi tu hapa Mhe.Naibu Spika, alikuja Rais wa China lakini kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu alitusaidia dola milioni 10 kwa kupitia Zanzibar ni kama mfuko wa mradi wa Maendeleo. Kwa hivyo, hizi zingetukidhi kwa wafanyabishara wadogo wadogo pia msamaha wa kodi, tukijua kwamba tumesaidiawa dola milioni 10. Kwa hiyo mimi naomba tuangalie sana Mhe. Naibu Spika, hawa wafanyabiashara wadogo wadogo kwa sababu mwisho wa siku watakuja kukimbia watakwenda Tanzania Bara wote itakuwa haya maduka yatakuwa mengine matupu watakuwa hamna wafanyabishara.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia kwenye kitabu hiki cha Bajeti kimesema kwamba pato la mtu mmoja kwa mwaka ni laki tisa na sitini elfu sisemi mbaya lakini bado nasema ni kidogo sana kulingana na maisha na hali

ilivyokuwa ngumu ya maisha haiwakidhi kwa pesa hizi mahitaji yao. Tukiangalia suala hili la bei ya mafuta Mhe. Naibu Spika hapa kunaonekana kuna uongezeko la bei ya mafuta lita 35 kuongezeka, pia na hili tuliangalie hawa wananchi wetu wanyonge tunawaongezea gharama zaidi. Hata tukitizama gharama za nauli sasa zitakuwa zinaongezeka tena kwa mnyonge wa chini sasa hivi nauli haiwezi.

Mhe. Naibu Spika, tizama mfano mdogo tu kama Jimbo langu la Bububu nimefanya utafiti na nimeona kuna wanafunzi hawawezi hata kupanda usafiri kuja mjini kulipia nauli wanashindwa wazazi wao, wanashindwa kuwapa fedha za kufika skuli. Kwa hivyo, naomba Mhe. Naibu Spika, hili pia liangaliwe kwanza mafuta kutokana na hali ya wananchi wetu hali zao ziko duni sana. Tukiangalia pia usafiri nao muhimu hawa watoto ni muhim. Hawa watoto taifa letu la kesho kama hawajaweza kusoma watoto nafikiri itakuwa taifa la kesho hata humu Barazani tutakuwa tunapata tabu sana kutafuta Wawakilishi waliokuwa wazuri na wema kabisa.

Tukiangalia pia suala la wagonjwa wetu kama jimbo langu la Bububu kwa kweli hali zao ni ngumu hawawezi hata kukodi usafiri wanakuwa wanashindwa, kama kuna gari pale ya kubebea wagonjwa unamchukua mgonjwa unampeleka mpaka Mnazi Mmoja akifika Mnazi Mmoja hasa mjamzito anaambiwa atoe elfu thalathini aweke pale halafu apate huduma ile inayotakiwa. Kwa kweli, hilo pia swali Mhe. Naibu Spika, tuliangalie kwa wananchi wetu gharama zilizokuwa za ziada.

Mhe. Naibu Spika, tukiangalia hata hizi kodi sasa hivi zinaongeza ukija huku *ZRB* kodi sawa tunaelewa. Lakini na Manispaa ndugu zetu pia wanalipisha wananchi ukiweka gari sasa hivi pale unaambiwa kuwa lete 300. Kuna wafanyabiashara wetu wadogo wadogo pale Darajani kuna Mjumbe alichangia hapa namshukuru sana kama hawa wananchi wanapata rizki zao kupitia pale, lakini utakuta Manispaa wanakwenda wanawanyang'anya bidhaa zao wanachukua utafikiri wananchi atafanya nini? Atafanya kazi gani na wananchi wengi na wanasikitikia wananchi wangu wa jimbo la Bububu wanafanya kazi pale.

Kwa hivyo, naomba Mhe. Naibu Spika, hili la Manispaa waangalie na hizi kodi ndogo ndogo ikiwezekana waziondoshe kwa sababu hatujui hizi fedha zinakwenda wapi, kama zinakwenda sehemu husika au wanatia mifukoni mwao tu. Inakuwa kama tunawafanyia wao mitaji yao tu kwa kupitia wananchi wetu kuwatoza kodi za ajabu ajabu.

Mhe. Naibu Spika, suala moja muhimu sana tuliangalie hawa walimu wetu wa skuli na madaktari kwa kweli hali zao ni duni sana, tufanye kila bidii

tuwaongezee mishahara yao. Lakini hapa nashukuru sana Mhe. Waziri kutuongezea wanasiasa pesa zetu hiyo namshukuru sana kwa sababu tuna hali ngumu katika majimbo yetu. Hilo Mhe. Waziri wa Fedha nakushukuru sana kwa kuliona hilo.

Mhe. Waziri wa Fedha pia nakupongeza sana pamoja na Mhe. Rais wa Zanzibar katika ukurasa wa 30 kuliona hili kulipa kipaumbele sekta ya elimu kwa kulipa milioni 32.8 sekta ya Afya milioni 23.9 na hili suala la maji safi na salama milioni 54 kulipa kipaumbele nakupongeza sana na nakushukuru sana. Mhe. Naibu Spika, hili suala linataka usimamizi wa hali ya juu na tuwe wakweli kwenye suala hili kulipatia ufumbuzi kwa haraka. Mhe. Naibu Spika, nakwenda haraka haraka nimalize muda wangu muda umebakia mdogo. Lakini hili la Sekta ya viwanda. Kitabu cha bajeti ukurasa wa 9 tumeambiwa sekta imekuwa ya viwanda hapa Zanzibar lakini ukitizama imekuwa kwa asilimia 9.2 mwaka 2012. Lakini mimi najiuliza hapa Zanzibar kuna viwanda, mimi nafahamu kwa ufahamu wangu Mhe. Naibu Spika, kuna viwanda vya aina mbili kuna viwanda vikubwa wasipungue waajiriwa 200 na kuna viwanda vidogo wasipungue waajiriwa 50.

Mhe. Naibu Spika, juzi kulikuwa na semina kule shamba tulifanyiwa vilitajwa viwanda vya kokoto na matofali. Je, Mhe. Waziri wa Fedha viwanda hivi kweli vinaweza kweli kuitwa viwanda? Naomba utoe ufafanuzi kidogo, na viwanda hivi vya kokoto na matofali Serikali inakusanya kodi kiasi gani kwa viwanda hivi vya matofali na kokoto tunaomba ufafanuzi Mhe. Waziri kujua hali halisi.

Mhe. Naibu Spika, kama tunavyojua nchi yetu imezungukwa na bahari pande zote kuna bahari kwa nini tusijikite katika viwanda vya kusindika samaki kwa sababu vijana wetu wengi hawana ajira wapo tu mitaani na uwezo huo upo wa kutafuta wafadhili watu binafsi ili kuweza kufanikisha suala hili.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie na sekta ya kilimo. Katika sekta ya kilimo imeshuka asilimia 2.7 mpaka kufikia asilimia 1.3% mwaka 2013 inasikitisha sana. Mhe. Naibu Spika, ardhi tunayo nyingi iko wazi lakini wananchi wetu hawawezi kulima, hata ukitizama eneo la Pemba kuna eneo kubwa sana la kilimo lakini wananchi hawawezi kulima. Lakini tuondokane sasa hivi kwa suala la kutumia yale majembe nafikiri wananchi wetu wangepatiwa matrekta ya kutosha nafikiri angejikita kwenye masuala haya ya kilimo na kilimo chetu kingependa kwa asilimia kubwa sana. Sidhani Mhe. Naibu Spika, kwamba sekta hii itashuka tukiwapatia dhana hizi za matrekta na vifaa mbali mbali vya kisasa vya kulimia kwa wananchi wetu tuondokane na zile za kutumia jembe ni mambo ya kizamani.

Mhe. Naibu Spika, mimi na wananchi wangu wa jimbo la Bububu tunaunga mkono asilimia mia juu ya mia ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Ibrahim Makungu kwa mchango wako. Waheshimiwa Wajumbe kabla sijaakhirisha naomba niseme mambo mawili.

Jambo la kwanza nimepewa taarifa sasa hapa kwamba za kusikitisha Mhe. Amina Iddi Mbarouk kafiliwa na mama yake mzazi na maziko yatakuwa kesho saa kumi pale pale kwake Mombasa. Kwa hiyo tunampa pole kwa niaba ya Baraza.

Pili, Wajumbe wetu wote walikuwa 37 lakini tayari 34 wameshachangia kabaki Mhe. Naibu Waziri wa Afya Dr. Sira Ubwa Mamboya atachangia kesho asubuhi, Mhe. Mussa Ali Hassan na Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi, baada ya masuali.

La msingi zaidi kwamba kesho tunategemea tumalize hotuba yetu hii kwa kufanya majumuisho Mhe. Waziri. Sasa nasisitiza tu tuna kawaida kwamba Waziri akifanya majumuisho Mjumbe hayupo wakati wa kupitisha vifungu mtu anapiga buti. Sasa tunaomba kila aliyechangia kesho aje mapema asikilize hoja zake, tutamruhusu kupiga buti yule ambaye imejibiwa hoja hayupo hatumpi nafasi hiyo.

Baada ya matangazo hayo naakhirisha kikao chetu hadi kesho siku ya Jumatano tarehe 19/06/2013 saa 3:00 za asuhubi.

(*Saa 1:43 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 19/06/2013 saa 3:00 asubuhi)*